

MUHTASARI WA RIPOTI YA DUNIA YA UFUATILIAJI WA ELIMU

2019

# Uhamiaji, ufurushwaji na elimu:

## KUUNGANISHA JAMII BADALA YA KUIGAWANYA

UNESCO
United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

Sustainable
Development
Goals

Global
Education
Monitoring
Report

MUHTASARI WA RIPOTI YA DUNIA YA UFUATILIAJI WA ELIMU

2019

# Uhamiaji, ufurushwaji na elimu:

KUUNGANISHA JAMII BADALA YA KUIGAWANYA

Azimio la Incheon la elimu la 2030 na Mfumo wa Utekelezaji zinabainisha kuwa mamlaka ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu ni kuwa "utaratibu wa kufuatilia na kuripoti juu yaLengo nambari 4 katika Maendeleao Endelevu (SDG 4) na juu ya elimu katika malengo mengine" Wajibu wake ni kuripoti kuhusu utekelezaji wa mikakati ya kitaifa na kimataifa ilikuhakikisha kuwa washirika wote husika wanatimiza ahadi zao kama sehemu ya ufuatiliaji naukaguzi wa jumla wa malengo ya SDG Ripoti hii imeandaliwa na timu ya kujitegemea kwa ushirikiano na UNESCO.

Majina yaliyotumika na uwasilishaji wa maudhui katika chapisho hili hayawasilishi maoni ya UNESCO kuhusiana na sheria ya nchi, taifa, jiji au eneo lolote lile, au mamlaka yake, au kuhusiana na uh mipaka yake.

Wajumbe wa timu hii wanawajibika kwa uchaguzi na uwasilishaji wa ukweli na maoni yaliyo katika kitabi hiki, ambayo si lazima yawe yanambatana na yale ya UNESCO na UNESCO haiwajibiki. Mkurugenzi wake anawajibika kwa mawazo na maoni yaliyotolewa katika Ripoti hii.

## Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu

*Mkurugenzi: Manos Antoninis*

Daniel April, Bilal Barakat, Madeleine Barry, Nicole Bella, Anna Cristina D'Addio, Glen Hertelendy, Sébastien Hine, Priyadarshani Joshi, Katarzyna Kubacka, Kate Linkins, Leila Loupis, Kassiani Lythrangomitis, Alasdair McWilliam, Anissa Mechtar, Claudine Mukizwa, Yuki Murakami, Carlos Alfonso Obregón Melgar, Judith Randrianatoavina, Kate Redman, Maria Rojnov, Anna Ewa Ruszkiewicz, Will Smith, Rosa Vidarte na Lema Zekrya.

Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu ni toleo huru linalochapishwa kila mwaka. Ripoti hii imegharamiwa na muungano wa serikali mbalimbali, taasisi za kimataifa na mifuko binafsi na kuwezeshwa na UNESCO.

Australian Aid
Canada
Ministry for Foreign Affairs of Finland
République Française – Ministère de l'Europe et des Affaires Étrangères
Federal Ministry for Economic Cooperation and Development
William + Flora Hewlett Foundation
Irish Aid – Rialtas na hÉireann – Government of Ireland
mastercard foundation
Open Society Foundations
Norwegian Ministry of Foreign Affairs
Sida – Swedish International Development Cooperation Agency
Swiss Agency for Development and Cooperation SDC
UKaid from the British people
UNGEI United Nations Girls' Education Initiative
UNESCO – United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization

Ripoti hii inapatikana kwa kila mtu chini ya leseni ya IGO (CC-BY-SA 3.0 IGO) ya Attribution-ShareAlike 3.0 (http://creativecommons.org/licenses/by-sa/3.0/igo/). Kwa kutumia maudhui yaliyo ndani ya ripoti hii, watumiaji wanakubali kutii masharti ya matumizi ya UNESCO Open Access Repository (http://www.unesco.org/open-access/terms-use-ccbysa-en).

Leseni ya sasa inasimamia sehemu ya maandishi pekee. Ili kutumia nyenzo yoyote ambayo haijabainishwa kuwa ni inamilikiwa na UNESCO, anayetaka kutumia atahitaji kuomba ruhusa mapema kutoka: publication.copyright@unesco.org au UNESCO Publishing, 7, place de Fontenoy, 75352 Paris 07 SP Ufaransa.

Kichwa asili kwa Kiingereza: Global Education Monitoring Report Summary 2019: Migration, displacement and education: Building bridges, not walls

Ripoti hii inaweza kutajwa kama: UNESCO. 2018. Muhtasari wa Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu 2019: Uhamiaji, Ufurushwaji na Elimu - Kuunganisha jamii badala ya Kuigawanya. Paris, UNESCO.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu ripoti hii, tafadhali wasiliana na:**
Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu
k.k UNESCO, 7, place de Fontenoy
Paris 07 SP, Ufaransa
Barua pepe: gemreport@unesco.org
Simu: +33 1 45 68 07 4
www.unesco.org/gemreport
https://gemreportunesco.wordpress.com

Makosa yoyote ya kiuchapishaji au kuondolewa kwa baadhi ya maneno yatarekebishwa kwenye toleo litakalowekwa kwenye tovuti ya www.unesco.org/gemreport

© UNESCO, 2018
Haki zote zimehifadhiwa
Toleo la kwanza
Ilichapishwa mwaka wa 2018 na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni

7, Place de Fontenoy, 75352
Paris 07 SP, Ufaransa

Mpangilio wa uchapishaji umefanywa na UNESCO
Ubunifu wa vielelezo: FHI 360
Mpangilio: UNESCO
Mpangilio wa kurasa na Apricot Business Solutions

ED-2018/WS/51

***Ripoti zilizotangulia***

| | |
|---|---|
| 2019 | Uhamiaji, ufurushwaji na elimu: Kuunganisha jamii badala ya kuigawanya |
| 2017/8 | Uwajibikaji katika elimu: Kutimiza ahadi zetu |
| 2016 | Elimu kwa ajili ya watu na dunia: Kujenga hatima endelevu kwa wote |

***Ripoti zilizotangulia***

| | |
|---|---|
| 2015 | Elimu kwa Wote 2000-2015: Mafanikio na changamoto |
| 2013/4 | Kufundisha na kujifunza: Kufanikisha ubora kwa wote |
| 2012 | Vijana na stadi: Kufanya elimu yenye manufaa kwa kazi |
| 2011 | Mgogoro ulifichika: Mapambano ya silaha na elimu |
| 2010 | Kuzifika jamii zilizoko pembezoni |
| 2009 | Kuushinda ubaguzi: Umuhimu wa utawala bora |
| 2008 | Elimu kwa Wote kufikia 2015: Je, tutaweza? |
| 2007 | Msingi Imara: Maelezi na elimu ya awali |
| 2006 | Kusoma, kuandika na kuhesabu kwa ajili ya maisha |
| 2005 | Elimu kwa Wote: Ubora ni kigezo |
| 2003/4 | Jinsia na Elimu kwa Wote: Kuelekea usawa |
| 2002 | Elimu kwa Wote: Je, dunia inafuata mwelekeo sahihi? |

Picha ya jalada: Rushdi Sarraj/UNRWA
Nukuu: Wanafunzi wakimbizi wa Palestina katika siku yao ya kwanza kwenye shule za UNRWA, muhula wa pili, huko Gaza.

Michoro: Housatonic Design Network

Ripoti hii na maudhui yote yanazohusiana yanaweza kupakuliwa hapa:
http://bit.ly/2019gemreport

# Dibaji

Watu daima wamehama kutoka sehemu moja hadi nyingine, wengine wakitafuta nafasi bora zaidi na wengine wakikimbia hatari. Harakati hizi zinaweza kuathari pakubwa mifumo ya elimu. Toleo la mwaka wa 2019 la Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu ndilo la kwanza la aina yake kuchunguza masuala haya kwa kina katika maeneo yote duniani.

Ripoti hii imetolewa kwa wakati unaofaa, kwani ndiyo jumuiya ya kimataifa inapomalizia mikataba miwili muhimu ya kimataifa: Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji Salama, wenye Utaratibu na wa Mara kwa Mara (Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration) na Mkataba wa Kimataifa juu ya Wakimbizi (Global Compact on Refugees). Mikataba hii ya kipekee - pamoja na ahadi za kimataifa za elimu zilizo katika lengo la nne la Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa - zinaonyesha haja ya kushughulikia elimu kwa ajili ya wahamiaji na waliofurushwa makwao. Ripoti hii ya GEM ni nyenzo muhimu ya kurejelewa na watunga sera wenye jukumu la kutimiza matarajio yetu.

Sheria na sera zilizopo kwa sasa zinashindwa kuwawakilisha wahamiaji na watoto wakimbizi kwa kupuuza haki zao na mahitaji yao. Wahamiaji, wakimbizi na watu waliofurushwa makwao ndani ya nchi, ni baadhi ya watu wanaokabiliwa na mazingira magumu zaidi duniani. Kikundi hiki kinajumuisha wale wanaoishi katika makazi duni, wale wanaohama kwa misimu ili kujitafutia riziki na watoto wafungwa. Hata hivyo, mara kwa mara wanakatazwa kuingia shule ambazo zinawapa usalama na ahadi ya maisha bora.

Kupuuza elimu ya wahamiaji ni kupoteza uwezo mkubwa ulio ndani ya binadamu. Wakati mwingine shughuli rahisi ya kutayarisha hati rasmi, ukosefu wa data au mifumo yenye ukiritimba na inayokosa utaratibu hufanya watu wengi kutojumuishwa katika sajili ya serikali. Hata hivyo kuwekeza katika elimu ya wahamiaji na wakimbizi wenye vipaji na ari kunaweza kuendeleza maendeleo na kukuza uchumi, sio tu katika nchi walikohamia bali hata katika nchi walikotoka.

Kutoa elimu pekee hakutoshi. Mazingira ya shule yanahitajika kurekebishwa na kukidhi mahitaji ya wale wanaohama. Kuweka wahamiaji na wakimbizi katika shule moja na wenyeji ni hatua muhimu katika kujenga ushirikiano wa kijamii. Hata hivyo, njia na lugha inayotumiwa kufundisha pamoja na ubaguzi, yanaweza kuwafanya wasijiunge na shule.


Ni muhimu walimu wawe wamepewa mafunzo yanayoyofaa ili kuhakikisha wanawashirikisha wanafunzi wahamiaji na wakimbizi. Lakini pia, walimu hao wanahitaji usaidizi ili kufunza madarasa yenye wanafunzi wanaozungumza lugha na wenye tamaduni mbalimbali, mara nyingi wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji ya kisaikolojia.

Ni muhimu kuwa na mtalaa ulioandaliwa vizuri ili kuunga mkono uanuwai, mtalaa unaowapa wanafunzi ujuzi muhimu na unaokabiliana na ubaguzi. Manufaa ya mtalaa kama huu hayataonekana darasani tu bali hata nje ya darasa. Wakati mwingine, vitabu vinavyotumiwa darasani vinajumuisha maelezo ya uhamiaji yaliyopitwa na wakati hivyo kukatiza juhudi za kuwashirikisha wahamiaji. Mitalaa mingi si rahisi kubadilisha hivyo inashindwa kuzifaa jamii ambazo zinahamahama.

Ili kuweza kuwapa elimu na kuwajumuisha watoto zaidi, ni lazima kuwe na uwekezaji, ambao nchi nyingi zinazopokea wahamiaji haziwezi kufanya peke yake. Msaada unaotolewa kwa sasa haukidhi mahitaji ya watoto kwa sababu mara nyingi ni mdogo na kutolewa kwake si hakika. Mfuko mpya wa Elimu Haiwezi Kusubiri (Education Cannot Wait) ni njia muhimu ya kufikia baadhi ya wale walioathirika zaidi.

Ujumbe wa ripoti hii ni wazi: kuwekeza katika elimu ya jamii zinazohamahama ndio uamuzi unaoweza kuelekeza kwa maisha yenye kukatisha tamaa na machafuko au maisha yenye mshikamano na amani.

Audrey Azoulay
Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO



# Dibaji

Ripoti yaDunia ya Ufuatiliaji wa Elimu ya mwaka wa 2019imeandaliwa kwa kuwashirikisha timu ya wahamiaji wa kimataifa. Wanne kati yao ni watoto wa wakimbizi. Hawakatai kuwa watu wana mitazamo tofauti kuhusu suala la uhamiaji na wahamiaji. Utafiti wao unaonyesha jinsi ambavyo elimu inaweza kusaidia kupanua mitazamo hiyo na kuwapa wote fursa kubwa zaidi.

Kuna mambo ambayo wahamiaji, wakimbizi na wenyeji wanayajua na wasioyajua. Hata hivyo, kuna watu ambao hawajui lingine ila kunyimwa na haja walio nayo ya kutoroka hali ile; hawajui kama kutakuwa na nafasi kule wanakoelekea. Wenyeji wanaowapata hawajui zile majirani wao wapya, wenye mavazi tofauti, desturi tofauti na wanaozungumza kwa lafudhi tofauti watabadilisha maisha yao.

Uhamiaji huja na sifa mbili: utaratibu na vurugu. Mara nyingi jamii zinajitahidi kudhibiti harakati za watu kuhama. Hata hivyo, jamii hizi zinaweza kupokea idadi kubwa ya wahamaji bila kutarajia. Harakati hizo zinaweza kuwagawanya watu upya, ingawa wakati mwingine zimefaidi pakubwa nchi wanakotoka na kule wanakoenda.

Watu wanapohama, kuna wale wanaojitakia na wale wanaolazimishwa. Watu wengine huamua kuhama ili kufanya kazi na kusoma, huku wengine wakilazimika kukimbia mateso na vitisho. Jamii zinazowapokea na wanasiasa wanaweza kujadili bila kukoma, ikiwa wale wanaokuja wanasukumwa au wanasukuma, ni halali au haramu, wana faida au ni tishio au ikiwa watasaidia au ni mzigo.

Kuna wale wanaowapokea na wale wanaowakataa. Watu wengine huweza kuishi katika mazingira yao mapya huku wengine wakishindwa. Kuna wale wanaotaka kusaidia na wale wanaotaka kutenga.

Kwa hiyo, kote duniani tunaona masuala ya uhamiaji na ufurushwaji yakizua hisia kali. Hata hivyo, kuna maamuzi yanayohitaji kufanywa. Uhamiaji unahitaji majibu. Tunaweza kuongeza vikwazo au tunaweza kuegemea upande mwingine, yaani, kujengaimani, kushirikisha, kuhakikishia.

Katika ngazi ya kimataifa, shirika la Umoja wa Mataifa limetia jitihada ili kushirikisha mataifa pamoja katika kuunga mkono masuluhisho ya kudumu ya changamoto za uhamaji na ufurushwaji. Katika Mkutano ulioandaliwa mwaka wa 2016 na Umoja wa Mataifa kuhusu suala la Wakimbizi na Wahamiaji, niliomba tuwekeze katika kuzuia mapigano, upatanisho, utawala bora, utawala wa sheria na kuwajumuisha wote katika kukuza uchumi. Pia nilielezea haja ya kupanua upatikanaji wa huduma za msingi kwa wahamiaji ili kukabiliana na suala la kutokuwa na usawa.

Ripoti hii inapanua zaidi hoja ya mwisho kwa kutukumbusha kwamba kutoa elimu sio tu wajibu unaotokana na maadili ya wale wanaohusika, lakini pia ni suluhisho la mambo mengi yanayotokana na watu kuhama. Lazima iwe, na inafaa tayari kuwa, sehemu muhimu ya njia za kukabiliana na uhamiaji na ufurushwaji - wazo ambalo wakati wake umefika, kulingana na yaliyoandikwa katika mikataba miwili za kimataifa kuhusu wahamiaji na wakimbizi.

Wale wanaonyimwa elimu watajiona wamebaguliwa na kukata tamaa. Elimu ikitolewa kwa njia isiyofaa, inaweza kupotosha historia na kusababisha kutoelewana.

Lakini, kama Ripoti inavyotuonyesha kupitia mifano mingi inayotia moyo ya nchi kama Kanada, Chad, Colombia, Ireland, Lebanon, Ufilipino, Uturuki na Uganda, elimu inaweza pia kuwa daraja. Inaweza kuwasaidia watu wengi na kuwafanya watupilie mbali mitazamo iliyopitwa na wakati, utengaji na ubaguzi na kuanza kuwa na umakinifu, umoja na uwazi. Inaweza kuwafaa wale waliopata mateso na kuwapa nafasi wale ambao wanaoihitaji sana.

Ripoti hii inazungumzia moja kwa moja changamoto kuu: walimu wanawezaje kusaidiwa ili waweze kuwajumuisha wanafunzi wote. Inatupa maarifa ya kushangaza kuhusu ubinadamu na suala hili la kutoka jadi la uhamiaji. Ninakualika uzingatie mapendekezo yake na uyatekeleze.

Mheshimiwa Helen Clark
Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Taarifa ya GEM



# Uhamiaji, ufurushwaji na elimu

Visa vya kuhamasisha na kusisimua vya uhamiaji na ufurushwaji hutokea duniani kote. Visa hivi vilivyojawa na tamaa, matumaini, hofu, matarajio, ujuzi, kuridhika, mhanga, ujasiri, uvumilivu na dhiki hutukumbusha kwamba 'uhamiaji ni kiashiria cha hamu ya binadamu ya kutaka heshima, usalama na maisha bora. Ni sehemu msingi ya jamii, mojawapo ya nguzo zinazotutambulisha kama binadamu Hata hivyo, uhamiaji na ufurushwaji 'pia ni chanzo cha mgawanyiko ndani na kati ya Mataifa na jamii …. Katika miaka ya hivi karibuni, kuhama kwa makundi makubwa ya watu, wakiwemo wahamiaji na wakimbizi, kumevuruga faida kubwa za uhamiaji.

Ingawa kuna majukumu ya pamoja katika kutimiza hatima yetu sote iliyoidhinishwa rasmi katika Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu, uhamiaji na ufurushwaji huendelea kuibua hisia hasi katika jamii. Hisia hizi hutumiwa na baadhi ya watu ambao wanaona faida katika kugawanya jamii badala ya kuileta pamoja. Hapa ndipo jukumu la elimu la 'kukuza uelewa, uvumilivu na urafiki miongoni mwa mataifa yote, makundi ya kikabila au ya dini', ahadi kuu katika Azimio la Umoja wa Haki za Binadamu, linachukua nafasi muhimu.

Ripoti hii inaangalia masuala ya uhamiaji na ufurushwaji kupitia macho ya walimu na wasimamizi wa elimu wanakabiliwa na suala la madarasa, shule, jumuiya, masoko ya kazi na jamii zenye watu kutoka maeneo mbalimbali. Mifumo ya elimu ulimwenguni kote imeungana katika 'kuhakikisha elimu bora inayowajumuisha wote na kwa usawa inapatikana, na kuwapa wote fursa za kujifunza' na 'kutomwacha yeyote nyuma'. Ili wanafunzi wote waweze kutimiza ahadi zao, mifumo ya elimu inahitaji kurekebisha ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi hao bila kujali asili zao. Pia inahitaji kutimiza mahitaji ya jamii 'ya kuwa thabiti na kukabiliana na masuala ya uhamiaji na ufurushwaji - changamoto inayoathiri nchi zilizo na idadi kubwa na ndogo ya wahamiaji na wakimbizi.

Aina zote za kuhama kwa watu zimejumuishwa. Kwa wastani, mtu 1 kati ya 8 ni wahamiaji wa ndani. Uhamiaji huu unaweza kuwa na madhara makubwa kwa fursa za elimu za wale wanaohama na wale walioachwa nyuma, hasa katika nchi za mapato ya chini na ya kati ambazo miji yake inaendelea kukua kwa kasi. Mtu 1 kati ya 30 wanaishi katika nchi tofauti na walipozaliwa. Karibu theluthi mbili ya wahamiaji wa kimataifa wanaelekea nchi za kipato cha juu. Ingawa wengi huhama ili kufanya kazi, baadhi pia huhamia ili kupata elimu. Na uhamaji wa kimataifa pia huathiri elimu ya watoto wao. Mtu 1 kati ya 80 hulazimika kuhamia ndani au nje ya nchi kutokana na mapigano au maafa asilia.Tisakati ya kumi, kati ya hawa huishi katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Ni muhimu kuwajumuisha katika mifumo ya kitaifa ya elimu ingawa suala hili litalingana na mazingira ya kipekee ya ufurushwaji.

Uhusiano kati ya uhamiaji na ufurushwaji na elimu una pande mbili-tatanishi na huathiri wale wanaohama, wale wanaobaki na wale ambao hukaribisha wahamiaji na wakimbizi **(Jedwali 1)**. Utambuzi wa ni wakati upi katika maisha ambapo watu wanafikiri au kuamua kuhama ni kigezo msingi katika maamuzi ya uwekezaji, ukatizwaji, uzoefu na matokeo katika elimu.Watoto wanaohama kutoka maeneo yenye viwango vya chini vya maendeleo ya elimu wanaweza kupata fursa ambazo hawangepata. Wakati huo huo, utimizaji wa malengo ya elimu na mafanikio ya wanafunzi wahamiaji mara nyingi huwa nyuma ya wanafunzi wenyeji.

**JEDWALI LA 1:**

**Mifano kadhaa ya uhusiano kati ya elimu na uhamiaji / ufurushwaji**

| | | Athari za uhamiaji / ufurushwaji kwenye elimu | Athari za elimu kwenye uhamiaji / ufurushwaji |
|---|---|---|---|
| Nchi wanakotoka | Wahamiaji | • Uhamiaji huzua changamoto za kupata bidhaa msingi katika makazi duni.<br>• Mifumo ya elimu inahitaji kurekebishwa ili kukidhi mahitaji ya watu wanaohamia katika mifumo ya msimu au ya mzunguko. | • Waliopata elimu ya juu ndio walio na uwezekano mkubwa zaidi wa kuhama. |
| | Waliobaki nyuma | • Uhamiaji hupunguza idadi ya watu katika maeneo ya vijijini na kutatiza utoaji wa elimu.<br>• Upelekaji fedha kwingine huathiri elimu katika jamii asilia<br>• Kutokuwepo kwa wazazi kunaathiri watoto walioachwa nyuma.<br>• Uwezekano wa watu kuhama hupunguza motisha wa kuwekeza katika elimu.<br>• Miradi mipya huandaa wale ambao wangependa kuhama. | • Kuhama kwa waliopata elimu huathiri maendeleo ya maeneo yaliyoathirika, kwa mfano kupitia kuhama kwa wataalamu. |
| Nchi wanakoenda | Wahamiaji na wakimbizi | • Fursa ya kupata na ufanisi katika elimukwa wahamiaji na watoto wao huwa nyuma ya wenyeji.<br>• Wakimbizi wanahitaji kujumuishwa katika mifumo ya kitaifa ya elimu.<br>• Haki ya wakimbizi kupata elimu inahitaji kuhakikishwa. | • Wahamiaji huwa wamehitimu kupita kiasi kinachohitajika, ujuzi wao hautambuliwi au hautumiwi na maisha yao huwa yamebadilika.<br>• Umataifishaji wa elimu ya juu huchochea wanafunzi kuhama. |
| | Wenyeji | • Uanuwai darasani unahitaji walimu waliotayarishwa kwa njia bora zaidi, mipango inayolengwa wanafunzi wapya ili kuwasaidia na kuzuia utengano, na data iliyogawanyika. | • Elimu ya darasani na ya nje ya darasa inaweza kujenga jamii imara, kupunguza chuki na ubaguzi. |

Uhamiaji na ufurushwaji huhitaji mifumo ya elimu ili kuzingatia mahitaji ya wale wanaohama na wale wanaoachwa nyuma. Nchi zinahitaji kutambua katika sheria haki ya wahamiaji na wakimbizi ya kupata elimu, na kutekeleza sheria hii. Wanahitaji kuhakikisha elimu inawafaa wale walio katika makazi duni, wale ni wahamahamaji au wanaosubiri kuandikishwa kama wakimbizi. Mifumo ya elimu inahitaji kuwajumuisha wote na kutimiza ahadi ya usawa. Walimu wanapaswa kujiandaa kukabiliana na uanuwai na masumbuko yanayohusiana na uhamiaji na hasa, ufurushwaji. Kuna haja ya kupiga msasa utambuzi wa sifa na mahitaji ya awali ya mafunzo ili kutumia kikamilifu ujuzi wa wahamiaji na wakimbizi, ambao huchangia sana katika ustawi wa muda mrefu.

“Uhamiaji na ufurushwaji huhitaji mifumo ya elimu ili kuzingatia mahitaji ya wale wanaohama na wale wanaoachwa nyuma”

Elimu pia huathiri sana uhamiaji na ufurushwaji - katika upana wake na jinsi yanavyotazamwa. Elimu ni kichocheo kikubwa katika uamuzi wa kuhama, kinachochangia katika juhudi za kutafuta maisha bora. Elimu huathiri mtazamo wa wahamiaji, matarajio na imani yao, na kiwango ambacho watajihisi nyumbani katika mahali walikohamia. Kuongezeka kwa uanuwai darasani kuna changamoto, ikiwa ni pamoja na kwa wenyeji (hususan maskini na waliotengwa), lakini pia hutoa fursa za kujifunza kutoka kwa tamaduni na uzoefu tofauti. Imo haja ya kuwa na mitalaa inayoshughulikia mitazamo hasi.

Masuala ya uhamiaji na ufurushwaji yamekuwa mada kuu katika ulingo wa kisiasa, na elimu ina wajibu mkuu katika kuwapa raia ufahamu muhimu wa masuala yanayohusika. Elimu inaweza kuchangua katika usindikaji wa habari na kuendeleza jamii zenye ushirikiano, masuala muhimu katika ulimwengu wenye utandawazi. Hata hivyo, elimu haifai kukomea tu katika uvumilivu, unaoweza kuonekana kama kutojali; elimu ni chombo muhimu katika kupambana na chuki, mitazamo iliyoshikiliwa tangu jadi na ubaguzi. Mifumo ya elimu iliyoandaliwa bila umakini inaweza kueneza mitazamo hasi, inayotenga, ya kipekee au isiyokubalika ya wahamiaji na wakimbizi.

Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu ya 2019 inakaguaushahidi wa kimataifa juu ya uhamiaji, ufurushwaji na elimu na inalenga kujibu maswali yafuatayo:

- Je, kuhama kwa watu huathiri vipi upatikanaji na ubora wa elimu?Je, kuna matokeo gani kwa wahamiaji na wakimbizi binafsi?
- Je, elimu inawezaje kuleta tofauti katika maisha ya watu wanaohamia na katika jamii wanakohamia?

### KISANDUKU CHA 1

#### Dunia inachukua hatua kushughulikia mahitaji ya elimu na mahitaji mengine ya wahamiaji, wafurushwaji na wenyeji

Kushughulikia mahitaji ya elimu na mahitaji mengine ya wahamiaji, wafurushwaji na wenyeji katika ngazi za mitaa, kitaifa na kimataifa kunahitaji kutafuta rasilimali na kuratibu vitendo. Dunia inachukua hatua kuelekea upande huo. Mnamo Septemba 2016, nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa walitia saini Azimio la New York kwa Wakimbizi na Wahamiaji ili kuimarisha na kuboresha mbinu za kugawana wajibu, hivyo kuanzisha utaratibu wa kufikia mikataba miwili ya kimataifa: mmoja juu ya wahamiaji na mwingine juu ya wakimbizi.

Rasimu ya Mkataba wa kimataifa wa Uhamiaji Salama, wenye Utaratibu na wa Mara kwa Mara (Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration) imejumuisha masuala mengi yanayohusiana na ripoti hii kwenye ajenda. Rasimu hiyo inazungumzia upatikanaji wa huduma msingi, ikiwa ni pamoja na elimu ndani na nje ya shule.

Ingawa imetilia mkazo suala la utambuzi wa ujuzi, ina ujumbe mzuri kwa jumlajuu ya elimu kama fursa ya kupata manufaa zaidi kutokana na uhamiaji. Hata hivyo, nchi husika haziwezi kulazimishwa kutii mkataba huu na haubainishi jinsi nchi zinavyofaa kutimiza ahadi zake.

Kuwapa waliofurushwa elimu kunahitaji msaada zaidi ili kuwasaidia watu kuweza kuishi katika mazingira mapya na kukabiliana na ufurushwaji unaodumu muda mrefu. Ingawa haki ya wakimbizi ya kupata elimu katika nchi wanamokimbilia imethibitishwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa 1951 kuhusiana na Hali ya Wakimbizi,Mkataba wa Kimataifa kuhusu Wakimbizi *(Global Compact on Refugees)* unalenga kurejesha ahadi Rasimu ya mwisho ina aya mbili zinazozungumzia elimu, na kulenga suala la fedha na matumizi yake kuendeleza sera maalum. Inabainisha wazi haja ya kubuni sera za kitaifa juu ya suala la ujumuishaji.

# Uhamiaji wa ndani mwa nchi

Inakadiriwa kuwa watu milioni 763 wanaishi nje ya eneo ambapo walizaliwa. Miongoni mwa aina mbalimbali za kuhama, kuhama kabisa au kwa muda, kati ya au ndani ya maeneo ya mijini na vijijini, ni uhamaji kutoka vijijini kwenda mijini na uhamaji kwa msimu au kwa mzunguko ambao huzua changamoto kubwa kwa mifumo ya elimu.

Katika karne ya 19 hadi katikati ya karne ya 20, watu wengi walihama kutoka vijijini kwenda mijini kutokana na ukuaji wa uchumi katika nchi za kipato cha juu, lakini leo watu wengi wanaohama kutoka maeneo mbalimbali ndani mwa nchi wamo katika nchi za kipato cha kati, hasa Uchina na India. Katika mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara, uhamaji kutoka vijijini kwenda mijini pia kumetatiza mipango ya maendeleo ya mijini.

> “Inakadiriwa kuwa watu milioni 763 wanaishi nje ya eneo ambapo walizaliwa”


Idadi ya wanaohama huwa tofauti kulingana na umri lakini huwa juu katika kikundi cha walio na miaka ishirini. Kwa upande wa elimu, uhamiaji wa ndani hauathiri watoto wengi wa shule za msingi bali huathiri vijana wa shule za sekondari. Lakini kuwepo na elimu ya ubora wa juu katika maeneo ya miji ni sababu kuu ya uhamaji miongoni mwa vijana. Katika nchi ya Thailand, asilimia ishirini na moja ya vijana walisema walihama kwa sababu ya elimu.

Wale walio na elimu ya juu wanaweza kuhamia kwingine kwa matarajio kuwa watapata kipato cha juu zaidi kutokana na elimu walio nayo (Mchoro wa 1). Mapendeleo na matarajio kutokana na elimu pia huwashawishi watu kuondoka maeneo ya vijijini bila kujali uwezo wa kupata kipato cha juu zaidi. Katika nchi 53, uwezekano wa kuhama uliongezeka maradufu miongoni mwa wale wenye elimu ya msingi, ukaongezeka mara tatu miongoni mwa wale wenye elimu ya sekondari na ukaongezeka mara nne miongoni mwa wale wenye elimu ya juu, ikilinganishwa na wale wasio na elimu.

**MCHORO WA 1:**

**Kuna uwezekano zaidi wa wale walioelimika kuhama**

*Kiwango cha kuongezeka kwa uhamaji kwa misingi ya elimu, baadhi ya nchi, vipindi vya miaka mitano, 1999-2010*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig2_3
*Chanzo:* Bernard na wengine (2018).




# Uhamaji huboresha matokeo ya elimu kwa baadhi lakini si wote

Uhamaji kwenda mijini unaweza kuongeza mafanikio ya kielimu katika nchi ambapo upatikanaji wa elimu katika maeneo ya vijijini ni finyu. Katika kikundi cha watu waliozaliwa katika vijiji fulani nchini Indonesia, wale waliohamia mjini wakiwa watoto waliendelea na masomo kwa miaka mitatu zaidi ikilinganishwa na wale ambao hawakuhama.

Hata hivyo, huenda watoto wanaohama wasipate matokeo ya elimu sawa na ya wenzao. Nchini Brazil, miongoni mwa vijana waliozaliwa mwaka wa 2000/01 katika kanda ya kaskazini, wale waliohama wakiwa shule ya sekondari hawakuweza kusonga mbele vizuri ikilinganishwa na wale ambao hawakuhama. Fursa za elimu za watoto wanaohama ndani mwa nchi zinaweza kuathiriwa na sababu kadhaa, zikiwemo hali mbaya ya kisheria, umasikini, serikali kutokuwa makini au vikwazo na ubaguzi.

## VIDHIBITI WA UHAMAJI NDANI MWA NCHI VINAATHIRI UPATIKANAJI WA ELIMU

Nchi nyingi zimebuni sera za kuzuia uhamaji kutokana na hofu ya kutoweza kuhimili ukuaji wa miji na kutokuwa na urari wa watu walio vijijini na mijini. Sera hizi zinaweza kuathiri uwezo wa wahamaji kupata elimu. Mfumo wahokhau uliofuatwa huko Viet Nam ilizuia uwezo wa wahamaji kupata elimu katika shule za umma, na wahamaji maskini wa vijijini kwenda mijini walienda katika maeneo ambayo hayakuwa na shule za umma za kutosha. Marekebisho ya hivi karibuni yanalenga kufutilia vikwazo hivyo mbali, lakini athari ya sera za awali bado unawanyima nafasi wahamaji wa muda.

Mfumo wa usajili wa hukou uliofuatwa huko Uchina , ambao ulihusisha upatikanaji wa huduma na mahali pa kuzaliwa, haukuwajumuisha watoto wa wahamaji waliotoka vijijini katika shule za umma. Mfumo huu umefanyiwa marekebisho muhimu katika miaka ya hivi karibuni. Katika mwaka wa 2006, serikali ilitaka mamlaka za mitaa kutoa elimu kwa watoto wahamiaji. Katika mwaka wa 2008, serikali pia iliwaondolea watoto wahamiaji ada ya shule katika shule za umma na katika mwaka wa 2014, ikaanza kutenganisha upatikanaji wa huduma na usajili wa mahali mtu alikozaliwa. Tangu mwaka wa 2016, serikali imekuwa ikiwaomba wote, isipokuwa miji mikubwa, wapunguze vikwazo zaidi.

Hata hivyo, bado kuna vikwazo vinavyowazuia wahamiaji kupata elimu. Hati rasmi na mahitaji mengine ya usajili yanaweza kuwa vikwazo. Katika Beijing, wahamiaji wanahitaji vyeti tano ili kujiandikisha katika shule ya umma. Walimu wanaweza kuwa na maoni ya ubaguzi dhidi ya vijana wahamiaji. Huenda walimu katika shule zisizoidhinishwa za wahamiaji wakapata malipo duni na kukosa ukakika wa kudumisha kazi yao, na mara nyingi wazazi hulalamikia ubora wa kazi ya walimu katika shule hizo.

## WATOTO WALIOBAKI NYUMA WANAKABILIWA NA MATATIZO FULANI YA ELIMU

Uhamiaji pia huathiri elimu ya mamilioni ya watoto waliobaki nyuma na mzazi mmoja au wanafamilia wengine. Nchini Cambodia, kulikuwa na uwezekano mkubwa wa watoto waliobaki nyuma, hasa wasichana, kuacha shule.

Ripoti ya China Family Development ya 2015ilikadiria kuwa aslimia 35 ya watoto walibaki nyuma katika maeneo ya vijijini. Ushahidi wa athari za uhamiaji kwa elimu na ustawi wa watoto walioachwa nyuma umechanganyika. Baadhi ya tafiti zinaonyesha kuwa watoto hawa wanafanya vizuri zaidi shuleni, huku zingine zikionyesha kuwa watoto hao wanapata alama za chini na wanakabiliwa na matatizo zaidi ya afya ya akili kuliko wenzao.

Tangu mwaka wa 2016, Uchina imepitisha sera zilizolenga kuboresha huduma kwa watoto waliobaki nyuma, ikiwa ni pamoja na wito kwa serikali za mitaa kuwahimiza wazazi wawateulie mlezi watoto waliowaacha. Shule za bweni ni mkakati muhimu, lakini mara nyingi huwa hazina walimu na vifaa vya kutosha. Kuna haja ya kuwapa wafanyakazi wasimamizi mafunzo bora ya usimamizi ili kuboresha ustawi wa watoto.

Hakuna takwimu za shule za bweni na wanafunzi waliopo, ingawa shule hizo zimeshamiri katika baadhi ya nchi. Nchini Uganda, idadi ya wanafunzi wenye hadi miaka 13 katika shule za bweni ni karibu asilimia 15, na idadi hii inaongezeka hadi asilimia 40 katika miaka ya mwisho ya vidato vya juu vya masomo ya sekondari.

## UHAMIAJI KWA MSIMU KUTOKA NA SABABU ZA KAZI HUATHIRI FURSA ZA ELIMU

Uhamiaji kwa msimu, ambao ni mkakati wa kujikimu maishani kwa maskini, unaweza kukatiza elimu na kutia watoto hatarini ya kutumikishwa na pia hatari zingine za mahali pa kazi. Nchini India, utafiti ulionyesha kuwa karibu asilimia 80 ya watoto wa wahamiaji kwa muda katika miji saba hawakuweza kupata elimu karibu na maeneo ya kazi, na asilimia 40 walifanyishwa kazi, walinyanyaswa na walitumiwa vibaya. Mipango ya hivi karibuni na serikali ya India inalenga kuhakikisha kuwa watoto wa wahamiaji wanahudhuria shule kwa kuhamasisha uandikishaji rahisi, kutoa elimu kupitia simu na kuboresha uratibu kati ya majimbo wanakotoka na wanakohamia, lakini utekelezaji umekumbwa na changamoto nyingi. Mpango wa majaribio katika jimbo la Rajasthan uliofanywa mwaka wa 2010-2011 katika maeneo ya kuchomea matofali, ulikumbwa na matatizo ya walimu na wanafunzi kutofika darasani kutokana na hali mbaya ya kufundisha na kujifunza na haja ya wanafunzi kufanya kazi.

## WATOTO WANAOAJIRIWA KAMA WAFANYAKAZI WA NYUMBANI WAMO HATARINI YA KUTOPATA ELIMU

> “Katika mwaka wa 2012, karibu watoto milioni 17.2 wenye umri wa miaka 5 hadi 17 waliajiriwa kama wafanyakazi wa nyumbani, wakiwa au bila malipo”

Katika mwaka wa 2012, karibu watoto milioni 17.2 wenye umri wa miaka 5 hadi 17 waliajiriwa kama wafanyakazi wa nyumbani, wakiwa au bila malipo. Theluthi mbili kati yao walikuwa wasichana. Wasichana wadogo, kwa mfano huko Lima, Peru, huona kazi ya nyumbani kama njia ya kuondoka vijijini na kuendelea na elimu, lakini mzigo wa kazi mara nyingi huwazuia kufika shuleni.

Ulezi wa watoto ni mkakati unaofutwa katika nchi nyingi za Afrika. Karibu asilimia 10 ya watoto nchini Senegal walipelekwa katika familia za kulea. Kulikuwa na uwezekano mkubwa wa kuwapeleka wavulana katika familia zinazotilia mkazo elimu, hivyo wavulana hao kupata elimu zaidi ya ndugu zao. Kwa upande mwingine, kulikuwa na uwezekano mara nne zaidi wa wasichana kusaidia kufanya kazi za nyumbani katika familia walikopelekwa, na uwezekano wa kupelekwa katika familia kwa sababu zinazohusiana an elimu ulikuwa chini.

### MAHITAJI YA ELIMU YA JAMII ZINAZOHAMAHAMA NA ZA WAFUGAJI HAYASHUGHULIKIWI

Kuhama ni sehemu msingi ya maisha ya jamii za wafugaji na zinazohamahama na ni lazima hatua zinazochukuliwa zitambue mahitaji yao. Si wengi wanaojiandikisha shuleni na idadi yao hubadilika sana kutegemea msimu. Aidha, wanafunzi hutatizika kujifunza kusoma na kuhesabu kwa kasi sawa na wenzao. Nchini Mongolia, kutopata fedha za kutosha kumedhoofishashule za bweni zasoumzilizolenga watoto wa jamii zinazohamahama, na kusababisha tofauti za kujifunza kati ya watoto wa jamii zinazohamahama na wa zile zisizohama.

Nchi nyingi zenye jamii zinazohamahama au za wafugaji zina idara za serikali, tume au mabaraza, kama vile Idara ya Elimu ya Jamii Zinazohamahama nchini Sudan. Jitihada zinazotiwa zinalenga kurekebisha elimu kulingana na msimu na uhamaji; mifano ni shule za makazi na shule zinazotumia simu.

Katika kaskazini mwa Nigeria, watu wengi wa jamii yaalmajiri(‘wanafunzi wahamiaji wa dini ya Uislamu’) ni wafugaji wanaohamahama. Katika jimbo la Kano, hatua ya kusuluhisha iliyowalenga walimu wa jadi 700 ilizingatia kuhusisha jamii na kushirikiana ili kuchagua walimu wa masomo yasiyo ya kidini.

Kuwepo kwa kikundi cha shule ambazo wanafunzi wanaweza kuondoka na kuingia wakati wowote au mahali popote laweza kuwa suluhisho linalofaa, lakini litahitaji mifumo madhubuti na yenye ufanisi ya kufuatilia. Baadhi ya nchi, zikiwemo Kenya na Somalia, zimefanya iwe rahisi kwa walimu kusafiri, hivyo wanaweza kuandamana na jamii zinazohamahama na kutoa elimu.

Elimu inayopewa jamii zinazohamahama inapaswa kutambua na kuimarisha njia yao ya maisha. Elimu ya kitaalamu inayoambatana na maisha ya uhamaji inaweza kuwa muhimu kwa wafugaji. Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa limefanya kazi na jamii zinazohamahama katika shule za ufugaji zilizo mahali walipo, katika nchi za Djibouti, Ethiopia, Kenya, Sudan Kusini na Uganda tangu mwaka 2012. Kozi wanazofunzwa zinazingatia ufanisi wa kuchunga mifugo na kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi.

### MAKUNDI YA ASILI YANAJITAHIDI KULINDA UTAMBULISHO WAO KATIKA MIJI

Katika maeneo mengi, elimu kwa watu wa asili imehusisha usimilishaji kwa lazima kupitia shule. Athari hiiinaendelezwa zaidi na umasikini na uhamiaji kwenda mijini, ambayo mara nyingi hufanya tamaduni zisahaulike, lugha zipotee na ubaguzi. Kupoteza lugha ni suala kubwa kwa wakazi wa mijini waliotoka vijijini. Idadi ya vijana katika miji ya Ecuador, Mexico na Peru inayoweza kuzungumza lugha za asili iko chini sana ikilinganishwa na wenzao wa vijijini.

Mifumo inayosimamia haki za asili haitaji watu wa asili wanaoishi mijini. Zaidi ya asilimia 50 ya wakazi asili wa Kanada wanaishi mijini. Uchambuzi wa jamii asili ya Australia ulionyesha umuhimu wa elimu katika kuboresha maisha yao na ikapatikana kuwa kujumuisha mitalaa na desturi zinazoendana na tamaduni kuliboresha matokeo ya elimu ya chekechea.

## Uhamiaji hutatiza wanaopanga masuala ya elimu katika vijiji na miji

Kupungua kwa idadi ya watu vijijini humaanisha kuwa wanaopanga masuala ya elimu, hasa katika nchi za kipato cha juu, lazima wasawazishe ugawaji wa rasilimali kwa kuzingatia ustawi wa jamii zilizoathiriwa. Kati ya miaka ya 1990 na 2015, nchi ya Ufini ilifunga au kuunganisha pamoja karibu asilimia 80 ya shule zilizokuwa na chini ya wanafunzi 50 - zaidi ya shule 1,600 kwa jumla. Kukua kwa miji na kupungua kwa uzazi kumezua changamoto sawa katika nchi nyingi za kipato cha kati. Kati ya mwaka wa 2000 na 2015, idadi ya shule za vijijini katika Urusi ilipungua kutoka 45,000 hadi chini ya 26,000. Nchini Uchina, idadi ya shule za msingi za vijijini ilipungua kwa asilimia 52 kati ya mwaka wa 2000 na 2010.

Wakati serikali zinafikiria kuunganisha shule ili kuongeza ufanisi, zinapaswa kutambua wajibu muhimu wa shule katika jamii, pamoja na faida nyingine. Uchambuzi wa data kutoka Mradi wa Tathmini ya Kimataifa ya Wanafunzi (PISA) wa 2015 ulionyesha kuwa wanafunzi kutoka shule ndogo hawakuwa na matatizo mengi ya nidhamu, kuchelewa na kutofika shuleni.

Ili kuunganisha kwa mafanikio, ni lazima wadau wote wanaoathirika wajumuishwe na gharama izingatiwe. Serikali ya Lithuania ilibuni hatua kuu ili kuhifadhi shule ndogo za msingi za vijijini na kutoa usafiri salama na mamia ya mabasi mapya.

Nchi zingine huhimiza shule za vijijini kushiriki rasilimali na katika kujifunza ili kuendelea mbele vizuri. Nchi ya Chile ina vituo 374 vidogo vya walimu wa vijijini kukutana na kujadili changamoto zinazowakabili. Tangu mwaka wa 2011, serikali ya Uchina imekuwa ikifanyia shule ndogo za vijijini ukarabati mkubwa na kuziboresha, nayo mashirika yasiyo ya serikali (NGOs), jamii zilizo karibu na shule zenyewe zimeanzisha mitandao ya kushiriki rasilimali.

## WAHAMIAJI KATIKA MAKAZI DUNI WANA NAFASI CHACHE ZA KUPATA ELIMU

Angalau watu milioni 800 wanaishi kwenye makazi duni. Huenda ufafanuzi wa kitaifa au mbinu za makadirio zikapunguza idadi hii. Wakazi wengi katika makazi duni ni wahamiaji waliotoka vijijini na huwa hawapati huduma za msingi, ikiwa ni pamoja na elimu ya umma. Kufukuzwa na kuhamishwa upya kwa wakazi wa makazi duni huongeza viwango vya wanaoacha shule na wanaokosa kuhudhuria masomo. Katika mwaka wa 2016 nchini Bangladesh, idadi ya vijana wa umri wa kwenda shule ya sekondari waliokuwa hawaendi shule ilikuwa mara mbili zaidi katika makazi duni ikilinganishwa na maeneo mengine ya mijini.

Ukusanyaji data ya elimu katika makazi duni haupewi kipaumbele kwani mijadala mingi hulenga changamoto za makazi, maji na usafi wa mazingira. Shirika la Shack / Slum Dwellers Internation hukusanya data katika nchi zaidi ya 30, lakini data yake ya elimu ni finyu. Huenda ukadiriaji wa shughuli zinazohusiana na elimu katika makazi duni ukawa si sahihi kwani kuna shule za binafsi ambazo hazijasajiliwa, ambazo zinajaza pengo la kutokuwa na shule za umma. Huko Kibera, nchini Kenya, mradi wa kutambua ramani ya eneo ulibainisha shule 330 ilhali makadirio rasmi yalikuwa 100. Mara nyingi, chaguo walio nalo wakazi wa makazi duni ni shule za binafsi, ambazo huwa hazielekezwi vizuri na ambazo huajiri walimu ambao hawajahitimu. Mradi wa kuleta walimu bora katika makazi duni jijini Nairobi uliboresha matokeo ya wanafunzi ya kusoma na kuhesabu.

Elimu inahitaji kupewa kipaumbele katika mijadala ya mijini juu ya suala la makazi duni. Kupata hati rasmi ya umiliki wa makazi na kubainisha haki ni hatua muhimu katika utoaji wa elimu, kwani mara nyingi serikali husita kukija ni kuwekeza katika miundombinu ya elimu kwa watu wanaoishi kwenye ardhi ambao hawamiliki. Nchini Argentina, upatikanaji wa hatimiliki za ardhi ulihusishwa na kuinuka kwa muda mrefu kwa ubora wa elimu.

Mara nyingi, masharti makali ya usajili na upataji nyaraka huzuia wahamiaji kushiriki katika mipango ya ulinzi wa jamii ambayo inaweza kufaidi elimu yao. Katika makzi duni ya Kenya, mpango wa ulinzi wa jamii mijini ulihitaji kitambulisho cha kitaifa, na hivyo kuzuia asilimia 5 ya waliokuwa wamechaguliwa ambao walikuwa ama ni wakimbizi, hawangeweza kuthibitisha kuwa walikuwa wakenya au familia zilizoongozwa na watoto.

# Uhamiaji wa kimataifa

Watu wanapohama ili kutafuta nafasi bora za kazi na za maisha, wanalazimika kurekebisha maisha ili kuendana na mifumo mipya, kukabiliwa na changamoto za kisheria na utawala na kukabiliana na vikwazo vya lugha na labda hata ubaguzi. Katika nchi wanakohamia, mifumo ya elimu hulazimika kurekebisha gharama ili kuwajumuisha wahamiaji hao.


Mwaka wa 2017, kulikuwa na wahamiaji wa kimataifa milioni 258, ambao ni asilimia 3.4 ya idadi ya watu duniani. Takribani asilimia 64 walihamia nchi za kipato cha juu, ambapo sehemu ya wahamiaji kama sehemu ya idadi ya watu iliongezeka kutoka asilimia 10 katika mwaka wa 2000 hadi asilimia 14 katika mwaka wa 2017. Katika nchi nyingi za Ghuba, ikiwa ni pamoja na Kuwait, Qatar na Falme za Kiarabu, wakazi wengi ni wahamiaji.

Katika nchi mbalimbali za kipato cha kati kama vile Costa Rica, Côte d'Ivoire, Malaysia na Afrika Kusini, viwango vya uhamaji viko mara mbili hadi tatu juu ya viwango wastani vya kimataifa. Kwa upande mwingine, nchi zilizo na viwango vya uhamaji vilivyozidi asilimia 5 ya idadi ya watu ni pamoja na Albania, Georgia, Jamaica, Kyrgyzstan na Nicaragua. Idadi ya juu zaidi ya wahamaji ni ya wale wanaotoka Mexico kuelekea Marekani. Wengine ni wale wanaotoka Ulaya ya mashariki kuelekea Ulaya ya magharibi, kaskazini mwa Afrika kuelekea kusini mwa Ulaya na kusini mwa Asia hadi nchi za Ghuba.

**MCHORO WA 2:**

**Katika nchi nyingi za OECD, angalau mmoja kati ya wanafunzi watano wa miaka 15 alikuwa kizazi cha kwanza au cha pili cha wahamiaji**

*Kusambaa kwa wanafunzi wa miaka 15 kulingana na walikotoka, baadhi ya nchi, 2015*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig3_4

*Kumbuka:* Takwimu hazijumuishi nchi na wilaya tano zenye data na hata viwango vya juu zaidi vya wanafunzi walio na asili ya wahamiaji: Eneo la Hong Kong lililo chini ya mamlaka ya Uchina; Luxemburg; Macao, Uchina; Qatar; na Falme za Kiarabu.

*Chanzo:* Uchambuzi wa timu ya Ripoti ya GEM kulingana na ripoti ya PISA ya 2006 na 2015 na TIMSS ya 2015.

Katika mwaka wa 2015 katika nchi nyingi za Shirika la Ushirikiano na Maendeleo ya Uchumi (OECD), angalau mwanafunzi mmoja kati ya tano wa miaka 15 alikuwa mhamiaji au na asili ya wahamiaji **(Mchoro wa 2)**. Makadirio ya ripoti hii yanaonyesha kuwa katika asilimia 80 ya shule za sekondari katika nchi za kipato cha juu, angalau asilimia 5 ya wanafunzi wana asili ya wahamiaji; katika asilimia 52, angalau asilimia 15 wana asili ya wahamiaji.

# Uhamiaji na elimu huathiriana

Wahamiaji si idadi ya watu ya kubahatisha. Miongoni mwa tofauti kati yao na wale ambao si wahamiaji, wao huwa na elimu zaidi, jambo ambalo huwasaidia kukusanya taarifa bora, kuweza kutambua na kutumia fursa za kiuchumi, kutumia ujuzi unaohamishika na kuhamisha fedha. Katika mwaka wa 2000, viwango vya uhamiaji wa kimataifa vilikuwa asilimia 5.4 kwa wale walio na elimu ya juu, asilimia 1.8 kwa walio na elimu ya sekondari na asilimia 1.1 kwa walio na elimu ya msingi.

> “Katika mwaka wa 2000, viwango vya uhamiaji wa kimataifa vilikuwa asilimia 5.4 kwa wale walio na elimu ya juu, asilimia 1.8 kwa walio na elimu ya sekondari na asilimia 1.1 kwa walio na elimu ya msingi”

Kuweza kupata elimu wakati wa uhamiaji pia kunategemea njia ambazo wahamiaji walitumia kuvuka mipaka: Wahamiaji wa Marekani kutoka El Salvador, Haiti, Mexico na Nikaragua wasio na nyaraka rasmi walikuwa na elimu zaidi, kwa wastani, ikilinganishwa na wale walio na mikataba ya muda mfupi lakini elimu yao ilikuwa chini ya wale waliokubaliwa rasmi kuwa mle.

Ili kuelewa jinsi uhamiaji unavyoathiri fursa ya kupata na ufanisi katika elimu, ni vyema kulinganisha mambo yafuatayo. La kwanza ni kulinganisha wale waliohama na wale waliobaki, ingawa kuna tofauti zingine kati ya makundi haya kando na uamuzi wa kuhama (kwa mfano huenda wahamiaji wangepata elimu zaidi kama wangekosa kuhama). La pili ni kulinganisha wahamiaji na wenyeji, ambao pia tofauti kati yao ni zaidi ya hali ya uhamiaji. Katika hali nyingine, sera za uhamiaji zinazobagua zinaweza kusababisha wahamiaji kupata elimu zaidi ya wenyeji; katika hali nyingine, huenda wahamiaji wakaishi katika maeneo maskini yenye shule duni, jambo ambalo huenda likafanya watoto wao kutofanya vizuri na kutofanikiwa shuleni.

## UHAMIAJI HUATHIRI ELIMU YA WALE WALIOBAKI NYUMA

Mara nyingi, wale wanaohama huwaacha watoto nyuma. Nchini Ufilipino, takriban watoto milioni 1.5 hadi milioni 3 wana angalau mzazi mmoja ambaye ni mhamiaji wa kimataifa. Athari ya fedha zinazotumwa kwa elimu inaweza kuwa muhimu.

Kote duniani, familia zilipokea dola za Marekani bilioni 613 kutoka kwa wanafamilia wanaoishi ng'ambo katika mwaka wa 2017. Dola za Marekani milioni 466 zilienda kwa familia katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Kiasi hiki ni mara tatu ya kile rasmi cha usaidizi wa maendeleo. Nchi za India na Uchina ndizo zilipata kiasi kikubwa zaidi kwa jumla lakini Kyrgyzstan na Tonga zilipata asilimia ya juu zaidi kwa misingi ya jumla ya pato nchini.

Kwa kukisia, fedha zinazotumwa na walio ng'ambo zinaweza kuwa na athari nzuri au mbaya kwa elimu. Vyanzo vingi vya mapato huwa kama kinga kwa familia: hivyo huenda wasipunguze pesa wanazotumia kugharamia elimu. Hata hivyo, ingawa kuongezeka kwa mapato huongeza matumizi ya familia, elimu hushindana na matumizi mengine, huenda watoto wakachukua nafasi ya kazi ya waliohama, na ukosefu wa mchango wa wazazi unaweza kuzuia elimu. Fedha zinazotumwa kutoka ng'ambo zinaweza pia kuibua 'utamaduni wa kuhama' ambapo nafasi ya kupata hela nyingi kutokana na ujuzi wa chini huko ng'ambo inaweza kupunguza ari ya kuendelea na masomo.

Katika hali halisi, fedha zinazotumwa kutoka ng'ambo ziliongeza matumizi katika elimu ya familia kwa asilimia 35 kwa wastani, kulingana na tafiti kadhaa katika mataifa 18 ya Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia ya Kati, Kusini na Kusini mashariki. Matumizi haya yaliongezeka zaidi katika Amerika ya Kusini (asilimia 53).

## Kupunguza gharama kwa wahamiaji ya kutuma pesa nyumbani




Lengo la 10.c la Malengo ya Maendeleo Endelevu linahimiza kupunguzwa kwa gharama inayotozwa wakati wa kutuma pesa kutoka ng'ambo kwa hadi chini ya asilimia 3, kwa wastani. Wastani wa sasa ni asilimia 7.1. Mabenki ya jadi ndiyo yanayotoza gharama ya juu zaidi, ya asilimia 11, na makampuni mengine nchini Afrika yanatoza zaidi ya asilimia 20. Ikichukuliwa kuwa matumizi ya jumla ya familia kwa elimu ni asilimia 4, kupunguza gharama za kutuma fedha kutoka ng'ambo hadi asilimia 3 kunaweza kuruhusu familia kutumia dola za Marekani bilioni 1 ziada, kugharamia elimu kwa mwaka.

Tafiti kadhaa zinaonyesha kwamba pesa zinazotumwa kutoka ng'ambo, kwa jumla, zina athari nzuri kwa elimu. Nchini Ufilipino, ongezeko la asilimia 10 katika pesa zilizotumwa kutoka ng'ambo liliongeza mahudhurio ya shule kwa zaidi ya asilima 10 na kupunguza utumikishaji wa watoto kwa zaidi ya saa tatu kwa wiki. Matokeo haya yanaweza kutofautiana kulingana na jinsia. Nchini Jordan, pesa zilizotumwa kutoka ng'ambo zilikuwa na matokeo mazuri katika mahudhurio ya elimu ya lazima kwa wanafunzi wa kiume tu.

Huenda matokeo chanya yakaonyesha njia fulani pekee za uhamiaji au mazingira yenye viwango vya chini vya usajili. Katika baadhi ya njia za uhamiaji zinazotumiwa na watu wenye ujuzi wa chini, kuna ushahidi wa athari hasi kwenye matokeo.Kupokea pesa kutoka ng'ambo kulihusishwa na kupungua kwa uwezekano wa kujiunga na shule nchini Guatemala, ingawa waliojiandikisha walifanya vizuri zaidi kutokana na pesa walizopokea.Katika vijijini vya Mexico, wanafunzi waliobakiwalifanya vibaya zaidi katika masomo kutokana na pesa walizopokea.

### WAHAMIAJI HULIPA GHARAMA YA ELIMU KATIKA NCHI WANAZOHAMIA

Katika nchi wanazohamia, wahamiaji mara nyingi huacha elimu mapema. Katika Umoja wa Ulaya, asilimia 10 ya wenyeji na 19 ya wahamiaji wenye umri wa miaka 18 hadi 24 waliacha shule mapema, katika mwaka wa 2017. Umri aliokuwa nao mhamiaji alipowasili huathiri uwezekano wa kuacha shule; matokeo hutofautiana kulingana na kama wanafunzi hujiunga na mifumo ya wanakohamia mwanzoni, katikati au mwisho wa kipindi cha elimu ya lazima. Nchini Marekani, asilimia 40 ya wahamiaji kutoka Mexico ambao walifika wakiwa na umri wa miaka 7 hawakukamilisha shule ya sekondari, ikilinganishwa na asilimia 70 ya wale waliofika wakiwa na umri wa miaka 14.

Hata hivyo, hali ya elimu ya wahamiaji huboreka haraka zaidi kuliko ya wenyeji na wale walioachwa nyuma. Nchini Ujerumani, wenyeji ambao wazazi wao walikuwa na elimu chini ya wastani waliendelea polepole zaidi kuliko wenzao wahamiaji. Katika nchi 8 kati ya 10 za Amerika Kusini na Karibi, watoto wa wahamiaji walikuwa, kwa wastani,na mwaka1.4zaidi wa elimu ikilinganishwa na watoto wa wazazi ambao hawakuhama.

Viwango vinavyofikiwa vya elimu huathiri vizazi. Katika ripoti ya PISA ya 2015, asilimia 49 ya kizazi cha kwanza na asilimia 61 ya kizazi cha pili cha wahamiaji wa umri wa miaka 15 walipata ujuzi wa daraja la 2 katika kusoma, hisabati

na sayansi, ikilinganishwa na asilimia 72 ya wenyeji. Nchini Kanada, Ujerumani na Italia, idadi ya wenyeji wanaofika kiwango cha elimu ya juu inaendelea kuwa juu kuliko ya kizazi cha pili cha wahamiaji.

Ulinganisho wa wahamiaji wa Kituruki wa kizazi cha pili katika nchi sita ulionyesha kuwa ni asilimia 5 tu ya walio Ujerumani na asilimia 37 ya wale walio Ufaransa waliopata elimu ya juu. Sababu za kitaasisi nchini Ufaransa, kama vile upatikanaji mapema wa elimu ya msingi, kuchelewa kugawanya kwa misingi ya uwezo katika shule ya sekondari na upatikanaji wa elimu ya juu hata kwa walio na uwezo wa chini kielimu, kunafafanua tofauti iliyopo katika asilimia ya waliopata elimu ya juu.

Takriban asilimia 20 ya pengo la wahamiaji ambao hawajapata elimu katika nchi za OECD inaweza kuhusishwa na kutokuwa na uwezo wa kutosha, kijamii na kiuchumi; katika nchi nyingine, zikiwemo Ufaransa na Ugiriki, ukosefu huu unaweza kuhusishwa na hadi nusu ya idadi hii. Uwezekano wa wanafunzi wahamiaji katika nchi za OECD kurudia daraja huongezeka maradufu ikilinganishwa na wenyeji.

## Sera za uhamiaji na uraia huzuia kujiunga na shule

Haki ya elimu na kanuni ya jumla ya kutobagua zimewekwa katika Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiuchumi, Jamii na Utamaduni na Mkataba wa Haki za Mtoto. Mkataba wa kimataifa unaolenga uhamiaji pekee unathibitisha kuwa wahamiaji na wakimbizi wanapaswa kuchukuliwa kama wananchi kukija ni elimu, ingawa kufikia sasa umeidhinishwa na nchi moja tu kati ya nne, na karibu zote hutuma wahamiaji ng'ambo. Katika hali halisi, sera finyu za uhamiaji, sheria kinzani na mahitaji makali ya hati rasmi katika nchi wanakohamia yanaweza kuzuia utimizaji wa haki hii.

Baadhi ya sheria za kitaifa zinaweza kuzuia haki ya kikatiba ya kupata elimu. Nchini Cyprus na Slovakia, shule zinalazimishwa kuripoti familia bila hati halali kwa mamlaka ya uhamiaji. Nchini Afrika Kusini, Sheria ya Uhamiaji ya mwaka wa 2002 inazuia wahamiaji wasio na hati rasmi kujiandikisha shuleni.

Sheria inayoimarisha haki za elimu kwa wale ambao si wenyeji huongeza uwezekano wa kutimizwa kwa haki ya elimu. Katika Argentina, Sheria ya Elimu ya Taifa ya mwaka wa 2006 inathibitisha haki ya elimu kwa wakazi wote. Sheria ya shule za msingi nchini Slovenia inatoa wazi haki ya elimu kwa watu wasio na uraia wowote.

Mfumo wa kisheria unaojumuisha wote hauzuii visa vya ubaguzi katika eneo husika. Shule zinaweza kuitisha vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya elimu ya hapo awali, hati za utambulisho za kitaifa au uthibitisho wa makazi ili kujiandikisha. Nchini Chile, ambapo idadi ya wahamiaji kutoka Haiti iliongezeka kutoka chini ya 5,000 katika mwaka wa 2010 hadi 105,000 katika mwaka wa 2017, sera inaeleza kuwa elimu ya umma inapaswa kutolewa kwa watoto wote; katika hali halisi, uamuzi wa utoaji wa elimu umeachiwa viongozi wa serikali za mitaa. Viongozi wa shule nchini Uzbekistan mara nyingi huhitaji uthibitisho wa makazi, pasipoti au uwezo wa kujifunza lugha ya kitaifa kwa urahisi kabla ya kusajiliwa.

Ufafanuzi rasmi unaweza kuwahakikishia wasimamizi wa shule kwamba sheria haihitaji hati kamili, na mfumo thabiti wa kitaifa wa kisheria unaweza kutoa fursa za watu kuwasilisha malalamiko yao. Katika mwaka wa 2014, nchi za Italia na Uturuki zilifafanua kwamba haikuwa lazima kuwa na hati ili mtu aandikishwe. Nchini Ufaransa, wazazi wanaweza kukata rufaa kwa mwakilishi wa umma au mahakama ili kuomba kuangaliwa tena kwa maamuzi ya uandikishaji yenye ubaguzi.

Hata hivyo, wahamiaji ambao hawajapata hati rasmi bado wanaendelea kukabiliwa na vikwazo vya kufikia elimu. Nchini Marekani, ambamo kulikuwa na wahamiaji milioni 11 bila hati rasmi katika mwaka wa 2014, tishio la kufukuzwa linaweza kufanya watoto wasipelekwe shuleni: mnamo Februari 2017, visa vya watoto kutofika shuleni huko wilaya ya Las Cruces, New Mexico, viliongezeka kwa asilimia 60 baada ya shambulio la kuwatafuta wahamiaji wasio na

hati rasmi. Mradi wa Deferred Action for Childhood Arrivals (DACA) wa mwaka wa 2012 ulilenga vijana milioni 1.3 bila hati rasmi ambao walihamishwa wakiwa watoto na uliwapatia ulinzi dhidi ya kurudishwa makwao na haki ya kupata vibali vya kazi. Mradi huu uliongeza viwango vya waliohitimu masomo ya sekondari kwa takriban asilimia 15 kwani wahamiaji wanaostahiki walijikakamua kutimiza masharti.

Mara nyingi, mahitaji ya elimu ya watoto wahamiaji walio pekee yao, ambao wamo katika hatari zaidi ya kunyanyaswa huwa hayatimizwi. Idadi ya watoto hawa duniani kote iliongezeka kutoka 66,000 katika mwaka wa 2010-2011 hadi 300,000 katika mwaka wa 2015-2016. Katika nchi nyingi, zikiwemo Australia, Ugiriki, Indonesia, Malaysia, Mexico, Nauru na Thailand, watoto na vijana walio katika kizuizi cha wahamiaji mara nyingi huwa na nafasi ndogo au kukosa nafasi yoyote ya kupata elimu. Karibu asilimia 73 ya watoto 86,000 waliofika nchini Italia kati ya mwaka wa 2011 na 2016 walikuwa peke yao. Licha ya sheria za mwaka wa 2015 na 2017 zilizolenga kuwalinda, ni wachache tu wanaohudhuria shule.

Ukosefu wa hati rasmi unaweza kuzua vikwazo kwa watu milioni 10 wasio na uraia duniani kote, baadhi yao ambao ni vizazi vya wahamiaji. Nchini Côte d'Ivoire, ambako kuna watu 700,000 wasio na uraia, uthibitisho wa utaifa unahitajika ili kupata elimu. Katika Jamhuri ya Dominika, ambapo maelfu ya wahamiaji kutoka Haiti wamenyimwa haki ya utaifa, katika mwaka wa 2012 kiwango cha watoto wenye umri wa miaka 6 hadi 13 walihudhuria shule za msingi, kilikuwa asilimia 52 kati ya wale waliozaliwa Haiti lakini asilimia 82 kati ya wahamiaji waliozaliwa katika nchi nyingine.

# Sera za elimu zinaweza kuwasaidia wahamaji kujiunga na shule

Mipango ya elimu kwa watoto wachanga, ile ya kusaidia kujifunza lugha na sera zinazohusiana na kutiririsha mafunzo, uteuzi na ubaguzi ni muhimu ili kuboresha upatikanaji wa elimu.

Ni muhimu kwa wahamiaji kushiriki katika mipango ya elimu kwa watoto wachanga. Kwa wastani, alama za kusoma za wahamiaji wenye umri wa miaka 15 waliokuwa wamepata elimu ya chekechea zilikuwa juu kwa kiasi kilicholingana na zaidi ya mwaka mmoja wa shule. Wahamiaji wasio na hati rasmi wanaweza kutatizika kujiunga na mipango ya elimu kwa watoto wachanga: huko Marekani, idadi ya watoto wenye umri wa miaka 3 na 4 bila hati rasmi waliosajili katika shule za watoto wachanga, ilikuwa chini ya ile ya watoto wahamiaji wenye hati rasmi na wenyeji.

Kukosa umilisi wa lugha hutatiza elimu kwa sababu kunazuia kutagusana na jamii, kujenga uhusiano na kujihisi mtu akiwa mahali anapofaa. Pia huongeza hatari ya ubaguzi. Katika mwaka 2012, asilimia 53 ya wanafunzi wa kizazi cha kwanza wa wahamiaji katika nchi 23 za kipato cha juu, waliokuwa hawawezi kusoma na kuandika vizuri, walikuwa katika kozi za ziada za kuandika na kusoma.

Muda wa madarasa ya maandalizi hutofautiana kulingana na nchi: huko Ubelgiji, Ufaransa na Lithuania ni mwaka moja na huko Ugiriki ni miaka minne. Mafunzo ya 'kukaribisha' huko Ujerumani hutoa maelekezo tofauti yanayolenga umilisi wa lugha kwa wanafunzi wenye asili ya wahamiaji. Katika Uhispania, mikoa mbalimbali hufuata mojawapo ya mifano mitatu - madarasa ya muda ambayo wanafunzi huhudhuria kwa kipindi fulani cha siku, madarasa ya kuzamia lugha na madarasa yanayohimiza mtagusano wa tamaduni ambayo hayalengi tu umilisi wa lugha bali yanalenga kujenga uhusiano kati ya familia na shule. Serikali zinahitaji kuepuka kutofautisha shule kwa muda mrefu kwa sababu kunaweza kuongeza upungufu na madhara.

Uteuzi wa mapema kulingana na uwezo huwa kizuizi kwa wanafunzi wahamiaji na huwanyima nafasi, hivyo kusababisha kutokuwa na usawa na kuendeleza mtazamo unaohusisha mahali mwanafunzi alikotoka na matokeo yake shuleni. Nchini Italia, asilimia 59 ya wahitimu wa sekondari wenye asili ya wahamiaji walijiunga na vyuo kikuu,

ikilinganishwa na asilimia 33 ya wale wa shule za kitaaluma na asilimia 13 ya wale waliohitimu shule za kiufundi.

Mara nyingi, wanafunzi wahamiaji huwa katika maeneo ya miji na shule zenye viwango vya chini vya elimu na matokeo duni. Ubaguzi huongezeka wanafunzi wenyeji wanapohamia maeneo yaliyostawi zaidi. Nchini Uingereza, kuliwa na uwezekano mkubwa zaidi wa wahamiahi kuhudhuria shule sawa wa wenyeji wasio na uwezo. Idadi ya wahamiaji pia inaweza kuathiri matokeo ya elimu ya wenyeji wasio na uwezo. Nchini Norway, ongezeko la asilimia 10 la idadi ya wahamiaji katika shule ilihusishwa na ongezeko la asilimia 3 ya idadi ya wenyeji walioacha shule.

Nchi tofauti hutumia zana mbalimbali ili kupambana na ubaguzi. Nchini Italia, notisi rasmi ya mwaka wa 2010 iliweka idadi ya juu ya wanafunzi wahamiaji wa kizazi cha kwanza darasani kuwa asilimia 30. Katika hali halisi, madarasa ya shule za msingi yalizidisha idadi hiyo kwa asilimia 17. Licha ya sera na marekebisho ya kupunguza ubaguzi katika shule nchini Ufaransa na Ujerumani, wazazi huepuka shule walizopewa, na shule hupata njia za kuwa na madarasa tofauti kulingana na uchaguzi wa wazazi wa mafundisho ya kidini au ya lugha ya kigeni. Uchunguzi wa maeneo 108 yenye shule za msingi katika wilaya nne za Berlin ulionyesha kwamba katika shule moja kati ya tano, idadi ya wanafunzi wahamiaji waliojiandikisha ilikuwa maradufu ile ya wanaoishi eneo hilo.

## SERIKALI ZINGINE HUELEKEZA MSAADA KATIKA SHULE ZENYE IDADI KUBWA YA WANAFUNZI WAHAMIAJI

Kuna uwezekano kuwa shule zilizo na idadi kubwa ya wanafunzi wahamiaji au wakimbizi zina mahitaji ya juu ya kifedha. Mfumo wa kugawa pesa kwa mpangilio uliokubalianwa unalenga kuongeza usawa kwa kugawia shule zilizo na uwezo rasilimali zaidi. Baadhi ya mipango inajumuisha wahamiaji kama sababu ya wazi katika kuigawia shule fedha. Katika Lithuania, bajeti ya shule inatoa asilimia 20 ya ziada kwa wanafunzi ambao wametoka katika jamii za wachache nchini na asilimia 30 kwa wanafunzi wahamiaji katika mwaka wao wa kwanza wa shule nchini.

Si wengi wanaofuata utaratibu huu, lakini wanafunzi wahamiaji na wakimbizi bado wanaweza kusababisha kuongezeka kwa fedha za ufadhili, hata kama si kwa njia ya moja kwa moja. Fedha zinaweza kutolewa kwa misingi ya kutokuwa na umilisi wa kutosha wa lugha ya mafundisho au ukosefu wa uwezo wa kijamii na kiuchumi katika mazingira wanamoishi, mambo ambayo yanawaathiri sana wahamiaji. Mfumo mpya wa Kitaifa wa Kugawa Fedha nchini Uingereza unafutilia mbali suala la kuwapatia wahamiaji fedha maalum lakini unagawa fedha ili kulipa fidia mambo kama vile ‘kunyimwa’, ‘kiwango cha chini cha elimu hapo awali’ na ‘Kiingereza kama lugha ya ziada’.

Shule zinaweza kupata fedha zaidi za kusaidia wahamiaji na wakimbizi kando na zile za msingi wanazopewa. Serikali ya Denmark ilitenga karibu dola milioni 3 za Marekani katika miaka ya 2008-2011 kwa ajili ya shughuli na rasilimali, kama vile washauri wa shuleni na nyumbani, ili kuimarisha ushirikiano kati ya familia za wahamiaji na shule.

Nchi zingine zinalenga kugharamia mafunzo ya lughabila kutumia fedha zilizokubalianwa kutengewa shule. Mpango wa Kufundisha Lugha ya Kiingereza cha Marekani unatoa karibu dola milioni 740 za Marekani kila mwaka kama misaada kulingana na idadi ya wanafunzi wanaojifundisha Kiingereza. Shule hutoa fedha katika mfuko huu ili kuendeleza mafunzo ya lugha. Usaidizi wa ziada unaweza pia kuwalenga walimu, ambao huenda wakatatizika kuwasiliana na wanafunzi na familia za wahamiaji.

Huenda msaada maalum unaowalenga wanafunzi wahamiaji na wakimbizi usitatizwe na changamoto za kimuundo na utawala za shule. Wahamiaji na wakimbizi walio na elimu ya chini huwa mara nyingi wanakaa katika maeneo ambayo tayari hayana wafanyakazi wa kutosha. Kutoa vichocheo vya kuwavutia walimu katika shule zenye mahitaji si rahisi nje ya bajeti ya kawaida ya shule. Aidha, maamuzi ya kisiasa yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwafedha zinazotolewa kwa kusudi maalum au zile za ziada za kugharamia mipango mbalimbali, kama ilivyo nchini Marekani.

## MIRADI YA MAFUNZO YA NGUMBARU YA KUSOMA NA KUANDIKA NA LUGHA NI NJIA KUU YA KUWAJUMUISHA WAHAMIAJI NA WAKIMBIZI

Uwezo wa kusoma na kuandika wanaomilisi wahamiaji na wakimbizi hutofautiana sana. Utafiti uliofanyiwa wakimbizi huko Ujerumani mnamo mwaka wa 2016 ulionyesha kuwa asilimia 15 walikuwa hawajasoma, asilimia 34 waliweza kusoma hati za Kilatini na asilimia 51 walijua kusoma hati nyingine tofauti. Elimu ya ngumbaru inaweza kuwafanya wahamiaji na wakimbizi wajihisi wamekaribishwa zaidi na kuongeza uwezo wao wa kuwasiliana na

kukidhi mahitaji ya kila siku. Ufasaha katika lugha ya wenyeji umehusishwa na kuongezeka kwa nafasi za kazi, mapato ya juu na afya bora zaidi. Hata hivyo, hakuna mipango mingi mikubwa ya umma inayotoa elimu ya ngumbaru ya kuandika na kusoma kwa wahamiaji na wakimbizi.

Ni lazima miradi hii iwe rahisi kubadilisha na maudhui, ratiba na ushadidi wake uwe tofauti ili ziambatane na uanuwai miongoni mwa wahamiaji na wakimbizi. Wanafunzi ambao hawawezi kusoma na kuandika katika zao za kwanza wanakabiliwa na changamoto maalum. Kadirio moja linasema kwamba wale ambao hawajapata elimu yoyote au wamepata ndogo wanaweza kuchukua muda mara nane zaidi ili kufikia kiwango cha msingi katika kusoma lugha ya pili. Nchini Ufini, huenda mafunzo yanayotolewa kwa watu wazima wasioweza kusoma na kuandika yakawa mafupi sana kwa kuwa wanajifunza polepole.

Ili kuwasaidia wanafunzi kama huo, walimu wanahitaji ujuzi wa kutumia vifaa vinavyolenga changamoto ambazo wahamiaji hukutana nazo katika maisha ya kila siku. Katika mradi wa AlfaZentrum für MigrantInnen huko Vienna, wanafunzi hutoa vifaa kutoka mahali pa kazi au nyumbani ambavyo wangependa kuelewa.

Kufundisha na kujifunza kwa kutumia lugha ya kwanza ya wahamiaji kunaweza kuwa njia bora ya kuwasaidia kupata ujuzi wa kusoma na kuandika. Nchini Norway, vituo vya mafunzo ya ngumbaru vimeanza kuwashirikisha wanafunzi wenye elimu zaidi kama wasaidizi katika madarasa ya kwanza ya kujifunza kusoma na kuandika, ili kuwawezesha walimu na wanafunzi kuelewana.

Ukosefu wa fedha za kutosha unaweza kuzuia utekelezaji wa mpango, hasa ambapo rasilimali na usaidizi wa serikali haziendani na sera, kama nchini Uingereza. Umaskini, kuhofia usalama na ukosefu wa miradi inayofaa kitamaduni unaweza kuwazuia watu, hasa wanawake, kuhudhuria madarasa. Kuwaweka wageni wapya katika maeneo yenye makunzi yanayozungumza lugha sawa kunaweza wazuia wasijifunze lugha ya wenyeji. Na kuhama kwa muda kunaweza kupunguza msukumo wa kujifunza lugha mpya.

Miradiya mafunzo ya lugha inapaswa kuwa rahisi kurekebisha kulingana na hali, izingatie tamaduni na iwe nyenzo za kutosha. Kuwajumuisha wahamiaji na wakimbizi katika kupanga na maelekezo kunaweza kusaidia. Nchini New Zealand, serikali, katika awamu ya kuandaa mpango, ilishauri waliokuwa wakimbizi hapo awali na kwa wakati huo, juu ya sifa zinazofaa za kozi na vikwazo vya kufikia.

Ajira ni jambo ambalo wahamiaji na wakimbizi wanalikipatia kipaumbele pindi wanapowasili, na ujumuishwa na kumilisi lugha zinaweza kuathiri kiwango cha ushiriki kazini. Nchini Cabo Verde, mpango wa Uendelezaji wa Kuandika na Kusoma na Kufundisha Wahamiaji wa Jumuiya za Kiafrika zinazoishi Cabo Verde, hufundisha kusoma na kuandika, lugha ya Kireno na mafunzo ya kiufundi, kama ujuzi wa kompyuta na useremala. Kozi za ujumuishaji zinazotolewa na serikali ya Ujerumani zinahusisha masaa 600 ya mafunzo ya lugha ya Kijerumani, na wakimbizi ambao wanafikia ustadi wa B1 wanastahiki mafunzo ya lugha yanayohusiana na kazi.

## WAHAMIAJI WANAHITAJI ELIMU YA FEDHA

Elimu ya fedha ni finyu mno katika nchi nyingi ambazo wahamiaji wanatoka na miongoni mwa jumuiya za wahamiaji wenye ujuzi mdogo, hivyo kuongeza hatari ya wahamiaji na wakimbizi kudanganywa na kunyang'anywa pesa. Cha kutambua hasa ni kwamba huenda wasifahamu vizuri mifumo ya kifedha na ustawi katika nchi wanakohamia, pamoja na njia za utoaji na utumaji wa fedha.

Mipango ya kimataifa kama Mtandao wa Kimataifa wa Elimu ya Fedha wa OECD (OECD International Network on Financial Education) inalenga wahamiaji kama sehemu ya mipango pana ya kukuza ujumuishaji katika masuala ya fedha. Mipango ya elimu ya fedha kwa wahamiaji mara nyingi inahusisha mchanganyiko wa wadau wa kimataifa, serikali, mashirika yasiyo ya serikali na wadau binafsi.

Indonesia ilipitisha mkakati wakitaifa wa elimu ya fedha katikamwaka wa 2013. Mkakati huu ulitokana naushahidi uliozalishwa na mradi wa pamoja na Benki ya Dunia, na mafunzo yanalenga wakati ambapo wanaoweza kuhama wanakabiliwa na maamuzi makubwa ya kifedha. Shirika la Elimu ya Fedha la Morocco liliungana na Shirika la Kazi Duniani katika kuanzisha mipango ya elimu ya fedha kwa wahamiaji huko Morocco. Huko Romania, Shirika la

Kimataifa la Uhamiaji (International Organization for Migration) lilizindua mpango kwa ushirikiano na MasterCard Foundation ili kuunga mkono kujumuishwa kwa wahamiaji na wakimbizi, huku wakipa kipaumbele vikundi vinavyoweza kuathirika kwa urahisi, ikiwa ni pamoja na watoto, wanawake na watu wenye mahitaji maalum.

Hata wakiwa na elimu nzuri ya fedha, huenda wahamiaji wakawa hawajui masharti ya kifedha na vipengele vya bidhaa za kifedha. Huenda wakawa hawana imani na taasisi za fedha, nyumbani na wanakohamia. Mara nyingi, wahamiaji wasio na hati rasmi na wale wapya huogopa kuwa taarifa binafsi wanayoombwa ili wapate huduma za kifedha itatumiwa kuwatambua na hata labda kuwarejesha nchini mwao. Sekta ya kifedha haina bidhaa muhimu na zinazozingatia tamaduni mbalimbali za wahamiaji na familia walizoacha nyumbani.

Ushahidi wa athari za elimu ya fedha kwa ustawi wa kiuchumi wa wahamiaji umechanganyika. Utafiti wa wahamiaji kutoka India huko Qatar ulionyesha kwamba elimu ya fedha ilileta tofauti, hata kama ndogo, katika maamuzi ya kifedha. Tafiti zilizofanywa nchini Australia na New Zealand zilionyesha kwamba miradiya elimu ya fedha haikuathiri sana matumizi ya benki rasmi.

# Ufurushwaji


Idadi ya watu waliofurushwa makwao sasa ndio imefika juu zaidi tangu mwisho wa Vita Kuu vya Pili vya Dunia. Mara nyingi, watu hawa huwa wametoka baadhi ya sehemu maskini na zilizopungukiwa zaidi duniani,na hatari inayowakabili huongezeka wakati wahamiaji wananyimwa nafasi ya kupata elimu.

Kuna wakimbizi milioni 19.9 chini ya ulinzi wa Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa Wakimbizi (UNHCR), ambao asilimia 52 hawajafikisha miaka 18. Kuna wakimbizi milioni 5.4 kutoka Upalestina chini ya ulinzi wa Shirika la Usaidizi na Kazi la Umoja wa Mataifa kwa Wakimbizi wa Wapalestina huko Mashariki ya Kati (UNRWA). Karibu asilimia 39 ya wakimbizi wanaishi katika kambi zilizosimamiwa, za kujitengenezea au za wasafiri au vituo vya ujamaa, hasa katika mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara. Wengi wa wanaosalia wanaishi katika malazi binafsi katika maeneo ya mijini.

> “Hatari inayowakabili waliofurushwa makwao huongezeka wanaponyimwa nafasi ya kupata elimu”

Aidha, mapigano yamewaacha watu milioni 40 wakiwa wakimbizi wa ndani (IDPs), idadi kubwa zaidi ya wakimbizi hawa ikiwa Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, huku wengine milioni 19 wakilazimika kuhama makwao kutokana na majanga ya asili. Wengi kati ya hawa wako Uchina.

**MCHORO WA 3:**
**Ni asilimia 11 tu ya wakimbizi katika nchi za kipato cha chini wanaopata masomo ya sekondari**
*Asilimia ya wakimbizi wenye umri wa miaka 5 hadi 17 walio shuleni, kwa misingi ya kiwango cha elimu, 2017*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig4_2
*Chanzo:* UNHCR (2018).

## Wakimbizi wengi wako nyuma katika kupata elimu na elimu bora

Kutambua hali ya elimu ya wahamiaji ni changamoto, lakini shirika la UNHCR linakadiria kuwa kuna asilimia 61 katika shule za msingi na asilimia 23 katika shule za sekondari. Katika nchi za kipato cha chini, idadi ilikuwa chini ya asilimia 50 katika shule za msingi na asilimia 11 katika sekondari **(Mchoro wa 3)**. Kwa jumla, karibu wakimbizi milioni 4 wenye umri wa miaka 5 hadi 17 hawakuwa shuleni katika mwaka wa 2017.

Asilimia ya wakimbizi wanaenda shule inaweza kutofautiana sana katika nchi. Katika mwaka wa 2016, asilimia ya wakimbizi waliojiunga na shule za sekondari nchini Ethiopia ilikuwa tofauti katika kila wilaya, Samara ikiwa na asilimia 1 huku Jijiga ikiwa na asilimia 47. Katika mwaka wa 2011 huko Pakistan, asilimia ya wakimbizi kutoka Afghanistan waliokuwa wamejiunga na shule ya msingi (asilimia 29) ilikuwa chini ya nusu ya asilimia ya kitaifa (asilimia 71), huku asilimia ya wasichana wakimbizi wa Afghanistan (asilimia

18) ikiwa nusu ya ile ya wavulana (asilimia 39) na pia chini ya nusu ya asilimia ya wasichana waliohudhuria shule huko Afghanistan. Mara nyingi wakimbizi huenda katika maeneo ya nchi yasiyo na shule za kutosha. Wakimbizi nchini Uganda kutoka Sudan Kusini hukaa katika eneo maskini la Magharibi mwa Nile (West Nile), ambapo jumla ya waliohudhuria masomo ya sekondari ilikuwa chini ya nusu ya asilimia ya kitaifa mwaka 2016.

Hakuna taarifa nyingi kuhusu ubora wa elimu ya wakimbizi, lakini ambapo data zinapatikana, hali yake inavunja moyo. Katika kambi ya wakimbizi ya Dadaab nchini Kenya, asilimia 8 ya walimu wa shule za msingi wana vyeti vya kuhitimu vya kitaifa, na walimu 6 kati ya 10 wanaowafundisha wakimbizi hawajapata mafunzo.

### KUFUATILIA JINSI ELIMU YA WAHAMIAJI INAVYOENDELEA SI RAHISI

Katika nchi nyingi zilizoathiriwa na mapigano, ukimbizi wa ndani umeongezea mzigo mifumo ya elimu ambayo tayari si imara. Katika kaskazini-mashariki mwa Nigeria, tathmini ya hivi karibuni ya mahitaji ya elimu ilipata kuwa katika shule 260, asilimia 28 zimeharibiwa na risasi, makombora au marisau, asilimia 20 zimechomwa kimakusudi, asilimia 32 zimeporwa na asilimia 29 ziko karibu na makundi yenye silaha au ya kijeshi.

Kufikia Januari 2018, shirika la UNHCR liliripoti kuwa watu milioni 1.8 walikuwa wakimbizi wa ndani nchini Ukraine. Katika Dnipro, Kharkiv, Kiev na Zaporizhzhia, maeneo ambayo yana wakimbizi wengi wa ndani, taasisi za elimu zinakabiliwa na uhaba wa nafasi ya madarasani na rasilimali. Ili kukabiliana na uhaba huu, serikali imetenga sehemu zaidi za shule, ikahamisha vyuo vikuu vya serikali kutoka maeneo yenye mapigano, ikarahisisha taratibu za kuingia shuleni, ikagharamia mafunzo ya ziada na ikatoa vichocheo kama vile mikopo na vitabu kwa ajili ya wakimbizi wa ndani (IDP).

Maafa ya asili pia hukatiza elimu, hasa huko Asia na Pasifiki. Ufilipino hupatwa na takriban dhoruba 20 kwa mwaka na imo hatarini ya kupatwa na mlipuko wa volkano, mitetemeko ya ardhi na maporomoko ya ardhi. Nchi hii imechukua hatua za kupunguza hatari za maafa na kuwepo kwa shule zisizoathiriwa na dhoruba, zenye vifaa vya kufundisha kumesababisha ongezeko la wastani wa miaka 0.3 ya elimu.

## Wakimbizi wanahitaji kujumishwa katika mifumo ya kitaifa ya elimu

Serikali nyingi zinapokabiliwa na migogoro, mara nyingi huwa zinaamua kuwapatia wakimbizi elimu kupitia mfumo sambamba. Hata hivyo, kumekuwa na makubaliano kuwa suluhisho hili si endelevu. Mara nyingi ufurushwaji hudumu kwa muda. Kwa kawaida, mifumo sambamba huwa haina walimu waliohitimu. Mitihani yake haitambuliwi rasmi. Vyanzo vya ufadhili vinaweza kukatizwa wakati wowote.

Mkakati wa kimataifa wa elimu wa UNHCR wa 2012-2016 ulihimiza nchi, kwa mara ya kwanza, ziwapatie watoto wakimbizi fursa za kujifunza zilizokubaliwa na kutambuliwa rasmi ili waweze kuendelea na elimu yao. Lengo lake ni kuwahusisha wakimbizi kikamilifu katika mfumo wa elimu ya kitaifa ili waweze kujifunza katika darasa moja na watoto wenyeji, baada ya kupata mafunzo mfupi ya kuwasaidia kuwafikia wenzao, ikiwa watayahitaji, ili kuwaandaa kuingia shuleni katika madaraja yanayolingana na umri walio nao. Lakinikiwango cha kujumuishwa kwa wakimbizi hutofautiana katika miktadha mbalimbali ya uhamisho. Eneo husika, historia, upatikanaji wa rasilimali na uwezo wa mfumo huathiri hali ya kujumuishwa inayoendelea kubadilika.

> “Lakini kiwango cha kujumuishwa kwa wakimbizi hutofautiana katika miktadha mbalimbali ya uhamisho. Eneo husika, historia, upatikanaji wa rasilimali na uwezo wa mfumo huathiri hali ya kujumuishwa inayoendelea kubadilika”

Wakati mwingine, hatua ya kuanza kujumuisha imefanyika polepole. Nchi ya Uturuki, ambayo ina wakimbizi milioni 3.5, ilianza kwa kutambua shule zisizo

za umma kama vituo vya elimu vya muda, kisha ikavitambua kama shule za mpito, na kufikia mwaka wa 2020, watoto wote wa Syria watajumuishwa katika shule za umma. Katika hali nyingine, ahadi ya serikali imekuwa ikikatizwa. Katika Jamhuri ya Kiislam ya Iran, sera ya kujumuishwa kwa wakimbizi kutoka Afghanistan imekumbwa na matatizo mara kwa mara katika kipindi cha miongo minne.

Katika matukio kadhaa, ahadi ya kujumuisha huwa haifikiwi kikamilifu licha ya kujitolea kuitimiza. Wakimbizi wanaweza kutumia mtalaa, mitihani na lugha ya kufundisha ya nchi walimokimbilia lakini wakose kujumuishwa kikamilifu kwa kuwa wako katika maeneo tofauti ya kijiografia, kama ilivyo katika kambi nchini Kenya, au wakose nafasi za kutosha, kama katika shule za zamu mbili huko Lebanon na Jordan. Hata nchi zilizo na rasilimali zaidi, kama vile Ugiriki, zimekabiliwa na changamoto katika kutoa elimu kwa wakimbizi kupitia mfumo wa kitaifa.

Katika mazingira kadhaa, bado wakimbizi hupata elimu yao kando. Mfumo wa elimu nchini Palestina ni wa kipekee. Wakimbizi kutoka Burundi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wakimbizi wa Karen kutoka Myanmar, walio nchini Thailand wanahudhuria shule tofauti za jumuiya na zisizo rasmi au za binafsi.

## VIKWAZO VINGI VINAVYOZUIA UJUMUISHAJI VINAHITAJI KUTATULIWA

Ugumu unaohusiana na kujumuishwa kwa wakimbizi katika mifumo ya kitaifa ya elimu huonekana sana katika hali ambapo hakuna uwezowa kutosha na kuna haja kubwa ya kuwa na uratibu na mipango. Mipango inahitaji kutambua masuala kama vile ukosefu wa nyaraka na ujuzi finyu wa lugha, na kukatizwa kwa elimu na umaskini.

Taasisi ya kimataifa ya UNESCO ya Mipango ya Elimu imeanzisha mwongozo juu ya mipango ya elimu ya mpito inayozingatia mahitaji ya haraka na kujumuisha wakimbizi nje na wa ndani. Nchi ya Chad ndiyo ilikuwa ya kwanza kutengeneza mpango kama huo katika mwaka wa 2013. Katika mwaka wa 2018, serikali ilibadilisha shule 108 katika makambi na maeneo ya wakimbizi 19, kuwa shule za kawaida za umma.

> “Kutokuwa na hati tambulishi, kutojua lugha husika, ukosefu wa masomo na gharama fiche ni sababu zinazoweza kuzuia ujumuishaji kamili”

Mara nyingi, wakimbizi hukosa hati tambulishi, jambo ambalo hutatiza kufikia mifumo ya elimu ya taifa. Katika Jordan, wakimbizi walihitaji kuwa na ‘kadi ya huduma’ ili kwenda shule, na kupata kadi hiyo kulihitaji cheti cha kuzaliwa. Hata hivyo, mwishoni mwa mwaka wa 2016, Jordan ilianza kuruhusu shule za umma kuandikisha watoto bila kadi za huduma.

Kutojua lugha ya nchi walikohamia ni kizuizi kingine. Wakimbizi kutoka Burundi nchini Rwanda huingia kozi ya mafunzo ya kina inayochukua miezi sita, kisha wanajiunga na shule za umma wakifikia umulisi unaohitajika wa Kiingereza. Masomo ya maandalizi, kama yanavyotolewa nchini Ujerumani, yanaweza kusaidia, lakini huwa yanachukua muda mrefu, jambo ambalo linaweza kuwafanya wakimbizi wasijiunge na mfumo wa elimu. Mahitaji ya lugha ya wakimbizi si kuwasiliana kwa maneno tu bali pia mawasiliano yasiyohusisha maneno. Wakimbizi wanaweza kujifunza mawasiliano haya kwa kutagusana na wenyeji.

Watoto wakimbizi wanahitaji aina mbalimbali za mipango - masomo ya ziada, ya kujirekebisha, ya kuwasaidia kufikia viwango vya masomo vya wenyeji - ili waweze kupata elimu tena. Mpango wa kujifunza kwa haraka wa Baraza la Wakimbizi la Norway huko Dadaab unafupisha mtalaa wa miaka minane nchini Kenya kuchukua miaka minne, na una alamambalimbali za kuingia na kuondoka. Mpango huu umewawezesha wavulana zaidi kupata elimu, ingawa idadi ya wasichana imekuwa chini. Hata hivyo, mipango kama hiyo inapaswa kutolewa na serikali na kujumuishwa katika mipango ya sekta ya elimu.

Hata wakati elimu ni bure, gharama kama vitabu na usafiri inaweza kuwa juu. Mradi wa majaribio nchini Lebanon, ambao ulitoa fedha za kugharamia usafiri na kufidia mapato ambayo watoto watakosa wakihudhuria shule badala ya kufanya kazi uliongeza mahudhurio kwa siku 0.5 hadi 0.7 kwa wiki au takriban asilimia 20. Serikali ya Uturuki imepanua uhamisho wa kifedha wenye masharti kwa wakimbizi na ilikuwa imefikia watoto 368,000 kutoka Syria kufikia 2018.


## MAFANIKIO KATIKA KUJUMUISHA YANATEGEMEA WALIMU

Maeneo yote yenye wakimbizi yanakumbwa na uhaba wa walimu, hasa walimu waliohitimu. Kusajili wanafunzi wote wa Syria walio nchini Uturuki kutahitaji walimu zaidi ya 80,000. Nchini Ujerumani, waelimishaji 18,000 na walimu 24,000 wanahitajika. Uganda inahitaji walimu 7,000 wa shule za msingi kwa ajili ya elimu ya wakimbizi.

Malipo sawa na yanayoweza kukisiwa kwa walimu huhakikisha kuna walimu wa kutosha na huathiri ajira, uhifadhi na motisha. Hata hivyo serikali na washirika wanaotoa msaada wanaweza wakatatizika kugharamia mishahara kutokana na bajeti finyu na misaada inayodumu kwa muda mfupi tu. Kutumia walimu wa kujitolea, mara nyingi wakimbizi, na kuwalipa posho ni jambo la kawaida lakini tofauti hizi za malipo zinaweza kusababisha mvutano.

Walimu katika mazingira ya uhamisho wanahitaji mafunzo ili kukabiliana na madarasa yenye msongamano wa wanafunzi, wenye umri mbalimbali au wanaozungumza lugha mbalimbali, lakini mara nyingi hupokea msaada huu mara kwa mara.Nchini Lebanoni, asilimia 55 ya walimu na wafanyakazi walikuwa wamehusika katika maendeleo ya kitaaluma katika miaka miwili iliyopita, ingawa uwepo wa watoto wa wakimbizi uliathiri kazi yao ya kufundisha ya kila siku. Mbinu zinazotumiwa kuwasaidia walimu katika kambi ya Kakuma, Kenya, ni pamoja na mafunzo rasmi ya diploma na vyeti yanayotolewa na chuo kikuu cha kitaifa na kozi isiyo rasmi, ambayo bado haijaidhinishwa, ya walimu wa shule za msingi katika mgogoro, iliyoanzishwa na shirika la Inter-Agency Network for Education in Emergencies.

> “Walimu katika mazingira ya uhamisho wanahitaji mafunzo ili kukabiliana na madarasa yenye msongamano wa wanafunzi, wenye umri mbalimbali au wanaozungumza lugha mbalimbali, lakini mara nyingi hupokea msaada huu mara kwa mara”




Mara nyingi wakimbizi ambao ni walimu huwa hawajumuishwi katika mipango ya mafunzo ya kitaifa kwa sababu ya kanuni za kitaalamu za haki ya kufanya kazi. Nchi zingine zinawasaidia wakimbizi ambao ni walimu kurudi kazi. Nchi ya Chad imewapa mafunzo na kuwaidhinisha walimu kutoka Sudan kufanya kazi katika shule nchini humo. Nchini Ujerumani, Mpango wa Chuo Kikuu cha Potsdam unalenga walimu wakimbizi unanuia kuwawezesha walimu kutoka Syria na walimu wengine ambao ni wakimbizi kurudi darasani.

Viwango vya kuenea kwa mfadhaiko baada ya kiwewe kati ya wanafunzi ni kati ya asilimia 10 na asilimia 25 katika nchi za kipato cha juu na kufikia hadi asilimia 75 katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Ambapo huduma za

afya ya akili kwa watoto hazipatikani, shule inaweza kuwa mahali pekee ambapo msaada huo unaweza kupatikana. Hata hivyo, usaidizi unaotolewa shuleni unahitaji wataalamu wenye ujuzi na walimu hawana ujuzi kama huu. Badala yake, walimu wanaweza kutoa msaada wa kisaikososiolojia kwa kuhakikisha mazingira salama na faafu kupitia ushirikiano na wanafunzi na shughuli zinazogusia masuala ya jamii na tabia na mawazo binafsi. Wanahitaji mafunzo ya kitaalamu katika usimamizi wa darasa na njia za kuelekeza ili kupata usaidizi.

## WAKIMBIZI WANAHITAJI ELIMU YA CHEKECHEA

Hatua zinazofaa, zikiwemo elimu ya chekechea na utunzaji wa watoto wachanga (ECEC), ni muhimu kwa watoto wadogo katika mazingira yenye vurugu ambao vinginevyo hawana mazingira mazuri, ya kukuza na ya kuimarisha. Hata hivyo, katika mazingira mengi ya uhamisho mahitaji ya kujifunza mapema hayatimizwi.

Utafiti wa nchi nane zenye kipato cha kati na juu unaonyesha kuwa hatua za kukidhi mahitaji ya watoto wakimbizi na wanaotafuta uhifadhi zimekuwa 'dhaifu sana'. Jambo hili linaonyesha kuwa suala hili halijapewa kipaumbele katika uamuzi wa sera za kitaifa na majukumu ya kupanga na kutekeleza yametawanyika. Ukaguzi wa Mipango ya Msaada wa Kibinadamu na kwa Wakimbizi unaonyesha kuwa karibu nusu ya mipango hii haijataja mafunzo au elimu kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 5, na chini ya theluthi moja ndiyo inataja hasa elimu ya msingi au ECEC.

Pengo hili mara nyingi hujazwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji ilijaribu mpango wa kutoa mafunzo kwa walimu wa chekechea ulioitwa 'Healing Classrooms'. Mpango huu uliwalenga watoto kutoka Kongo waliokuwa katika kambi huko Burundi na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mpango huo ulianza kutumiwa na Lebanon katika mwaka wa 2014, ambapo sasa unahudumia watoto 3,200 wa chekechea na umetoa mafunzo kwa walimu 128. Baada ya majaribio ya miezi minne, washiriki wa umri wa miaka 3 walionyesha uweza bora wa kutembea, ujuzi wa kijamii na kihisia, uwezo wa kutekeleza mambo na kusoma na kuandika pamoja na kuhesabu.

Nchi zingine zimeanzisha ushirikiano na watendaji wengi wa ndani na wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Serikali ya Ethiopia inawasaidia watoto watatu kati ya watano wakimbizi wenye umri wa miaka 3 hadi 6 katika vituo 80 vya huduma na mafunzo kwa watoto wachanga katika kambi, na shule 150 za chekechea za binafsi na za umma huko Addis Ababa. Serikali ya Ujerumani imepitisha mpango wa kina wa elimu ya wakimbizi na wanaotafuta uhifadhi, kwa ushirikiano na watendaji katika maeneo mbalimbali ya taifa. Pia inapanga kuwekeza karibu yuro milioni 400 katika mwaka wa 2017-2020 ili kupanua mipango wake wa ECEC na kuongeza wafanyakazi.

## ELIMU YA WAKIMBIZI WENYE ULEMAVU IMO HATARINI

Vyombo vya sheria vya kimataifa vinahakikisha haki za elimu kwa watoto wenye ulemavu, lakini rasilimali zinazofaa hazipatikani. Ulemavu ulikuwa unapimwa kupitia kutambua kwa macho, kupimwa hospitalini au taarifa iliyotolewa kwa hiari, jambo ambalo lilisababisha kupuuzwa kwa hali na kiwango cha ulemavu miongoni mwa wakimbizi. Njia za hivi karibuni zitumia maswali yenye utaratibu, yanayolenga utendaji, kama vile yaliyoandaliwa na kampuni ya Washington Group.

> “Shule maalum katika maeneo ya uhamisho ni chache au hazipatikani, na huwa zinalipisha ada”

Kukabiliana na ulemavu kunaweza kutofautiana sana kulingana na aina na mbinu zilizowekwa za kusaidia Utafiti kati ya Waafghan nchini Pakistan ulionyesha kuwa kulikuwa na uwezekano mkubwa wa wale walio na matatizo ya kuona kuhudhuria shule (asilimia 52); uwezekano wa wale walio na matatizo ya kujitunza walitegemea ulikuwa mdogo (asilimia 7.5).

Uwezo finyu wa ufikivu kwa mtu binafsi - kama umbali na vifaa - na ukosefu wa mafunzo kwa walimu ni vikwazo vikubwa kwa watoto wakimbizi wenye ulemavu, kama ilivyopatikana nchini Indonesia na Malaysia. Shule maalum katika maeneo ya uhamisho ni chache au hazipatikani, na huwa zinalipisha ada. Huenda ulemavu pia ukafichwa au kutoripotiwa sana kutokana na hofu ya unyanyapaa wa kijamii au kukataliwa na mamlaka ya uhamiaji au serikali. Hata hivyo, changamoto hizo zinaweza kushughulikiwa. Kambi mpya za wakimbizi zinajumuisha miundombinu yenye ufikivu, kama ilivyo katika Jordan.

Ni muhimu kutambua na kushirikiana kwa misingi ya uwezo walio nao wenyeji na wakimbizi. Mradi wa shirika la Taifa la Umoja wa Watu wenye Ulemavu nchini Uganda unalenga kuhusisha wakimbizi wenye ulemavu katika shughuli za maendeleo. Chama cha Taifa cha Viziwi nchini Uganda kina shule za watoto walio na matatizo ya kusikia zilizo karibu na makazi mawili ya wakimbizi.

## TEKNOLOJIA INAWEZA KUWASAIDIA WATU WALIOFURUSHWA KUPATA ELIMU

Mara nyingi ufurushwaji huathiri mifumo ya elimu. Ufumbuzi wa teknolojia, unaowezesah kufikia wengi kwa haraka, wenye kasi na unaoweza kubebwa popote, unaweza kusaidia kujaza pengo la ukosefu wa rasilimali za kawaida za elimu. Mpango wa Instant Network Schools, ambao ulianzishwa kwa ushirikiano wa UNHCR na Vodafone, unafikia zaidi ya wanafunzi 40,000 na walimu 600 katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Sudan Kusini na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutoa internet, umeme na maudhui dijitali.

Changamoto ya masuluhisho kama hayo ni kuwa mara nyingi huwa yanatoa maudhui ambayo hayaambatani na mitalaa ya kitaifa. Kuna baadhi ambayo ni tofauti, kama vile Tabshoura (Chalk) nchini Lebanoni, ambayo hutoa rasilimali za mtandaoni kwa shule za chekechea kulingana na mtalaa wa mwaka wa 2015. Masomo haya yanayopatikana katika Kiarabu, Kiingereza na Kifaransa, yanatumia Moodle, mfumo wa usimamizi wa kujifunza.

Teknolojia pia inaweza kutoa msaada wa kisaikososiolojia. The Ideas Box, kifurushi kilichoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Libraries Without Borders pamoja na UNHCR, kinajumuisha rasilimali za habari na utamaduni, pamoja na maudhui ya elimu. Tathmini ya ubora katika kambi mbili za Burundi za wakimbizi kutoka Kongo ilionyesha kuimarika kwa ustahimilivu.

Mipango mingi inasaidia walimu kujiendeleza kitaaluma. Nchini Nigeria, mradi wa elimu ya mwalimu wa UNESCO, kwa kushirikiana na Nokia, ulisaidia walimu kupanga masomo, kuuliza maswali ya kuchochea, kutoa majibu baada ya kutafakari na kutathmini wanafunzi katika lugha ya Kiingereza na uwezo wa kusoma na kuandika.

Masuluhisho ya teknolojia yana changamoto zake. Yanahitaji uwekezaji wa juu ili kuanza kutumia, na kila mtu hana umeme na muunganisho wa kutosha. La muhimu ni kuwa teknolojia haiwezi kuchukua nafasi ya kushiriki katika shule rasmi. Mashirika ya kimataifa yanatakiwa kuhakikisha kuwa mipango inaratibiwa kwa njia bora na inatumika kutimiza lengo kuu la kuhusisha wakimbizi katika mifumo ya kitaifa ya elimu.

## MIPANGO MBALIMBALI YA ELIMU YA JUU HUKIDHI MAHITAJI YA WAKIMBIZI

Nafasi za kupata elimu ya juu huongeza uwezekano wa wakimbizi kupata ajira na kuchangia katika idadi ya wanaojiunga na kuendelea na shule za msingi na za sekondari. Hata hivyoidadi ya wakimbizi inayoshiriki katika masomo ya juu inakadiriwa kuwa asilimia moja tu. Mara nyingi, ufikiaji hutelekezwa wakati wa dharura na kuangaliwa kwa utaratibu tu wakati ufurushwaji umedumu kwa muda mrefu. Mara nyingi haki za elimu kwa wakimbizi hutafsiriwa kuwa nje ya mipaka ya ubaguzi.

> “Ni asilimia moja pekee ya wakimbizi ambayo inashiriki katika masomo ya juu”

Mipango inayotumia teknolojia inaweza kufikia watu waliofurushwa makwao. Ubia wa Kujifunza kwa Pamoja katika Mazingira ya Mgogoro (Connected Learning in Crisis Consortium), uliozinduliwa na UNHCR na Chuo Kikuu cha Geneva, unachanganya mafunzi ana kwa ana na ya mtandaoni, na umefikia wanafunzi 6,500 tangu 2010.

Mipango ya ufadhili wa masomo kwa wakimbizi ni pamoja na Mfuko wa Albert Einstein German Academic Refugee Initiative Fund (DAFI), ambao umekuwa ukiwasaidia wakimbizi kupitia UNHCR tangu mwaka wa 1992. Eneo linalozingatiwa hurekebishwa kulingana na harakati za wakimbizi na mahitaji ya elimu. Kwa sasa, miradi mikubwa zaidi iko Ethiopia,Jamhuri ya Kiislam ya Iran, Lebanon, Uturuki na Uganda.

Mipango mingine ya ufadhili wa masomo hutoa fursa ya kujifunza katika nchi za kipato cha juu. Mpango wa Wanafunzi Wakimbizi wa World University Service of Kanada unasaidia kamati za vyuo vikuu zinazotaka kufadhili wakimbizi wahamie na kusomea katika taasisi zao. Tangu mwaka wa 1978, mpango huu umeleta wakimbizi zaidi ya 1,800 kutoka nchi 39 katika zaidi ya vyuo vikuu na vya elimu 80 nchini Kanada.

Huenda wahadhiri pia wakahitaji usaidizi. Muungano waa Wasomi walio Hatarini (Scholars at Risk) hupanga utafiti wa muda na nafasi za kufundisha kwa wasomi wanaohitaji ulinzi. Halmashauri ya Wasomi walio Hatarini (CARA) nchini Uingereza hutoa msaada wa dharura, hasa kwa wasomi walio hatarini katika nchi zao asili.

Faida za usaidizi zinapaswa kufaidi jumuiya kwa jumla. Ufadhili wa DAFI unatambua jumuiya za asili kama wanaotarajiwa kufaidika, kando na anayepokea ufadhili. Mitandao ya kusaidia wasomi wakimbizi pia inaweza kuendeleza ukuzaji uwezo. Halmashauri ya CARA imezindua mipango ya kujenga uwezo wa utafiti na ufundishaji nchini Iraq, Jamhuri ya Kiarabu ya Syria na Zimbabwe.

## Wakimbizi wa ndani hukabiliwa na changamoto za elimu sawa na zile za wakimbizi

Ijapokuwa Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Ufurushwaji wa ndani zinasema kuwa kila mtu ana haki ya kupata elimu, uwezo na siasa huzuia utambuzi wa tatizo na uratibu wa masuluhisho. Mara nyingi masuluhisho ya kisheria, kielimu na kiutawala kwa shida ya elimu kwa wakimbizi wa ndani huwa sawa na yale yaliyohusishwa na wakimbizi.

Serikali ya Colombia, ambapo kulikuwa na wakimbizi wa ndani milioni 6.5 kufikia mwaka wa 2017, imezingatia mwongozo wa ulinzi wa kisheria. Katika mwaka wa 2002, Mahakama ya Katiba iliamuru mamlaka ya elimu ya manispaa kuwapatia kipaumbele watoto waliofurushwa makwao katika suala la kupata elimu. Katika mwaka wa 2004, mahakama ilitangaza kuwa haki za msingi za wakimbizi wa ndani, ikiwa ni pamoja na haki ya elimu, zilikuwa zinakiukwa.

> “Mara nyingi walimu waliofurushwa makwao hukabiliwa na hatari na vikwazo vya usimamizi ambavyo hutatiza kupata mishahara”

Ufurushwaji unamaanisha kuwa maendeleo ya elimu ya watoto na vijana wengi yanakatizwa na wanahitaji kusaidiwa kujiunga tena na mfumo wa elimu. Katika Afghanistan, shirika lisilo la kiserikali la Watoto katika Mgogoro (Children in Crisis) huendesha mpango wa kijamii unaochukua muda mfupi wa kuwasaidia wanafunzi wa waliofurushwa makwao ambao hawaendi shuleni wanaoishi katika makazi yasiyo rasmi ndani ya na karibu na Kabul kukamilisha darasa la 6 na kujiunga na elimu rasmi.

Mara nyingi walimu waliofurushwa makwao hubaki chini ya usimamizi wa utawala wa wilaya yao ya nyumbani, jambo ambalo hutatiza kupokea mishahara, kama katika Jamhuri ya Kiarabu ya Syria. Nchini Iraq, washirika 44 hutoa huduma katika taarafa 15 na kusaidia karibu walimu 5,200 na mishahara na vichocheo, ingawa uratibu mbaya umesababisha mapengo katika huduma, tofauti katika malipo kati ya makundi ya walimu na mvutano kati ya washirika.

## Maafa ya asili na mabadiliko ya tabianchi yanahitaji mifumo ya elimu kuwa tayari na kuweza kuchukua hatua

Mipango ya sekta ya elimu inahitaji kuzingatia hatari za kupoteza maisha, uharibifu wa miundombinu na uhamaji kutoka kwa majanga ya asili na kuhakikisha kuwa huduma za elimu haziathiki sana, kwanzia kuchukua hatua za dharura hadi kurejea katika hali shwari. Katika mwaka wa 2017, Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupunguza Hatari za Maafa pamoja na Umoja wa Kimataifa wa Kupunguza Hatari ya Maafa na Uimarishaji katika Sekta ya Elimu

walizindua mwongozo wa Kina wa Usalama Shuleni. Nguzo zake tatu ni mazingira salama ya kusomea, usimamizi wa maafa shuleni na kupunguza hatari na elimu ya ujasiri.

Mataifa mengi ya kisiwa cha Pasifiki huzingatia hatari za mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya elimu. Katika mwaka wa 2011, Taarifa ya Sera ya Visiwa vya Sulemani na Mwongozo wa Maandalizi ya Maafa na Elimu katika Hali ya Dharura zililenga kuhakikisha kuwa wanafunzi waliendelea kupata mazingira salama ya kujifundishia kabla, wakati wa na baada ya matukio ya dharura, na kwamba shule zote zilijenga nafasi ya kufunzia na kujifundishia ya muda.

Katika miongo michache, huenda hali ya hewa ikawa moja ya sababu kuu za kuhama. Benki ya Dunia inakadiria kuwa watu milioni 140 watafurushwa makwao kutokana na mabadiliko ya tabianchi kufikia mwaka wa 2050. Ili kupunguza hatari, baadhi ya nchi tayari zinazingatia sera za kukabiliana. Sera ya 'uhamiaji kwa heshima' ya Serikali ya Kiribati, ambayo ni sehemu ya mkakati wa muda mrefu wa kuhama unaojumuisha nchi yote, inalenga kuinua ujuzi wa watu na kuwapa zana za kupata fursa za kazi nzuri ng'ambo katika sekta kamavile ya uuguzi.

# Uanuwai

Elimu ambayo inathamini uanuwai ni muhimu kwa nchi zote, kwani huziwezesha kujenga jumuiya zenye umoja ambapo tofauti zinakubaliwa na kuheshimiwa na wote kupata elimu bora.

Wakati mwingine wahamiaji na wakimbizi huhukumiwa kwa misingi ya maoni ya kikundi walimotoka badala ya sifa za kibinafsi. Hasa ikiwa waonekana tofauti na wenyeji, wanaweza kutazamwa kama 'wengine', na kasumba na upendeleo unaweza kusababisha kutengwa, ikiwa ni pamoja na kunyimwa nafasi ya kupata elimu bora.

Upendeleo na ubaguzi zipo katika mifumo mingi ya elimu, licha ya sera dhidi yake. Ubaguzi wa kimfumo dhidi ya wanafunzi kutoka familia za wahamiaji huko Marekani unajumuisha ukosefu wa mipango ya masomo kwa lugha mbili kwa watoto wadogo na mitihani ya kusoma na kuandika ambayo haitolewi kwa lugha zao asili.

Mtazamo wa umma unachangia katika ustawi wa wahamiaji na jinsi wanavyojitazama. Kuona kama wanabaguliwa kumehusishwa na unyogovu, wasiwasi na kutojiamini. Kulingana na Utafiti wa Maadili ya Dunia wa mwaka wa 2014, ni vigumu kwa wahamiaji kujiona kama wenyeji katika nchi walikohamia.

## Elimu huathiri mitazamo juu ya wahamiaji na wakimbizi

> "Elimu inaweza kuunguza taswira hasi inayochorwa na vyombo vya habari kwa kutoa ujuzi wa kisiasa na wa kufikiri kwa umakinifu ili kutofautisha ukweli na uongo"

Kiwango cha elimu kinahusishwa na mitazamo juu ya wahamiaji. Watu wengi wenye elimu hawakuzingatia makabila yao, waliunga mkono zaidi uanuwai wa tamaduni na kuliona faida ambayo wahamiaji walileta kwa uchumi. Utafiti ulionyesha kuwa wale walio na elimu ya juu walistahimili kwa asilimia mbili zaidi ya wale walio na elimu ya sekondari, ambao kwa upande wake, walistahimili kwa asilimia mbili zaidi ya wale wenye elimu ya msingi. Vijana, hasa wenye elimu, pia huwa na mtazamo chanya zaidi kuhusu uhamiaji.

Machapisho hasi ya vyombo vya habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi yanaweza kuendeleza ubaguzi. Vyombo vya habari vinaendelea kuangazia masuala ya uhamiaji na ufurushwaji kwa njia hasi na inayopinga, kwa mfano, huko Kanada, Jamhuri ya Czech, Norway na Uingereza, ambapo mara kwa mara vyombo vya habari vinaonyesha wahamiaji na wakimbizi

kama tishio kwa utamaduni, usalama na mfumo wa ustawi. Machapisho ya vyombo vya habari kuhusu uhamiaji mara nyingi huwa ni kasumba, ambazo hazijumuishi maoni ya wakimbizi au wahamiaji na ambazo zinatumia maneno yasiyo sahihi. Elimu inaweza kuunguza taswira hasi inayochorwa na vyombo vya habari kwa kutoa ujuzi wa kisiasa na wa kufikiri kwa umakinifu ili kutofautisha ukweli na uongo.

# Kujumuishwa kunastahili kuwa katika kiini cha sera na mifumo ya elimu

Nchi hutumia mbinu tofauti za kushughulikia uanuwai katika mifumo ya elimu: kusimilisha, uanuwai wa tamaduni/ ushirikiano na mtagusano wa tamaduni / kujumuisha. Kusimilisha kunaweza kuwa hatari kwa utambulisho wa wahamiaji. Mtagusano wa tamaduni kwa upande mwingine, huwasaidia wanafunzi kujifunza sio tu kuhusu tamaduni nyingine bali kuhusu vikwazo vya miundo katika nchi za wenyeji ambavyo vinazuia usawa.

Nchi chache zina sera maalum za elimu inayozingatia tamaduni. Nchini Ireland, ambapo watoto wahamiaji walikuwa asilimia 15 ya watu chini ya miaka 15 katika mwaka wa 2015, ilianzisha Mkakati wa Elimu uliojumuisha Tamaduni mbalimbali wa 2010-2015, wenye lengo la kuendeleza uwezo wa mtoa huduma, kuendeleza ujuzi wa lugha, kukuza ushirikiano na mashirika ya kiraia na kuboresha ufuatiliaji. Sheria zaidi ziliondoa vikwazo, kupiga marufuku ada za shule na kuzihitaji shule kuchapisha sera za kuingia mle. Uchunguzi wa Bunge la Ulaya uligundua kuwa nchi za Ireland na Uswidi ndizo zilikuwa na mifumo thabiti zaidi ya ufuatiliaji na tathmini ya elimu ya wahamiaji katika Ulaya.

Athari za kisiasa zinaweza kudhoofisha sera za elimu zinazohimiza mtagusanowa tamaduni. Nchini Uholanzi, mitazamo duni inayolenga wahamiaji imesababisha kubuniwa kwa sera ya ushirikiano inayohimiza uaminifu kwa jamii ya Uholanzi; elimu inayohimiza mtagusano wa tamaduni imeondolewa na badala yake kuwekwa elimu inayohimiza uraia.

Mwelekeo mwingine katika kuwafanya wanafunzi wahamiaji wajihisi nyumbani wakiwa shuleni ng'ambo ni kuendeleza uhusiano na nchi yao asili. Hili linaweza kufanyika kupitia njia kama vile shule zilizosimamiwa au kuratibiwa na serikali ya nchi walimotoka, kama ilivyo katika Poland; shule binafsi zilizoanzishwa na jumuiya za wahamiaji, kama walivyofanya wafilipino huko Saudi Arabia au wabrazili huko Japan; na shule zisizo rasmi, zinazofundisha lugha na tamaduni za nchi walimotoka.

## MITALAA NA VITABU VYA KUSOMA VINAWAJUMUISHA WATU ZAIDI

Mitalaa na vitabu vya kusoma vinaweza kupunguza ubaguzi na kuwafanya wahamiaji wajihisi nyumbani. Kujifunza kuhusu historia ya nchi zingine kulihusishwa na mtazamo chanya wa kuunga mkono haki za makundi ya kikabila katika nchi 12 kati ya 22 zilizoshiriki katika Uchunguzi wa Kimataifa wa Elimu ya Ustawi na Uraia uliofanywa mwaka wa 2016.

Nchi zaidi zinabadilisha mitalaa ili kujumuisha uanuwai unaoendelea kuongezeka katika jamii. Miongoni mwa nchi 21 za kipato cha juu zilichambuliwa kwa ajili ya ripoti ya sera juu ya uanuwai wa tamaduni, ni nchi za Australia na Kanada pekee zilizojumuisha uanuwai wa tamaduni katika mitalaa katika mwaka wa 1980. Kufikia mwaka wa 2010, suala la uanuwai wa tamaduni lilikuwa kwenye ajenda katika zaidi ya theluthi mbili ya nchi na ulikuwa umejumuishwa kikamilifu katika nchi nne zaidi, Ufini, Ireland, New Zealand na Uswidi **(Mchoro wa 4).**


Katika mwaka 2015, nchi 27 kati ya 38 za kipato cha juu zilifunza elimu inayohimiza mtagusano wa tamaduni kama somo lililojisimamia pekee ama zikalijumuisha katika mtalaa au yote mawili. Maadili yanayoshirikiwa na tamaduni yanaweza kujumuishwa katika masomo binafsi. Mafunzo ya historia mara nyingi hujikita katika kabila husika, lakini

masomo mengine huwa tofauti, kama vile jiografia nchini Ujerumani na uraia nchini Uingereza. Baadhi ya vitabu vya kisasa bado havijumuishi masuala tata yanayohusiana na uhamiaji. Nchini Mexico, vitabu vya kusoma havitaji suala la wahamiaji wasio na hati rasmi pamoja na uhusiano na Marekani. Hata hivyo, vitabu vya kusoma huko Côte d'Ivoire vinajadili suala la wakimbizi na ufurushwaji, ambayo yamejitokeza sana tangu mgogoro wa kisiasa wa mwaka wa 2002.

Maeneo yanaweza kubadilisha mitalaa yapendavyo, kama ilivyo huko Alberta, Kanada, ambapo vifaa vya kufundisha husaidia katika mafunzo kwa wakimbizi na wahamiaji hasa jamii maalum, kama vile Wakaren, Wasomali na waliotoka Sudan Kusini. Uongozi thabiti wa shule unaweza pia kusaidia. Nchini Marekani, ambapo viongozi wa shule wanathamini uanuwai, kuna uwezekano mkubwa wa wanafunzi kushiriki katika mitagusano ya kitamaduni.

Ufundishaji unahitaji kujumuisha shughuli zinazohamasisha uwazi kwa mitazamo mbalimbali ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujuzi wa kufikiria kwa umakinifu. Kujifunza kwa kushiriki na kwa pamoja kunaweza kusaidia kuboresha mahusiano ya kitamaduni, kuongeza kukubali tofauti na kupunguza ubaguzi.

**MCHORO WA 4:**
**Nchi zaidi zinaendelea kujumuisha uanuwai wa tamaduni katika shule**
*Kuongezwa kwa uanuwai wa tamaduni katika mitalaa katika nchi 21 za kipato cha juu, 1980-2010*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig5_2
*Kumbuka:* Ufafanuzi wa anuwai wa tamaduni unakaribiana sana na ule wa mtagusano wa tamaduni katika Jedwali la 5.1 katika ripoti kuu.
*Chanzo:* Westlake (2011).

## MAFUNZO YANAYOWAANDAA WALIMU KUFUNDISHA MADARASA YENYE WANAFUNZI ANUWAI SI YA LAZIMA KATIKA NCHI NYINGI

Walimu wanahitaji usaidizi ili kufundisha madarasa yenye wanafunzi anuwai, lakini asilimia 52 ya walimu waliohojiwa nchini Ufaransa, Ireland, Italia, Latvia, Uhispania na Uingereza walihisi kuwa hawakupata usaidizi wa kutosha kutoka kwa usimamizi katika kukabiliana na uanuwai. Nchi tofauti zinajumuisha viwango tofauti vya mafunzo kuhusu uanuwai katika masomo ya walimu. Katika Uholanzi, New Zealand na Norway, wanaotaka kuwa walimu huchukua kozi za lazima za mafunzo ya kuwasaidia wanafunzi kutoka familia za aina mbalimbali. Barani Ulaya, si lazima walimu wakamilishe kozi kama hizo.

Mipango ya masomo kwa walimu huwa inasisitiza ujuzi wa jumla badala ya jinsi ya kufundisha. Uchunguzi wa mipango 105 katika nchi 49 ulionyesha kuwa ni mpango moja tu kati ya tano uliotayarisha walimu na ujuzi wa jinsi ya kutatua migogoro ya kitamaduni au kuelewa matibabu ya kisaikolojia na chaguo la rufaa kwa wanafunzi wanaozihitaji. Walimu wanaohudumu wanahitaji kuendelea kupata mafunzo ya namna ya kukabiliana na suala hili. Utafiti wa Kimataifa wa Ufundishaji na Kujifundisha wa OECD wa mwaka wa 2013 ulionyesha kwamba ni asilimia 16 tu ya walimu wa vidato vya chini vya sekondari katika mifumo 34 ya elimu waliokuwa wamepata mafunzo ya tamaduni au lugha anuwai katika mwaka uliotangulia.

Kuna tafiti chache kuhusu athari za walimu wenye asili ya wahamiaji, na zile ambazo zimefanywa huenda zisitofautishe kati ya wahamiaji wa kizazi cha kwanza na vya baadaye au kati ya walimu wahamiaji na wale wa kutoka makundi yaliyotengwa. Baadhi ya ushahidi unaonyesha kwamba uanuwai kati ya walimu unahusishwa na mafanikio, kujiamini na hisia za usalama katika mwanafunzi wahamiaji. Hata hivyo, hakuna walimu wengi wenye asili ya wahamiaji ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi huko Ulaya. Sera zenye ubaguzi katika kujiunga na taaluma hii pamoja na upendeleo katika ajira zinachangia kwa kiasi fulani katika uhaba huu.

### ELIMU INA JUKUMU LA KUZUIA UKATILI MKALI

Ukatili mkali, mashambulizi ya kigaidi na wananchi wa kawadia kulengwa na serikali na makundi mengine bila shaka usababisha uhamiaji na ufurushwaji, lakini mtazamo wa umma katika nchi za kipato cha juu umesisitiza zaidi kinyume na kuhusisha uhamiaji na ugaidi. Hata hivyo uhusiano huo ni dhaifu sana, mashambulizi yanayotekelezwa na wageni yanawakilisha sehemu ndogo ya yale yanayotekezwa na wenyeji. Aidha, njia za fanya watu wachukue misimamo mikali ni nyingi.

Kuzuia kuibuka kwa ukatili ni njia muhimu wa ulinzi dhidi ya ugaidi. Wenye misimamo mikali hutumia changamoto za maendeleo au kuzizidisha ili kuunda na kutumia mzunguko usiokoma wa kutenga, hasa unaoathiri walio masikini zaidi na wanaoweza kuathirika kwa urahisi.

> “Kwa kukuza heshima ya uanuwai, amani na maendeleo ya kiuchumi, elimu inaweza kuwa kizuizi dhidi ya kufanywa muunga mkono misimamo mikali”

Kwa kukuza heshima ya uanuwai, amani na maendeleo ya kiuchumi, elimu inaweza kuwa kizuizi dhidi ya kufanywa muunga mkono misimamo mikali. Wale wanaoendeleza ukatili mkali mara nyingi huona elimu kama tishio na hulenga shule katika mashambulizi, kama vile mashambulizi ya Boko Haram nchini Nigeria.

Kinyume chake, kunyimwa nafasi ya kupata elimu kunaweza kuongeza uwezekano wa kufanywa muunga mkono misimamo mikali. Kunyimwa nafasi ya kupata faida za elimu kuna hatari sawa. Katika nchi nane za Kiarabu, ukosefu wa ajira uliongezeka uwezekano wa kuwa na misimamo mikali miongoni mwa walioelimika zaidi ambao matarajio ya maendeleo ya kiuchumi hayakutimia.

Nchi nyingi zinajumuisha jitihada za kuzuia ukatili mkali katika mitaala, lakini vifaa vya kufundisha havilingani. Kote ulimwenguni, kitabu 1 kati ya 10 kinazungumzia njia za kuzuia mapigano kwa silaha au kujadili njia za kutatua migogoro au taratibu za upatanishaji. Hili ni ongezeko ndogo tangu miaka ya 1950.

Walimu wanaweza kukuza mitazamo ya kuvumiliana lakini wanahitaji mafunzo ya kutosha. Mbinu za mafundisho, kama kufundishana wenyewe, kujifundisha kwa kufanya majaribio, kazi za vikundi, kujifundisha kwa kuiga na mbinu zingine zinazochochea kuwaza kwa umakini na majadiliano ya wazi, zina matokeo bora zaidi. Wakati huo huo, walimu hawapaswi kuwasimamia wanafunzi wao au kupunguza uhuru wa kibinafsi katika kutafuta usalama.

Shule zinaweza kuwa mahali rahisi pa kuandaa mipango ya kuzuia ukatili mkali inayohusisha wadau nje ya elimu. Mipango mingine, ikiwa ni pamoja na Indonesia, hutumia sauti za waathirika kufanya mada muhimu zaidi na zinazofaa kwa wanafunzi. Elimu dhidi ya ukatili mkali inapaswa kuzingatia jinsia na kushirikisha wanawake na wasichana. Wakati mwingine wanawake huongoza mipango kama hiyo ya elimu. Kwa mfano, katika jimbo la Pakistani la Khyber Pakhtunkhwa, shirika la wanawake limefundisha ujuzi wa utatuzi na kukabiliana na migogoro kwa wanawake 35,000 na vijana 2,000.

## Elimu ya nje ya darasa ina jukumu muhimu lililopuuzwa katika kujenga jamii imara

Elimu na shughuli ya kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya uhamiaji na ufurushwaji pia hufanyika nje ya shule. Elimu ya nje ya darasa ni ya aina nyingi na ina madhumuni mengi. Kwa bahati mbaya, hakuna taarifa yenye utaratibu kuyahusu kwa kuwa hayatolewi na serikali.

Vituo vya jamii vina jukumu muhimu katika elimu ya nje ya darasa juu ya uhamiaji. Nchini Uturuki, Shirika Lisilo la Kiserikali la Yuva Association linatoa kozi za lugha na warsha za ujuzi kupitia vituo vya jamii. Wawezeshaji au washauri wa kitamaduni wanaweza kutoa huduma za kutafsiri na usaidizi wa kuelewa mfumo wa elimu. Manispaa ya Linköping huko Uswidi iliwafundisha wakufunzi lugha za Kisomali au Kiarabu ili wafanye kazi kama 'kiungo' katika mpango wake wa Kujifunza Pamoja (Learning Together). Miji inaweza kuongoza juhudi za kukabiliana na unyanyasaa, kama huko São Paulo, Brazil, lakini inapaswa kuhusisha jamii za wahamiaji ili iwe na mafanikio.

Sanaa na michezo ni njia muhimu za kuwezesha elimu ya nje ya darasa. Sikukuu za Jumuiya nchini Norway na Uhispania zinatoa fursa ya kubadilishana tamaduni. Timu ya soka ya Kaizer Chiefs, huko Afrika Kusini imefanya kampeni katika mitandao ya kijamii inayoonyesha mchango mzuri wa wageni nchini.

# Uhamaji wa wanafunzi na wataalamu

Katika ulimwengu unaoendelea kuwa na utandawazi, vijana wanaenda ng'ambo kupata masomo na wataalamu wenye ujuzi wanafuata nafasi za ajira huko ng'ambo ili kuendeleza vipaji vyao. Uhamiaji wa wenye ujuzi una faida, gharama na hatari kubwa kwa watu binafsi, taasisi na nchi.

## Umataifishaji wa elimu ya juu unaweza kutekelezwa kwa njia mbalimbali

> "Nusu ya wanafunzi wote wa kimataifa huhamia nchi tano zinazozungumza Kiingereza, huku asilimia 25 ya wanafunzi waliohama walikuwa wametoka nchi tatu za bara Asia"

Umataifishaji wa elimu ya juu unajumuisha 'sera na mazoea ya mifumo na taasisi za kitaaluma - na hata watu binafsi - kukabiliana na mazingira ya kitaaluma'. Unahusisha kuhama kwa wanafunzi na wahadhiri, pamoja na kozi, mipango na taasisi zinazoathiri elimu nyumbani na ng'ambo.

Nusu ya wanafunzi wote wa kimataifa huhamia nchi tano zinazozungumza Kiingereza: Australia, Kanada, New Zealand, Uingereza na Marekani. Idadi ya wanafunzi wa kimataifa nchini Ufaransa na Ujerumani imeongezeka kwa asilimia 8 na asilimia 6 mtawalia, kwa upande mmoja kwa sababu nchi hizi zinaendelea kutoa masomo ya uzamili na uzamifu kwa Kiingereza. Asilimia 25 ya wanafunzi waliohama katika mwaka wa 2016 walikuwa kutoka Uchina, India na Jamhuri ya Korea. Eneo la pili kutuma wanafunzi wengi zaidi katika nchi hizi ni Ulaya, ambalo lilituma asilimia 23 ya jumla katika mwaka wa 2016, lakini asilimia 76 ya wanafunzi milioni 0.9 kutoka Ulaya husalia katika ukanda huo.

Wanafunzi huamua watakapoenda ili kupata elimu ya juu kwa kuzingatia upatikanaji wa nafasi katika vyuo vikuu bora vya nyumbani, uwezo wa kulipa na hali ya ubora wa elimu nyumbani na ng'ambo. Sera zinazoongoza uwezo wa wanafunzi kufanya kazi pia zinaweza kuchangia. Katika kipindi cha 2011-2014, idadi ya wanafunzi kutoka India nchini Uingereza ilishuka kwa asilimia 50 baada ya mabadiliko ya sera zilizowekea vikwazo visa za kazi baada ya kuhitimu; kwa wakati huo huo, idadi ya wanafunzi hawa iliongezeka kwa asilimia 70 nchini Australia na asilimia 37 nchini Marekani. Nchi zingine, zikiwemo Uchina na Ujerumani, hujaribu kudumisha wanafunzi wa kimataifa katika masoko yao ya kazi ili kujaza pengo la upungufu wa ujuzi.

Kwa vyuo vikuu, sababu kuu ya kusajili wanafunzi wa kimataifa ni kuongeza mapato. Katika mwaka wa 2016, wanafunzi wa kimataifa walileta takribani dola bilioni 39.4 za marekani katika uchumi wa nchi hiyo. Katika nchi kadhaa za Asia ambapo watu hawapati watoto wengi na waliomo wanaendelea kuzeeka, kama vile Japan, sekta ya elimu ya juu inategemea wanafunzi wa kimataifa ili kuzuia taasisi kufungwa.

Mexico na Marekani ni miongoni mwa nchi ambazo hutumia mipango ya uhamaji kama diplomasia ya kitamaduni na misaada ya maendeleo. Baadhi ya nchi zinazotuma wanafunzi, zikiwemo Brazil na Saudi Arabia, hutoa ruzuku ya kujifunza nje ya nchi kama mkakati wa maendeleo.

Wahadhiri wanaohama kimataifa wanaweza kuwa wasomi wanaotafutwa na vyuo vikuu vyenye uwezo, wasomi walioajiriwa kujaza mapengo ya ndani au 'wasomi wa muda mfupi' wanaoendelea na kazi zao katika nchi walikohamia ili kupata shahada za uzamifu. Uhamiaji katika taasisi unaweza kufanya uhamaji wa wanafunzi wa jadi kupungua lakini kuwafaidi wanafunzi wengi wenye mahitaji tofauti ya elimu. Kozi nyingi wazi mtandaoni zinapanua upatikanaji wa elimu, hasa katika nchi zinazoendelea. Mipango ya bara, baina ya nchi na isiyozuiwa na mipaka, ikiwemo matawi ya vyuo vikuu na vituo vya elimu vya kikanda, inawezesha kupatikana kwa elimu ya kimataifa nyumbani.

# Kusawazisha viwango na kutambua vyeti vya kuhitimu huwezesha umataifishaji wa elimu ya juu

Ili kuwezesha uhamaji wa wanafunzi, huenda taasisi zikashiriki katika mahusiano na makubaliano changamano, kwa mfano mafunzo ya pamoja, uhamisho wa alama, ushirika muhimu na ushirikiano. Nchi zinaendelea kujaribu kusawazisha viwango na utaratibu wa kuhakikisha ubora katika ngazi za kimakubaliano, kikanda au kimataifa.

Kuanzishwa kwa viwango sawa vya digrii, uhakikisho wa ubora, mbinu za kutambua viwango vya kuhitimu na mipango ya kuwezesha uhamaji kwa ajili ya elimu kuliwezesha Ulaya na nchi washirika kuanzisha Eneo la Elimu ya Juu ya Ulaya (EHEA) katika mwaka wa 2010. Makubaliano haya yalikuwa matokeo ya Mchakato wa Bologna, uliozinduliwa mwaka wa 1999 na uliohusisha Tume ya Ulaya, Halmashauri ya Ulaya na wawakilishi wa taasisi za elimu ya juu, mashirika yanayohakikisha ubora, wanafunzi, wafanyakazi na waajiri kutoka kufikia sasa nchi 48, . Mkataba wa Utambuzi wa Lisbon unasimamia kutambua kiwango cha kuhitimu kati ya nchi za EHEA na umethibitishwa na nchi 53.

Maeneo mengine yanajitahidi kuiga mipango hii, ikiwa ni pamoja na Chama cha Mataifa ya Kusini Mashariki mwa Asia (ASEAN) na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika Kongamano la tatu la Eneo kuhusu Elimu ya Juu, nchi za Amerika ya Kusini na Karibi zilikubali kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika elimu ya juu. Ili kuendeleza mipango kama hiyo, shirika la UNESCO limeandaa Mkataba wa Kimataifa juu ya Kutambuliwa kwa Vyeti vya Kuhitimu katika Elimu za Juu utakaoidhinishwa katika mwaka wa 2019.

### MIPANGO YA UBADILISHANAJI WA WANAFUNZI HUKO ULAYA INATOA MAFUNZO KWA ASIA YA KUSINI MASHARIKI

Kuweka mipango ya kubadilishana wanafunzi katika ukanda huongeza fursa za wanafunzi kuhama kwa muda. Chini ya mpango wa Erasmus, ulioanzishwa mwaka wa 1987 na kupanuka kama Erasmus + mwaka wa 2014, wanafunzi wanaoshiriki wanajifunzakwa kipindi cha miezi 3 hadi 12 katika nchi nyingine ya Ulaya, na taasisi za nyumbani zinaongeza wakati huu katika muda wa digrii zao. Lengo lake ni kuimarisha ufahamu wa tamaduni mbalimbali, ujuzi na nafasi za kazi kwa washiriki pamoja na kukuza ushirikiano wa kijamii katika Ulaya.

Washiriki 9 kati ya 10 waliripoti kwamba kushiriki kuliwaongezea ujasiri, uvumilivu na kukapanua mtazamo wao wa maisha kwa jumla. Kuna ushahidi unaoonyesha kwamba uwezo wa wanafunzi wa Ulaya kusafiri kwingine

uliwaongezea nafasi za kupata kazi. Hata hivyo, tathmini ambazo hudhibiti sababu zinazowafanya wanafunzi kuhama hutoa picha sahihi zaidi ya usawa. Takribani asilimia 4.4 ya wanafunzi wa Uingereza wenye wazazi waliosoma walishiriki Erasmus + katika mwaka wa 2015/16, ikilinganishwa na asilimia 2.8 ya wanafunzi wenye wazazi wasio na ujuzi. Pengo hili limeongezeka kadri muda unavyopita.

Katika mwaka wa 2015, ASEAN na Umoja wa Ulaya zilizindua mpango wa Umoja wa Ulaya kusaidia kuimarisha Elimu katika eneo la ASEAN (SHARE) ili kuunga mkono usawazishaji wa mifumo ya elimu ya kiufundi katika eneo hilo. Vikwazo vinavyozuia kuongezeka kwa usafiri wa wanafunzi vinatokana wadau wa eneo kutotia juhudi thabiti. Tofauti na Ulaya, mifumo ya kuhamisha alama hutofautiana sana kati ya nchi za ASEAN.

# Kutambua sifa za kitaaluma huongeza faida za uhamaji wa wafanyakazi kimataifa

Kutambua sifa za kitaaluma huwezesha na kuongeza faida za uhamiaji wa wanyakazi wenye ujuzi. Katika nchi za OECD, zaidi ya theluthi moja ya wahamiaji wana ujuzi zaidi ya unaohitajika katika kazi wanazofanya, ikilinganishwa na robo moja ya wenyeji. Nchini Marekani, mapato wanayopoteza wahamiaji waliohitimu chuo kikuu wanaofanya kazi zilizo chini ya kiwango chao cha kuhitimu, yanatoshana na dola za Marekani bilioni 10.2 za mapato ya kodi yanayopotea kila mwaka.

Lakini mara nyingi mifumo tambuzi huwa haijatengenezwa kikamilifu au imegawanyika kiasi kwamba haiwezi kukidhi mahitaji ya wahamiaji. Michakato yake ni tatanishi, inachukua muda mwingi na ina gharama kubwa, kwa hivyo mara nyingi wanaowasilisha maombi ni wachache. Ili kuboresha ufanisi, mashirika yanayotathmini, taasisi za kutoa leseni na zile za kitaaluma zinaweza kusawazisha mahitaji na taratibu. Serikali zinaweza kuhakikisha kwamba mashirika yanadumisha taratibu za haki, zenye uwazi na kwamba yanazingatia mbinu bora. Kuweka haki za kisheria za utambuzi pia kunaweza kuboresha kukubalika na ufanisi, kama ilivyo nchini Denmark. Sheria ya mwaka wa 2012 nchini Ujerumani inawawezesha wananchi wa kigeni kupata utambuzi bila kujali hali ya makazi au uraia.

Wahamiaji hawakubaliwi kisheria kufanya kazi zilizosimamiwa, kama vile kufundisha na uuguzi wakati kiwango chao chakuhitimu hakitambuliwi, licha ya kuwepo kwa nafasi za kazi katika nchi wanakohamia. Kutambua kwa sehemu kunaweza kusaidia. Wanaowasilisha maombi wanaweza hitajika kupita mtihani fulani, kufanya kazi chini ya usimamizi kwa muda au wasiachwe wafanya kazi fulani. Maelekezo ya Sifaza Kitaaluma ya Umoja wa Ulaya yanaruhusu makundi fulani ya wataalamu yenyekiwango cha kuhitimukilichoidhinishwa kufanya katika katika nchi za Umoja wa Ulaya. Kuanzisha na kudumisha utambuzi wa moja kwa moja unahitaji kujitolea kwa kisiasa na rasilimali, hivyo makubaliano sawa ni machache.

## UHAMIAJI WA MWALIMU HULETA FAIDA NA HATARI

Malipo duni, ukosefu wa ajira, kutokuwa na utulivu wa kisiasa, hali mbaya ya kazi na ukosefu wa miundombinu ni baadhi ya sababu zinazoweza kufanya walimu wahame. Lakini taaluma ya ufundishaji mara nyingi hufuata taratibu maalum na huwa na mahitaji maalum ya kitaifa ya kufuzu, jambo ambalo hutatiza wahamiaji.

Kwa kuwa kuwango cha kuhitimu kwa walimu sanasana kinahusiana na ujuzi wa lugha, mara nyingi uhamiaji huwa kati ya nchi zenye lugha na tamaduni zinazofanana. Walimu kutoka Misri na nchi nyingine za Kiarabu, waliovutiwa na mishahara ya juu, walisaidia kuinua mifumo ya elimu katika Baraza la Ushirikiano wa Ghuba. Sasa nchi zinatumia Kiingereza badala ya Kiarabu kama lugha ya mafundisho, na waajiri wenye ujuzi wa Kiingereza wanachukua nafasi za walimu kutoka Misri na Jordan.

Uhamiaji wa walimu unaweza kuzua msururu wa uhaba wa walimu katika nchi walikotoka. Kwa mfano, Uingereza huajiri walimu kutoka nchi kama vile Jamaica na Afrika Kusini. Kwa upande mwingine, nchi ya Afrika Kusini huajiri walimu kutoka ng'ambo hasa Zimbabwe, kwa sababu ya uhaba wa walimu. Katika miongo ya hivi karibuni, walimu wengi wamehama kutoka nchi za Karibi, hasa baada ya kupata ajira Uingereza na Marekani.

Hasara zinazopata nchi wanakotoka inaweza kuwa kubwa, kutokana na uwekezaji katika mafunzo na elimu ya walimu na kwa mfumo wa elimu kwa jumla. Wasiwasi huu umepelekea mipango ya kimataifa ambayo inatambua maslahi ya nchi wanakotoka, kama vile Makubaliano ya Kuajiri Mwalimu ya Jumuiya ya Madola (Commonwealth Teacher Recruitment Protocol). Hata hivyo, makubaliano haya si ya lazima kutii na hayawezi kuzuia walimu binafsi wanaotaka kuhama.

Uajiri wa walimu kimataifa ni biashara yenye faida inayovutia mashirika ya kibiashara. Kwa kawaida hayadhibitiwi na huenda hakadai ada ya juu ili kupata nafasi au kutotoa taarifa kamili, hivyo kuna haja ya usajili wa mashirika haya ya kuandikisha katika nchi inayopokea walimu na nchi wanakotoka.

## KUPOTEZA VIPAJI KUNAWEZA KUWA NA MADHARA MAKUBWA KWA NCHI MASIKINI


Viwango vya uhamiaji wa watu wenye ujuzi ni zaidi ya asilimia 20 katika zaidi ya robo moja ya nchi na maeneo 174, ikiwa ni pamoja na Grenada na Guyana katika Amerika ya Kusini na Karibi, Albania na Malta huko Ulaya, na Eritrea na Somalia katika mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara **(Mchoro wa 5)**.

Nchi tajiri hushindana kupata wafanyakazi wenye ujuzi, hivyo kuibua wasiwasi kuwa uhamiaji unaweza kuzuia maendeleo katika nchi wanakotoka walimu kutokana na kupoteza ujuzi. Hata hivyo, kando na athari za kupokea fedha kutoka ng'ambo, matarajio ya kutuma watu wenye ujuzi ng'ambo pia yanaweza kukuza uwekezaji kwenye elimu katika nchi zinazowatuma. Uchambuzi wa ripoti hii inaonyesha kwamba kiwango cha asilimia 14 wahamiaji wenye ujuzi wa juu huzalisha matokeo bora zaidi juu ya mkusanyiko wa mtaji wa binadamu. Baada ya kuhesabu sifa kama vile nchi za asili na nchi ya kuhamia, uhamiaji huzalisha faida ya wakazi wenye ujuzi katika nchi 90 kati ya 174.

**MCHORO WA 5:**

**Katika nchi kadhaa, zaidi ya moja kati ya watu watano wenye ujuzi huhama**

*Viwango vya wahamaji wenye ujuzi, baadhi ya nchi, 2010*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig6_1
*Chanzo:* Deuster na Docquier (2018).

Baadhi ya nchi, hasa katika Asia, zinapata raia wengi wanaorejea wakiwa na ujuzi wa thamani. Nchi ya Ufilipino imebuni sera za wanaorejea na kuwaunganisha na huduma tambuzi na wanaotazamiwa kuwa na nafasi za ajira.

## ELIMU YA KIUFUNDI NA KIUTAALAMU NI CHOMBO KWA WAHAMIAJI NA WAKIMBIZI

Masuala mawili yanaathiri mipango ya elimu ya kiufundi na kitaalamu (TVET) ya wahamiaji na wakimbizi.

Kwanza, vikwazo vingi vinapunguza haja ya wahamiaji na wakimbizi ya kuendeleza ujuzi kupitia TVET. Ukosefu wa ajira mwanzoni na ajira hatari katika kazi ambazo hawana ujuzi zinapunguza kipato cha wahamiaji ikilinganishwa na kiasi walichowekeza ili kupata ujuzi. Huenda wahamiaji wasio na hati rasmi za usajili na wanaotafuta kimbilio wasiwe na haki ya kisheria ya kufanya kazi, kama ilivyo nchini Ireland na Lithuania, hivyo kufanya wakose hamu ya kushiriki katika mafunzo ya kitaalamu. Wingi wa watoa huduma na alama za kuingia zinaweza kufanya kujiunga na TVET kuwa jambo gumu. Hata hivyo, watoa mafunzo ya TVET na huduma za ajira kwa umma wanaweza kuunganisha wahamiaji na waajiri wanaofaa ili kuwasaidia kupata uzoefu wa kazi. 'Washauri wa Kukaribisha' nchini Ujerumani husaidia makampuni madogo na ya kati katika kuajiri wafanyakazi wenye ujuzi miongoni mwa wageni; katika mwaka wa 2016, wakimbizi 3,441 walianza kupata mafunzo.

Pili, kutotambua mafunzo waliokuwa wamepata hapo awali huathiri uwezo wa wakimbizi kupata kazi nzuri au elimu na mafunzo zaidi. Ni nadra kwa wahamiaji na wakimbizi kubeba vyeti vya kuhitimu, na huenda isiwe rahisi kuhamisha digrii za TVET ikilinganishwa na digrii za vyuo vikuu kutokana na tofauti kubwa kati ya mifumo ya elimu ya kiufundi. Mnamo mwaka wa 2013, nchi ya Norway ilianzisha Utaratibu wa Kutambua Watu wasio na Hati Zinazoweza Kuthibitishwa (Recognition Procedure for Persons without Verifiable Documentation). Zaidi ya nusu ya wakimbizi ambao ujuzi wao ulitambuliwa mwaka wa 2013 ama walipata kazi inayohusiana au walijisajili kupata masomo zaidi. Utambuzi, uthibitishaji na uthibitisho rasmi zinawezekana pia serikali zikishirikiana. Kuna mikataba ya utambuzi wa kitaifa kati ya Jamhuri ya Kiarabu ya Syria na Misri, Iraq, Jordan na Lebanon.

.



Mina (miaka 11), darasa la 5, kisiwa cha Boeung Kachang, jimbo la Koh Kong, Cambodia.

KUTOKA: Shailendra Yashwant/Save the Children

# Ufuatiliaji wa hatua za Lengo la 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mfumo wa ufuatiliaji unaounga mkono Lengo la 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu elimu una maazimio makubwa sana, hata ingawa baadhi ya masuala magumu zaidi katika maendeleo ya elimu bado yametengwa. Mfumo huo una jukumu kubwa la awali linalotumika kuashiria masuala yanayostahili kushughulikia na ambayo nchi zinapaswa kuwekeza katika ufuatiliaji wake. Wakati huohuo, jitihada kubwa zinafanywa ili kubuni viashiria, viwango na zana za kuimarisha ulinganishaji wa data kati ya nchi mbalimbali. Mchakato huu unahitaji ushirikiano wa karibu kati ya mashirika ya kimataifa, nchi, wafadhili na wataalamu.

> Kufikia 2018, kutakuwa na ripoti za viashiria vingine vinne vinavyoripotiwa kwa mara ya kwanza na kufanya jumla ya viashiria vya SDG 4 vinavyopimwa kuwa 33 kati ya 43

Kuna viashiria 11 vya kimataifa vya Lengo la 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Taasisi ya Takwimu ya UNESCO (UIS) ndilo shirika la pekee linalosimamia viashiria vinane na linashirikiana na Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (ITU) kwa ajili ya kiashiria cha teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT). UNICEF ndilo shirika linalosimamia moja ya viashiria vya maendeleo ya watoto wachanga huku Shirika la Ushirikiano na Maendeleo ya Uchumi (OECD) likihusika na msaada wa masomo. Kuna viashiria vingine mahususi 32 ambavyo vinafanya mchakato wa ufuatiliaji wa Lengo la 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu kuwa na viashiria 43.

UIS huratibu mipango ya viashiria vya kimataifa na mahususi kwa ushirikiano na Mataifa Wanachama na mashirika kupitia Kikundi Shirikishi cha Kiufundi kwa ajili ya Lengo la 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu – Elimu 2030 (TCG). Kikundi hiki hufanya kazi na UNESCO. Kufikia mwaka wa 2018, viashiria vinne vitaandaliwa ripoti kwa mara ya kwanza (kushiriki katika mipango ya elimu ya kusoma na kuandika kwa watu wazima, elimu kamili ya ngono, ghasia shuleni na mashambulizi ya shule), hivyo kufanya jumla ya viashiriwa vinavyoripotiwa kuwa 33 kati ya 43. Kazi inaendelea au inakaribia kuanza katika viashiria vya lugha ya mafundisho, usambazaji wa rasilimali na ukuzaji wa taaluma ya walimu.

Muungano wa Kimataifa wa Kufuatilia Mafunzo, ambao pia umeanzishwa na UIS, huratibu kazi za viashiria vyenye matokeo tete ya kujifunza, hususan ufanisi mdogo katika kusoma na hisabati, kusoma na kuandika kwa watu wazima na ujuzi dijitali. UIS inafuatilia mikakati mitatu mbadala ili kuunganisha na kuzingatia ufanisi wa kusoma na hisabati. Kwanza, inaunga mkono mpango ambao utahakikisha kwamba wanafunzi katika mataifa yanayochaguliwa Amerika Kusini na magharibi mwa Afrika wanashiriki katika mitihani ya kanda na ya kimataifa ili kuwezesha ulinganishaji bora zaidi katika tafiti. Pili, imeainisha maudhui mbalimbali ya tathmini ambayo wataalamu watatumia kuweka viwango vya ugumu wa kila kipengele katika tafiti ili kuviweka kwenye mizani ya kuripoti. Tatu, inaendeleza jitihada za kuunganisha mizani ya ustadi kwa kutumia mbinu za takwimu.


# Tathmini ya enzi ya Elimu kwa Watu wote, 2000–2015

Ripoti ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote Duniani yamwaka 2015(EFA GMR) ilipima rekodi ya Elimu kwa Wote lakini ilitegemea kwa kiasi kikubwa data ya 2012. Tathmini iliyoboreshwa imefanywa, kulingana na data ya 2015. Haibadili hitimisho kwamba maendeleo katika enzi ya Elimu kwa Wote, ingawa ni makubwa, hayajakaribia kufikia malengo, lakini ni hatua nzuri ya kutahmini kuelekea 2030.

Matokeo mawili muhimu yanajitokeza. Kwa kuzingatia lengo la pili la Elimu kwa Wote kuhusu kukamilisha masomo ya msingi, baada ya kutobadilika kwa viwango vya kushiriki na kukamilisha masomo hayo hadi kufikia mwaka 1997, uwiano wa wanaojiunga na masomo ya msingi, kiwango cha jumla cha usajili katika darasa la kwanza na uwiano wa jumla ghafi ya wanaojisajili katika darasa la mwisho wa masomo ya msingi uliongezeka hadi mwaka wa 2008, kisha ukasimama **(Mchoro wa 6a)**. Kwa upande mwingine, kwa kuzingatia lengo la 5 kuhusu usawa wa kijinsia, ingawa lengo la usawa katika usajili kufikia 2005 halikutimizwa, hatua iliendelea katika miaka ya 1990 na 2000, na kufikia usawa mwaka 2009 katika elimu ya msingi na ya sekondari na kukaribia usawa katika ujuzi wa kusoma na kuandika kwa vijana mwaka 2015. Ukosefu wa usawa katika kusoma na kuandika bado upo miongoni mwa watu wazima, huku asilimia 63 kati ya wasiojua kusoma wala kuandika wakiwa wanawake, hali imegeuka katika elimu ya juu ambapo wanaume sasa wana nafasi ndogo ya kushiriki **(Mchoro wa 6b)**.

**MCHORO WA 6:**

**Kati ya 2000 na 2015, ulimwengu uliendelea kwa kasi kuelekea usawa wa kijinsia lakini sio katika kukamilisha elimu ya msingi**




*GEM StatLink*: http://bit.ly/fig7_1
*Chanzo*: hifadhidata ya UIS.

# Ufuatiliaji wa hali ya elimu ya wahamiaji na waliofurushwa makwao una changamoto nyingi

Mpango wa ufuatiliaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu unazingatia kwa umahususi zaidi kuainisha viashiria kwa sifa mbalimbali zinazohusishwa na athari hasi. Hata hivyo, data iliyoratibishwa ya hali ya elimu kwa wahamiaji na wakimbizi ni mbaya. Katika Dibaji ya Data ya Benki ya Dunia, zaidi ya kaya 2,000 kati ya 2,500 zilizoshiriki utafiti zinajumuisha taarifa kuhusu elimu, lakini takribani moja juu ya saba kati ya hizo inahusu uhamiaji, sehemu ndogo zaidi inahusu taarifa za walio furushwa makwao.

> "Familia za wahamiaji huhamahama sana na huwa na uwezekano mdogo wa kuwa nyumbani wakati wa ziara za wanaokusanya taarifa. Pia huenda wasihojiwe kwa sababu ya vikwazo vya lugha au wasiwasi wa kisheria"

Familia za wahamiaji huhamahama sana na huwa na uwezekano mdogo wa kuwa nyumbani wakati wa ziara za wanaokusanya taarifa. Pia huenda wasihojiwe kwa sababu ya vikwazo vya lugha au wasiwasi wa kisheria. Na kwa kuwa mtiririko wa wahamiaji unaweza kubadilisha haraka, huenda ikawa vigumu kwa idadi ya watafitiwa kuwiana na mabadiliko. Hali hii hasa huathiri watu waliokimbia makwao: yamkini data hukusanywa kwa uratibu zaidi katika kambi za wakimbizi, lakini chini ya asilimia 40 ya wakimbizi na kiwango kidogo zaidi cha waliofurushwa makwao huishi katika kambi.

Kuhakikishia kujumuishwa kwa wahamiaji na wakimbizi katika tafiti za kawaida, za jumla kwa kawaida hakuwezi kutatua suala la sampuli na kukusanya data. Utafiti wa kawaida huwa hautambui mabadiliko yanayotokea katika uhamiaji na pia unaweza kuwa haufanywi mara kwa mara ili kuweza kuzalisha taarifa kwa wakati. Mbinu nyumbufu, ikiwa ni pamoja na tafiti zinazozingatia uchunguzi unaohusisha kutuma na kupokea jamii, pamoja na kukusanya data kwa haraka kwa kutumia sampuli ya kinasibu, inaweza kuwa na ufanisi zaidi. Hatimaye, utafiti huenda usiweze kunakili mabadiliko ya mienendo ya uhamiaji na elimu au viwango vya kuhitimu vya nchi za asili.

Mnamo Machi 2016, Tume ya Takwimu katika Umoja wa Mataifa ilianza kuwa mwenyeji wa Kikundi cha Wataalamu wa Takimwimu kuhusu Wakimbizi na Waliofurushwa Makwao. Kikundi hicho kinachojumuisha nchi 40 wanachama na angalau mashirika 15 ya kikanda na kimataifa, kimetoa mapendekezo kuhusu kuboresha ukusanyaji wa data. UNESCO na UNHCR zinaandaa Mfumo wa Habari wa Usimamizi wa Elimu ya Wakimbizi, ambao ni mfumo huria mtandaoni unaopatikana bila malipo ili kusaidia nchi kukusanya, kuratibu, kuchambua na kutoa ripoti ya data ya elimu ya wakimbizi.




LENGO 4.1

# Elimu ya msingi na sekondari

Watoto waliozaliwa kati ya 2010 na 2014 wanaweza kuchukuliwa kuwa kizazi cha Malengo ya Maendeleo Endelevu. Aliye mkubwa zaidi alifika umri wa miaka 5 mwaka 2015 na katika nchi nyingi, wanatarajiwa kuwa katika elimu ya chekechea kufikia mwaka 2015/16, ambao ndio mwanzo wa kipindi cha Malengo ya Maendeleo Endelevu (2015-2030). Aliye mdogo kabisa atatimiza miaka 16 mnamo 2030, ambao unaweza kuwa umri mchanga zaidi wa kukamilisha elimu ya kawaida ya sekondari. Ili kizazi cha Malengo ya Maendeleo Endelevu kitimize lengo la kukamilisha masomo ya sekondari kwa wote kufikia 2030, kikundi cha sasa kinatakiwa kuanza masomo ya shule ya msingi kwa wakati. Kiwango cha kimataifa cha usajili uliorekebishwa kwa jumla wa kujiunga na darasa la kwanza la masomo ya msingi kilikuwa asilimia 86 mwaka wa 2017.


> “Ili kukamilisha masomo ya sekondari kufikia 2030, watoto wote wanastahili kujiunga na shule za msingi kufikia mwaka wa 2018”

Watoto milioni 64 walio katika umri wa kwenda shule ya msingi, au asilimia 9, hawakuwa shuleni mwaka 2017, hali ilikuwa sawa na hiyo miongoni mwa vijana wenye umri wa kupata elimu ya kawaida ya sekondari ikiwa milioni 61 yaani (asilimia 16) na vijana 138,000 wenye umri wa kuendelea na masomo ya sekondari (asilimia 36). Kiwango cha msingi ni kama hakijabadilika tangu 2008. Mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara yanachangia ukuaji huu, isipokuwa kwa umri wa kwenda shule ya msingi; migogoro imesababisha watoto kuondolewa shuleni katika baadhi ya maeneo, hasa Asia Magharibi **(Mchoro wa 7)**.

**MCHORO WA 7:**

**Mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara yanachangia idadi inayokua ya watoto wasio shuleni**

*Usambaaji wa wasio shuleni kulingana na kanda, 2000–2015*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig8_2
*Chanzo:* hifadhidata ya UIS.

Utafiti wa Maendeleo ya Kimataifa katika Kusoma, ambao ni utafiti unaowatathmini wanafunzi wa darasa la 4 kila baada ya miaka mitano, hutoa data mpya ya utafiti wa kimataifa kwa kiashiria cha matokeo ya kujifunza. Katika Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, asilimia ya kiwango cha kutimiza lengo la chini iliongezeka kutoka asilimia 56 mwaka 2001 hadi asilimia 65 mwaka 2016, yaani ukuaji wa chini ya asilimia moja kwa mwaka. Nchi zingine, ikiwa ni pamoja na Morocco na Oman, zimeongeza kiwango cha kufikia lengo kufikia 2030; kwa nchi zingine, kwa mfano Azerbaijan, Saudi Arabia na Afrika Kusini, idadi ya wanafunzi wanaotimiza kiwango cha chini cha ustadi haikuongezeka na hivyo kuashiria ugumu katika kufikia lengo hilo.

## KADIRIO JIPYA LA KIWANGO CHA KUKAMILISHA MASOMO KWA AJILI YA AJENDA YA ELIMU 2030

Kulingana na takwimu za uchunguzi katika kaya kwa miaka ya 2013–2017, viwango vya kukamilisha elimu vilikuwa asilimia 85 kwa msingi, asilimia 73 kwa sekondari ya kawaida na asilimia 49 kwa elimu ya vidato vya juu vya elimu ya sekondari. Hata hivyo, kuna kupishana kwa muda kati ya uchunguzi wa kaya na data ya sensa, kwa hivyo vyanzo mbalimbali vinaweza kutoa taarifa zinazokinzana.

Kwa kufuata mfano wa jumuiya ya ufuatiliaji wa afya, timu ya Ripoti ya GEM imeunda mfumo wa kukadiria viwango vya kukamilisha elimu. Kuangazia viwango vya kukamilisha elimu kwa vijana wa muda uliopita kunaweza kutoa mtazamo wa muda mrefu wa kiwango cha upanuzi kwa nchi fulani. Ngazi ya sasa ya kiashiria inaweza kukadiriwa kwa ujumuishaji wa muda mfupi kutokana na data ya hivi majuzi. Mtindo huu unapatanisha ruwaza na mwelekeo wa jumla katika vyanzo vyote vya data badala ya kuchukua makadirio ya hivi majuzi kwa namna yanavyoonekana.




LENGO LA 4.2

# Elimu ya chekechea

Elimu na utunzaji wa watoto wachanga ni muhimu kwa ukuaji wa utambuzi na wa kijamii na huwa na jukumu muhimu la ulinzi katika matukio ya migogoro.


Kiashiria cha kimataifa kuhusu ushiriki katika mafunzo kwa namna iliyopangika kwa mwaka mmoja kabla ya umri wa kujiunga na masomo ya msingini takribani asilimia 42 katika nchi zenye kipato ya chini na hadi asilimia 93 katika nchi za kipato cha juu. Wastani wa dunia ni asilimia 69 na inaendelea kuongezeka japo polepole. Kwa kulinganisha, kiwango cha awali cha kujiandikisha katika masomo ya chekechea, yaani kiwango cha elimu kinachodumu kwa mwaka mmoja katika baadhi ya nchi na miaka minnne kwa nyingine, kilifikia asilimia 50 mwaka 2017 **(Mchoro wa 8)**.

Kiashiria kingine cha maendeleo ya ustawi wa utotoni unatokana na Kielelezo cha Ustawi wa Utotoni (ECDI), ambao aghalabu huhesabiwa kwa kutumia data ya Uchunguzi Jumuishi wa Viashiria wa UNICEF (MICS), ingawa UNICEF inakagua mbinu za ECDI ili kutatua mapungufu. Mchakato huo unatarajiwa utamalizika mwishoni mwa 2018. Matokeo kutoka nchi zinazoshiriki katika mizunguko miwili ya MICS katika miaka mitano inaonyesha kwambaidadi ya watoto walio na umri wa miaka 3 hadi 4 wanaopata ujuzi wa kusoma na kuhesabu imeongezeka kwa chini ya asilimia moja kwa mwaka kwa wastani.

**MCHORO WA 8:**

**Watoto saba kati ya kumi huhudhuria masomo ya chekechea kabla ya kuanza elimu ya msingi**

*Kiwango cha ushiriki katika mfumo uliopangiliwa wa elimu mwaka mmoja kabla ya umri rasmi wa kuanza masomo ya msingi, uwiano wa jumla ya kujiunga, 2000–2016*





*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig9_2
*Chanzo:* hifadhidata ya UIS.

Hata hivyo, kuwa 'tayari' kwenda shule na 'kuendelea kukomaa kama inavyotarajiwa' ni dhana tete, zinazochukuliwa kwa utofauti kote duniani. Nchi huenda zikazingatia tahadhari zaidi wakati wa kutumia vipimo vinavyotimiza mahitaji yao na vinavyoambatana na miundo ya taasisi na sifa za kitamaduni.

Hata hivyo mifumo ya kitaifa ya kufuatilia utayari wa kwenda shuleni ni nadra. Kwa kawaida, nchi huwa na mifumo na taratibu za kitaifa za ufuatiliaji wa wafanyakazi, mafunzo, vifaa na viwango vya shule kati ya watoa huduma (kwa mfano, Sera ya Huduma ya Elimu ya Chekechea nchini India ya 2013) au kutathmini matokeo ya mpango (kwa mfano, kipengele cha Mfumo wa Taifa wa Kuripoti nchini Marekani chini ya mpango wa Elimu ya chekechea). Katika moduli ya ustawi wa watoto ya Mfumo wa Maendeleo ya Benki ya Dunia kwa Matokeo ya Elimu Bora, nchi 8 tu kati ya 34 za kipato cha chini na za kati zilikusanya data kuhusu watoto katika nyanja zote nne zilizotajwa (ukuaji wa ufahamu, lugha, kimwili na kijamii).

Mpango wa Kitaifa wa Mtalaa wa Afrika Kusini wa 2014 unazingatia tathmini isiyo rasmi, kuangalia na utahini endelevu katika vipengele sita vya Elimu ya Chekechea, bila kuashiria alama au asilimia lakini kunakili utayari wa kujiunga na daraja la kwanza la masomo ya msingi. Tangu 2014, Jamhuri ya zamani ya Yugoslavia ya Masedonia imenakili wasifu wa maendeleo ya watoto wote waliojiunga na vituo vya chekechea.





LENGO LA 4.3

# Elimu ya ufundi, utaalamu, ya juu na ya watu wazima

Kiashiria cha kimataifa kuhusu kushiriki katika elimu ya watu wazima kimeimarishwa ili kujumuisha fursa zote za elimu ya darasani na ya nje ya darasa, iwe inahusiana na kazi au la. Uanuwai na idadi ya watoaji hufanyauchunguzi wa nguvukazi kuwa chanzo bora ikilinganishwa na data ya usimamizi, lakini maswali katika tafiti hizi hutofautiana sana kati ya nchi, pia maswali machache yanaambatana na ufafanuzi mpya ulio kwenye kiashiria. Kusanifu maswali ili kupanua idadi ya nchi zenye data inayofanana hakutakuwa rahisi.

Utafiti wa Nguvukazi katika Umoja wa Ulaya huzingatia elimu rasmi na mafunzo katika wiki 4 zilizopita (ikilinganishwa na takwa la miezi 12 katika kiashiria). Viwango vya ushiriki vipo imara, kwa wastani ni asilimia 11, ingawa mienendo inatofautiana kati ya nchi (Mchoro wa 9). Uchunguzi Jumuishi wa Soko la Ajira nchini Misri, Jordan na Tunisia unawahusisha tu watu walioajiriwa, wenye ushiriki wa maisha na mafunzo ya Ufundi yanayohusiana na kazi. Uchunguzi huo unaashiria viwango vya ushiriki wa kila mwaka wa asilimia 4 kati ya wafanyakazi wenye ujuzi wa kiufundi.

**MCHORO WA 9:**
**Kushiriki katika elimu ya watu wazima katika mataifa ya Ulaya kumebakia imara, lakini mienendo hutofautiana kati ya nchi**
*Kiwango cha ushiriki wa watu wazima katika elimu na mafunzo katika wiki nne zilizopita katika Umoja wa Ulaya na nchi zilizochaguliwa, 2008–2017*





*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig10_1
*Chanzo:* Eurostat (2018).

> Uchunguzi wa nguvukazi ni chanzo bora cha data ya usimamizi ya kupima elimu ya watu wazima kutokana na uanuwai na idadi ya watoaji huduma

Uwiano wa jumla wa kujiandikishaji ulifikia asilimia 38 mwaka 2017, lakini kiwango cha matumizi binafsi kwa gharama ya elimu ya juu kinaongezeka. Msaada wa kifedha katika mikopo ya wanafunzi, ufadhili, ruzuku na udhamini wa masomo una maana kwamba elimu ya juu ni nafuu zaidi Ulaya na ina gharama ya juu katika Mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambako unagharimu zaidi ya asilimia 60 ya wastani wa pato la taifa katika nchi nyingi na kufikia karibu asilimia 300 nchini Guinea na Uganda.

Mifumo mingi ya elimu hulenga msaada mahususi wa kifedha, lakini ufanisi wa umahususi hutofautiana sana. Takwimu za Benki ya Dunia zinaonyesha kwamba, katika nchi kadhaa za kipato cha chini nacha kati, kaya zilizo katika humusi maskini zaidi zilikuwa na uwezekano mdogo wa kupata udhamini wa serikali zikilinganishwa na walio katika humusi ya matajiri zaidi. Mkusanyiko wa sera kadhaa ikiwa ni pamoja na mbinu mbalimbali, kama ilivyo Kolombia na Viet Nam, unaweza kuwa na mafanikio zaidi kuliko udhamini wa masomo pekee.




LENGO 4.4

# Ujuzi kwa ajili ya kazi

Viashiria vya kimataifa na vya kisekta kuhusu TEHAMA na ujuzi dijitali vina lenga kunakili zaidi ya ujuzi wa kusoma na kuhesabu ambao unakaribia kuwa muhimu sana katika ulimwengu wa kazi. Viashiria hivi vinahitaji serikali zizingatie upataji wa ujuzi nje ya shule.


Kiashiria cha kimataifa kuhusu vijana na watu wazima walio na ujuzi wa TEHAMA hutokana na uchunguzi unaotokana na majibu ya kaya kuhusu shughuli mahususi katika miezi mitatu iliyotangulia. Takwimu za hivi karibuni za ITU zinaonyesha kwamba kunakili na kuambatisha faili kwenye barua pepe ndio ujuzi wa pekee ambao mtu moja kati ya watatu waliohojiwa wanaofanya kazi katika nchi za kipato cha kati wanazo kwa kawaida; viwango linganishi vilikuwa kati ya asilimia 58 na 70 katika mataifa yenye kipato

> Mtu mmoja kati ya kumi katika nchi za kipato cha juu hawezi kuambatisha faili kwenye barua pepe

**MCHORO WA 10:**

**Usambaaji wa ujuzi wa TEHAMA bado hauna usawa**

*Asilimia ya watu wazima waliofanya shughuli zinazohusiana na kompyuta katika miezi mitatu iliyopita, kulingana na kundi la kipato cha nchi, 2014–2017*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig11_1
*Kumbuka:* Wastani katika nchi za kipato cha kati unategemea idadi ndogo ya nchi (nchi 5 za chini miongoni mwa za kipato cha kati, nchi 15 za juu miongoni mwa za kipato cha kati).
*Chanzo:* hifadhidata ya ITU.

cha juu (**Mchoro wa 10**). Usanidi bado ni kazi ya watu wachache hata katika nchi zenye kipato cha juu.

Kiashiria mahususi wa ujuzi dijitali ni zaidi ya uwezo wa kutumia vifaa vya TEHAMA. Mfumo mpya wa kimataifa wa ufahamu dijitali unapanua mfumo wa DigComp wa Tume ya Ulaya ili kujumuisha mifumo ya matumizi mapana, changamano inayoashiria matumizi ya mifano ya kitamaduni, kiuchumi na teknolojia ya nchi za kipato cha chini na za kati, kwa mfano ujuzi ambao wakulima wanahitaji kufanya maamuzi ya kilimo na biashara kwa kutumia huduma ya simu ya mkononi, kununua na kuuza bidhaa kupitia programu za simu mahiri au kuunda mfumo wa umwagiliaji unaotokana na data kwa kutumia vitambuzi vya unyevu vilivyounganishwa na kompyuta ya kupakata.

Kutambua mbinu nafuu za kupima uwezo huu bado ni changamoto kubwa. Tathmini za ufahamu dijitali hutofautiana kulingana na lengo, kundi linalolengwa, vitu, uwasilishaji, gharama na mamlaka husika. Mfano wa Ufaransa unaowawezesha raia kupata tathmini ya ujuzi wa digitali bila malipo, ugunduzi wa uwezo na udhaifu na mapendekezo ya nyenzo za kujifunza unaweza kuwa njia ya kupiga hatua.

Kutathmini ustadi wa wajasiriamali ni dhamira ya lengo la 4.4 ambalo bado halina kiashiria, nalo pia linakabiliwa na changamoto sawa na hizo. Ujuzi wa kijamii na kimawazo, ukiwa ni pamoja na uvumilivu na kujidhibiti, ni miongoni mwa ujuzi mbalimbali wa ujasiriamali, lakini kuupima kunahitaji tahadhari katika kufasiri tofauti kati ya tamaduni mbalimbali. OECD inatayarisha Utafiti wa Kimataifa wa Ujuzi wa Kijamii na Kimawazo kati ya watoto wa miaka 10 na 15.




**LENGO LA 4.5**


# Usawa

Kwa wastani, kuna usawa wa kijinsia kimataifa katika kujiandikisha katika elimu ya msingi na ya sekondari. Hata hivyo, wastani huu unaficha kutofautiana kunakoendelea katika ngazi ya nchi binafsi. Mnamo 2016, asilimia 54 ya nchi zilifikia usawa katika kujisajili kwenye elimu ya sekondari ya chini na asilimia 22 katika vidato vya juu vya

**MCHORO WA 11:**

**Nchi nyingi bado hazijafikia usawa wa kimaeneo na utajiri katika idadi ya wanaokamilisha shule, hasa katika elimu ya sekondari**

*Takwimu za jinsia, eneo na utajiri zikiwa zimeratibiwa kulingana na kiwango cha kukamilisha daraja za elimu, 2014–2017*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig12_1
*Vyanzo:* Mahesabu ya timu ya UIS na GEM kutumia tafiti za kaya.

sekondari. Aidha, sio nchi zote zinazofikia usawa zinaweza kuudumisha.

> “Wanafunzi wa vijijini huwa takribani nusu ya nafasi waliyo nayo wenzao wa miji kukamilisha elimu ya vidato vya juu vya sekondari katika nchi za kipato cha chini na za kati”

Utofauti mkubwa upo katika viwango vya kukamilika kwa eneo na utajiri. Wanafunzi wa vijijini huwa takribani nusu ya nafasi waliyo nayo wenzao wa miji kukamilisha elimu ya vidato vya juu vya sekondari katika nchi za kipato cha chini na za kati **(Mchoro wa 11)**.

Ulinganifu mdogo huzuia kiwango cha kupima kutofautiana kimaeneo: sehemu ya nguvukazi inayohusika katika kilimo, ukubwa wa idadi ya watu, uwiani wa idadi ya watu, vigezo vya upekee wa kitaifa au mchanganyiko wake unaweza kubainisha ‘maeneo ya miji’ na ‘vijijini’ katika nchi.

Kwa kuunga mkono ufuatiliaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, kufuatia mkutano wa 2016 wa Shirika la Makao la Umoja wa Mataifa uliofanyika Quito, fasili ya kimataifa kuhusu miji na makazi inayozingatia watu inaandaliwa ili kuidhinishwa mwaka 2019. Inalinganisha uainishaji wa kiutawala na data inayokusanywa kutoka mbali na maelezo ya sensa. Cha ajabu ni kwamba, ingawa fasili za kitaifa zinaonyesha kuwa chini ya nusu ya wakazi wa Afrika na Asia huishi katika miji, makadirio ya 2018 yanaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 80 wanaishi mijini. Makadirio ya sasa ya matokeo ya elimu vijijini yanaweza kujumuisha maeneo mengi ambayo kwa hakika ni miji na hivyo kuficha hali ya maeneo yaliyo vijijini kikweli.




LENGO 4.6

# Kuandika na kuhesabu


Kiwango cha watu wanaojua kuandika na kusoma duniani kilifikia asilimia 86 mwaka 2017, ingawa bado ni chini ya asilimia 65 katika mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara. Maendeleo katika uwezo wa kujua kusoma na kuandika miongoni mwa vijana – na kupungua kwake miongoni mwa vijana – yamekuwa ya haraka katika miaka ya hivi karibuni na kusababisha kushuka kabisa kwa jumla ya idadi ya vijana wasiojua kusoma wala kuandika walio na umri wa miaka 15 hadi 24, kwa kiasi kikubwa Asia inaongoza. Lakini idadi ya wazee wasiojua kusoma na kuandika, wenye umri wa miaka 65 na zaidi, inaendelea kukua; sasa kuna karibu zaidi ya asilimia 40 wasiojua kusoma na kuandika ukilingansiha na vijana wasiojua kusoma na kuandika **(Mchoro wa 12)**.

Watu wasiojua kusoma na kuandika wanaoishi katika kaya ambapo hakuna mtu anayejua kusoma, huwa na wakati mgumu katika soko la ajira na ubora wa

**MCHORO WA 12:**

**Kuna karibu zaidi ya asilimia 40 ya wazee wasiojua kusoma na kuandika ukilingansha na vijana**

*Idadi ya vijana na wazee wasiojua kusoma na kuandika, 2010–2016*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig13_1
*Chanzo:* hifadhidata ya UIS.

maisha kuliko watu wengine wasiojua kusoma na kuandika, wanaoishi na ndugu moja au zaidi anayejua kusoma na kuandika.

Matukio ya watu wasiojua kusoma na kuandika wanaoishi peke yao hutokea sana miongoni mwa wakazi wa vijijini. Katika nchi tajiri, watu wasiojua kusoma na kuandika wanaoishi peke yao ni wazee kuliko wasiojua kusoma an kuandika wanaoshi na wanaojua kusoma na kuandika.Hali hii ni tofauti katika mataifa maskini. Moja ya sababu ni kwamba watu wengi wasiojua kusoma na kuandika katika nchi masikini wanaishi katika kaya za watu wa rika mbalimbali na hivyo kuna uwezekano wa kuishi pamoja na vijana na ndugu wengine wenye elimu zaidi.

Kwa hivyo, hatua za kutatua tatizo la kutojua kusoma na kuandika zinafaa kuzingatia watu wazima wanaoishi katika kaya za mtu moja au wawili katika mataifa tajiri na vijana waliotengwa kijamii na kiuchumi, ambao kwa kawaida wanaishi vijijini, katika nchi maskini.




LENGO 4.7


# Maendeleo endelevu na uraia wa kimataifa

Taarifa kuhusu kiashiria cha kimataifa inayozingatia nchi 83 zilizoshiriki katika mashauriano ya sita kuhusu utekelezaji wa Mapendekezo ya UNESCO ya mwaka wa 1974 kuhusu Elimu ya Uelewa wa Kimataifa, Ushirikiano na Elimu ya Amani zinazohusiana na Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi. Zaidi ya asilimia 80 ya nchi zimeripoti kujumuisha kanuni za mapendekezo hayo katika mitihani ya wanafunzi. Takriban nchi zote zimeripoti kuwa zimejumuisha kanuni hizo katika mitalaa. Hata hivyo, asilimia 17 tu ya nchi zimeweka kanuni hizo kikamilifu katika

**MCHORO WA 13:**

**Asilimia 17 ya nchi pekee ndizo zimejumuisha kanuni za haki za binadamu na uhuru wa msingi kikamilifu katika elimu ya walimu wanaofanya kazi**

*Asilimia ya nchi zinazozingatia kanuni za Mapendekezo ya UNESCO ya mwaka wa 1974 katika sera zao za elimu, elimu kwa walimu na mitalaa, 2012–2016*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig14_1
*Chanzo:* UNESCO (2018).

mtalaa wa elimu ya mwalimu **(Mchoro wa 13)**.

Utafiti wa Kimataifa wa Ustawi na Uraia uliofanywa na IEA 2016 ulichanganua ujuzi, ufahamu, mtazamo, maoni na shughuli za wanafunzi wa darasa la 8 katika nchi 24 za kipato cha juu. Asilimia 35 ya wanafunzi walio katika ngazi nne za juu kabisa, walidhihirisha uwezo wa kuona uhusiano kati ya michakato ya mashirika ya jamii na siasa na taratibu za kisheria na taasisi zinazozidhibiti, huku asilimia 13 wakipata alama za chini au chini kabisa.

Nchi kumi na moja zilikuwa zimeboresha kwa kiasi kikubwa matokeo kati ya mzunguko wa uchunguzi wa 2009 na 2016,na hakuna iliyokuwa na kupungua kwa kiasi kikubwa. Kibali cha washiriki kuhusu haki sawa na mitazamo mizuri kwa makundi ya kikabila au watu wa rangi tofauti pia umeboreka. Wanawake na wanafunzi wanaojali sana mambo ya kiraia na kisiasa na wale walio na kiwango cha juu cha ufahamu wa kiraia walikuwa na mitazamo mizuri zaidi. Vigezo binafsi vinavyohusishwa sana na mielekeo chanya vinahusiana na mitazamo ya ubora wa michakato ya shule, kama vile uhusiano wa wanafunzi na walimu, kujifunza masuala ya kiraia na uwazi katika shule na majadiliano ya darasani.




LENGO 4.A

# Nyenzo za Elimu na mazingira ya kujifunza

Kote duniani, asilimia 69 ya shule zina maji ya kunywa, asilimia 66 zina misala na asilimia 53 zikiwa na usafi wa ngazi ya huduma ya msingi au bora **(Mchoro wa 14).** Nchini Jordan, asilimia 93 ya shule zina maji ya kunywa ya msingi, lakini asilimia 33 ndizo zina misala ya msingi. Nchini Lebanon, karibu asilimia 93 ina maeneo ya usafi wa msingi, huku asilimia 60 ikiwa na maji ya kunywa ya msingi. Aghalabu shule za msingi huwa na ubora wa chini wa huduma zililinganishwa na shule za sekondari.


Vipengele vichache vya usalama na ujumuishaji katika mazingira ya kujifunza vinafuatiliwa kikamilifu duniani kote. Dhana kama vile unyanyasaji kwa kawaida hazina ufafanuzi wa kimataifa na uchunguzi wazo hutofautiana sana. Utafiti mmoja unakadiria kwamba karibu asilimia 40 ya wavulana na asilimia 35 ya wasichana wenye umri wa miaka 11 hadi 15 wameripotiwa kuwa waathirika wa unyanyasaji. Idadi ya nchi zilizopiga marufuku adhabu ya viboko shuleni imeongezeka kufikia 131, kutoka 122 mwishoni mwa mwaka wa 2014.

Kati ya 2013 na 2017, kulikuwa na zaidi ya mashambulizi 12,700 dhidi ya elimu, ambayo yaliathiri zaidi ya wanafunzi na waelimishaji 21,000, kulingana na Vuguvugu la Kimataifa la Kulinda Elimu dhidi ya Mashambulizi. Matukio yaliyoripotiwa yalijumuisha mashambulizi ya kimwili au vitisho vya mashambulizi kwa shule, wanafunzi na wafanyakazi wa elimu; matumizi ya majengo ya kielimu kwa madhumuni ya kijeshi; kuajiri watoto au unyanyasaji wa

**MCHORO WA 14:**

**Chini ya shule 7 kati ya 10 zina maji ya kunywa ya kiwango cha huduma ya msingi**

*Usambazaji wa maji ya kunywa, misala na usafi katika shule kwa kiwango cha huduma, 2016*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig15_1
*Chanzo:* UNICEF na Shirika la Afya Duniani (2018).

> Kati ya 2013 na 2017, kulikuwa na zaidi ya mashambulizi 12,700 dhidi ya elimu

kimapenzi wakati wa kwenda au kwenye shule au vyuo vikuu na watu wenye silaha; mbali na mashambulizi katika taasisi za elimu ya juu. Nchi ishirini na nane zilikumbwa na angalau mashambulizi 20; Nigeria, Ufilipino na Yemen zilikuwa miongoni mwa nchi zilizoshambuliwa zaidi ya mara 1,000.

Takwimu za vuguvugu hili hazionyeshi mashambulizi fulani, ikiwa ni pamoja na yaliyotendwa na makundi ya uhalifu na kushambuliwa kwa shule na mtu mmoja mwenye bunduki. Nchini Marekani, angalau wanafunzi 187,000 katika shule 193 wamekumbwa na matukio ya mashambulizi ya risasi shuleni tangu mwaka wa 1999.




LENGO 4.B

# Udhamini wa elimu


Kiasi cha udhamini unaofadhiliwa na mipango ya misaada hakijaongezeka tangu mwaka 2010 na kimesalia kuwa kati ya dola bilioni 1.1 na dola bilioni 1.2 za Marekani (bila gharama za mwanafunzi). Hata hivyo, kiashiria hiki hakitoi taarifa kuhusu idadi ya wapokeaji wa udhamini au idadi ya waliopokea udhamini nje ya mipango ya misaada.

Ingawa idadi kubwa ya wanafunzi wanaosafiri kimataifa hutoka nje ya kanda zao, wanafunzi wengi wanaosafiri kimataifa kutoka Ulaya hubaki nadani ya jumuiya yao, uhamiaji wao unawezeshwa kupitia mipango ya kubadilishana wanafunzi. Kiwango cha kwenda ng'ambo huongezeka kwa kiwango cha elimu, kutoka asilimia 3 kwa shahada ya kwanza hadi asilimia 6 kwa ajili ya uzamifu na asilimia 10 uzamili **(Mchoro wa 15**).

**MCHORO WA 15:**

**Barani Ulaya, uhamaji wa wanafunzi huongezeka kulingana na daraja la masomo**

*Kiwango cha kutoka nje ya nchi kwa mujibu wa Uainishaji wa Kimataifa wa Ngazi ya Elimu, nchi zilizochaguliwa Ulaya, 2013*





*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig16_3
*Chanzo:* Flisi et al. (2015).

Mtazamo wa Uhamiaji wa Kielimu katika Umoja wa Ulaya kufikia 2020 unaashiria kuwa angalau asilimia 20 ya wahitimu wa elimu ya juu katika Umoja wa Ulaya watakuwa wamepokea mafunzo nje ya nchi kwa angalau miezi 3 au usawa na vipimo 15 katika Mfumo wa Uhamisho wa Vipimo wa Ulaya.

> “Mkakati wa Elimu ya Juu wa Umoja wa Ulaya unalenga kuhakikisha kuwa angalau asilimia 20 ya wahitimu wa elimu ya juu watakuwa wamepokea sehemu ya masomo yao ng’ambo”

Taasisi za taifa zinaweza kutoa data ya kukadiria uhamashaji waalama kwa muda; Nchi zinazopokea wanafunzi zinafaa kutoa data kuhusu wanaosafiri kwa ajili ya kupata shahada. Kwa mataifa ya Umoja wa Ulaya, ni lazima kuripoti, lakini kati ya nchi ambapo idadi kubwa ya wanafunzi huenda nje ya Ulaya, ni Australia, Brazil, Kanada, Chile, Israeli na New Zealand pekee ambazo hutoa data muhimu. Marekani ni chanzo kikuu kisichotoa data, pamoja na Uchina, India, Japan, Mexico na Jamhuri ya Korea. Kutokana na kutokamilika kwa taarifa, makadirio yaliyopo (sasa ni chini ya asilimia 20) huenda hayaoneshi taswira kamili ya wanaotoka nje ya mataifa yao kutafuta elimu.




LENGO 4.C

# Walimu

Kukusanya takwimu za kimataifa za kulinganisha viashiria vinavyowahusu walimu bado ni changamoto. Kwa kiasi kikubwa nchi chache zinazalisha data inayoweza kulinganishwa, hasa kwa elimu ya sekondari, hata kwa kuzingati ufafanuzi wa msingi zaidi wa idadi ya walimu, unaopuuza idadi ya saa za kufundisha na idadi ya walimu walio katika nafasi za usimamizi.

Nchi zenye kipato cha chini na za chini miongoni mwa zile zenye kipato cha kati zinaendelea kukumbwa na uhaba mkubwa wa walimu walio na ujuzi wa kufundisha shule za msingi. Baadhi ya mataifaya Kusini mwa Jangwa la Sahara yana viwango vya juu vya kuajiri, vinavyoweza kuathiri viwango vya wanaoingia ikiwa uwezo wa elimu ya mwalimu ni mdogo. Nchini Niger, ambako asilimia 13 ya walimu walikuwa wameajiriwa mwaka 2013, ni asilimia 37 pekee waliokuwa wamepokea mafunzo **(Mchoro wa 16)**.


Viwango vya juu vya kuajiri sio tu ishara ya upanuzi wa elimu; uajiri unaweza kuwa muhimu ili kuchukua nafasi ya wanaoondoka. Takwimu za kuaminika kuhusu wanaoacha taaluma ya ualimu ni chachena ni ngumu kufasiri. Makadirio sahihi yanahitaji data ya wafanyakazi inayowapa nambari ya utambulisho, ili iwe rahisi kufuatilia wanapofuzu, kuingia katika taaluma, kuondoka na kurejea tena. Takwimu zinapaswa kutofautisha miongoni mwa wanaofuatiliwa na iweze kubainisha wanaojiunga na wanaoondoka, ikiwa ni pamoja na wanaorejea tena kwenye taaluma. Utaratibu wa kufuatilia wanaondoka kwenye taaluma unahitaji mfumo wa kitaifa nataarifa kuhusu aina zote za shule katika mifumo iliyo na utofautishaji, lakini mara nyingi habari zinazopatikana ni za eneo mahususi tu (kwa mfano Brazil) au zinajumuisha shule za umma (kwa mfano Uganda).

Utafiti kutoka nchini Chile, Uswidina Marekani ulipata kwamba kiwango cha kuondoka kwenye taaluma kipo juu sana miongoni mwa walimu ambao hawakuwa wamedumu zaidi, wenye ujuzi zaidi (kwa hiyo wanaweza kuajiriwa kwa urahisi kwingine), waliokuwa wakifundisha katika shule zenye changamoto au za vijijini, walio na malipo duni au mikataba ya muda mfupi. Hata hivyo, ushahidi kutokana na uchunguzi wa muda mrefu nchini Australia ulionesha kwamba walimu wengi walioacha kazi walifanya hivyo kwa sababu za familia na kurudi kwenye taaluma ndani ya miaka miwili.

**MCHORO WA 16:**

**Ni vigumu kudumisha viwango vya elimu kwa walimu ikiwa kuna viwango vya juu vya kuajiri**

*Kiwango cha uajiri mpya wa walimu na asilimia ya walimu waliopokea mafunzo, kwa shule za msingi, Mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara yaliyochaguliwa, 2010–2014*




*GEM StatLink*: http://bit.ly/fig17_1
*Chanzo*: hifadhidata ya UIS.

# Elimu na malengo mengine ya Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ripoti hii inachunguza jinsi elimu inavyoweza kuharakisha mafanikio ya Malengo mengine ya Maendeleo Endelevu yanayohusiana na kupata kazi nzuri, miji endelevu na haki kwa njia tofauti, ikiwa ni pamoja na kupitia uwezo wa kitaaluma.

Nchi nyingi zina wafanyakazi wachache wenye ujuzi wa ustawi wa jamii ilikinganishwa na inavyohitajika kufikia Lengo namba 8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu kazi nzuri na ukuaji wa uchumi. Nchini Ethiopia, asilimia 60 ya wafanyakazi wa sekta ya ustawi wa jamii waliohojiwa walisema hawana mafunzo husika. Nchi nyingine zinaongeza juhudi za mafunzo: Uchina ina lengo la kuwa na wafanyakazi wapya 230,000 wa usatwi wa jamii kufikia 2020. Nchini Afrika Kusini, idadi ya wafanyakazi wa ustawi wa jamii imeongezeka kwa asilimia 70 kati ya miaka ya 2010 na 2015.

Kwa kuwa zaidi ya nusu ya idadi ya watu dunia wanaishi mijini, kutimiza Lengo namba 11 la Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu miji na jamii endelevu kunahitaji wajuzi wa mipango mijini ili kuboresha makazi yasiyo rasmi na kujiandaa kwa ongezeko la baadaye. Nchi nyingi zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa wataalamu wa mipango (Mchoro wa 17). India inahitaji wataalamu 300,000 wa mipango ya miji na nchi kufikia mwaka wa 2031; mnamo 2011, ilikuwa na takriban wataalamu 4,500. Juhudi za mipango zinafaa kujumuisha mipango ya mandhari, mazingira na mipango ya kijamii, ikiwa ni pamoja na elimu. Viongozi wa ngazi za chini katika nchi ikiwa ni pamoja na Malawi, Msumbiji na Namibia wanahitaji kuboresha uwezo wa kupanga.

Ili kufikia Lengo 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu amani, haki na taasisi thabiti, elimu ya maofisa wa utekelezaji wa sheria na mafunzo yanahitaji kuboreshwa ili kusaidia kujenga imani na kupunguza upendeleo na utumiaji wa nguvu. Nchini Marekani, mafunzo ya kawaida ya polisi huchukua wiki 19, ikilinganishwa na wiki


130 nchini Ujerumani. Asilimia 1 pekee ya idara za polisi nchini Marekani ndizo zinahitaji shahada ya chuo kikuu cha miaka minne; maafisa wenye shahada ya chuo kikuu wameonekana kuwa na uwezekano mdogo wa kutumia nguvu. Nchi nyingine, ikiwa ni pamoja na Singapore, zimetumia mafunzo ili kuzuia ufisadi miongoni mwa polisi; nyingine, kama Indonesia, zimeshirikiana na washirika wa kimataifa ili kuongeza uwezo wa kitaalamu wa polisi.

Inakadiriwa kuwa watu bilioni 4 ulimwenguni kote hawana haki, hivyo kuashiria haja ya kujenga uwezo wa kisheria. Elimu kuhusu mifumo ya mahakama inatofautiana kati ya nchi. Mafunzo ya kawaida huchukua miaka mitatu hadi mitano, lakini shahada ya sheria sio lazima ili kuwa hakimu, hata katika nchi za kipato cha juu. Nchi nyingine, ikiwa ni pamoja na Ufaransa, hutoa mafunzo ya kina ya kitaaluma mara baada ya majaji kuchaguliwa. Nchi kama vile Ghana na Jordan zina taasisi za elimu endelevu kwa majaji.

**MCHORO WA 17:**

**Kuna wapanga mijiwachache sana katika Afrika na Asia**

*Idadi ya wapanga miji kwa watu 100,000 na viwango vya ukuaji wa miji, nchi zilizochaguliwa*





*GEM StatLink*: http://bit.ly/fig18_2
*Kumbuka*: Takwimu ni za mwaka 2011 kwa idadi ya wapanga miji na 2014 kwa viwango vya ukuaji wa miji.
*Vyanzo*: UNDESA (2014); UN-Habitat (2016b).

# Ufadhili

Vyanzo vitatu vikuu vya fedha za elimu ni serikali, wafadhili na kaya husika. Uchambuzi wa ripoti hii unakadiriwakuwa matumizi ya kila mwaka kwa elimu ni dola trilioni 4.7 za Marekani duniani kote. Kati ya hizo, dola trilioni 3 (asilimia 65 ya jumla) hutumiwa katika nchi za kipato cha juuna dola bilioni 22 za Marekani (asilimia 0.5 ya jumla) zikitumiwa katika nchi za kipato cha chini **(Mchoro wa 18a)**, ingawa vikundi hivi viwili vya nchi vina idadi sawa vya watoto wenye umri wa kwenda shule. Serikali zinachangia asilimia 79 ya jumla ya matumizi huku kaya zikichangia asilimia 21. Wafadhili huchangia asilimia 12 ya jumla matumizi ya elimu katika nchi za kipato cha chini na asilimia 2 katika nchi za chini miongoni mwa zilizo na kipato cha kati **(Mchoro wa 18b).**

> “Matumizi ya kila mwaka kwa elimu ni dola trilioni 4.7 za Marekani duniani kote. Kati ya hizo, asilimia 65 hutumiwa katika nchi za kipato cha juu”

**MCHORO WA 18:**
**Serikali huchangia dola nne kati ya tano zinazotumika katika elimu**




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig19_1
*Kumbuka:* Uchanganuzi unategemea vigezo vitatu: (a) kwa nchi ambazo hazina data ya matumizi ya umma, kiasi kimehesabiwa kutokana na Pato la Taifa, kiasi cha Pato la Taifa kinachogharimia matumizi ya taifa na sehemu ya wastani wa matumizi ya umma yaliyotengewa elimu katika kikundi husika cha kipato cha nchi; (b) asilimia 60 ya matumizi ya misaada huchukuliwa kuwa imetumika katika bajeti ya umma (kwa hivyo imetolewa kwenye matumizi ya serikali), asilimia 40 inayobaki ikiwa imetengewa matumizi mengine; na (c) kiasi cha jumla ya matumizi ya kaya kinachotengewa elimu kinakadiriwa kuwa asilimia 18 katika nchi za kipato cha juu, asilimia 25 katika nchi za kipato cha kati na asilimia 33 katika nchi za kipato cha chini.
*Chanzo:* Uchanganuzi wa timu ya ripoti ya GEM.

# Matumizi ya fedha za umma

Ulimwenguni, elimu ya umma ilitumia wastani wa asilimia 4.4 ya Pato la Taifa mwaka 2017, matumizi haya ni juu ya kiwango cha chini ambacho ni asilimia 4 kama ilivyotajwa katika Mpango wa Elimu wa 2030; kulingana na kanda, utumiaji ni asilimia 3.4 Mashariki na Kusini ya nchi za Asia Kusini Mashariki hadi asilimia 5.1 katika mataifa ya Amerika Kusini na Karibi. Sehemu ya wastani wa matumizi ya umma iliyotengewa elimu ilikuwa asilimia 14.1, ambacho ni chini ya kima cha chini cha asilimia 15, viwango vya kikanda vikiwa asilimia 11.6 Ulaya na Amerika Kaskazini hadi asilimia 8 Amerika Kusini na Karibi. Kwa jumla, nchi 43 kati ya 148 hazijatimiza vigezo vyovyote.

Wastani wa matumizi ya elimu ya umma iliyotengewa elimu ya msingi ni asilimia 35, inatofautiana kutoka asilimia 47 katika nchi za kipato cha chini hadi asilimia 26 katika nchi za kipato cha juu. Wastani wa kimataifa wa asilimia 35 ya matumizi ya jumla ya elimu yalitengewa elimu ya sekondari; kiwango hicho kinatofautiana kutoka asilimia 27 katika mataifa yenye kipato cha chini hadi asilimia 37 katika nchi za kipato cha juu. Nchi za Ulaya na Amerika Kaskazini hutumia kiasi sawa kwa mwanafunzi wa msingi na wa sekondari. Mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara hutumia mara 10 zaidi kwa wanafunzi walio katika elimu ya baada ya sekondari ikilinganishwa na mwanafunzi wa shule za msingi.

Mijadala ya umma mara nyingi huangazi athari hasi za uhamiaji kwenye ustawi wa jamii ya wenyeji. Kwa upande mmoja, kuna uwezekano mkubwa wa wahamiaji waliotimiza umri wa kufanya kazi kuzalisha kodi chache ya mapato wakilinganishwa na wenyeji wao kwa sababu wana kipato cha chini. Kwa upande mwingine, wahamiaji wana uwezekano mkubwa wa kutegemea ruzuku za jamii na kutumia huduma za umma, kama vile elimu. Hata hivyo, uwekezaji wa elimu ya umma kwa ajili ya watoto wahamiaji inafaa kuchukuliwa kuwa uwekezaji: Kwa kawaida wanachangia zaidi katika kodi na mfuko wa usalama wa jamii zaidi ya wanavyopokea katika maisha yao. Athari za kifedha kutokana na uhamiaji si kubwa mno – kwa kawaida haizidi asilimia 1 ya Pato la Taifa, iwe chanya au hasi.

# Matumizi ya msaada

Mwaka 2016, misaada kwa elimu ilifikia kiwango chake cha juu tangu kumbukumbu zilipoanza kuwekwa mwaka 2002. Ikilinganishwa na mwaka 2015, misaada kwa elimu ilikua kwa dola bilioni 1.5 za Marekani, au asilimia 13 kwa uhakika, kufikia dola bilioni 13.4. Misaada ya elimu ya msingi ilikuwa theluthi mbili ya ongezeko hili; misaada ya elimu ya sekondari na elimu ya baada ya sekondari iliongezeka kwa kiwango cha chini, hivyo mgawo wa elimu ya msingi katika misaada ya elimu kwa jumla ulifikia kima cha juu cha asilimia 45.

Utoaji wa misaada kwa elimu ya msingi bado haijatengewa nchi zilizo na mahitaji kabisa. Kiwango cha misaada ya elimu ya msingi kwa nchi za kipato cha chini kimeshuka kutoka asilimia 36 mwaka 2002 hadi asilimia 22 mwaka 2016. Mgawo kwa nchi zenye maendelea madogo ulikuwa asilimia 34 mwaka 2016, kutoka kiwango cha juu cha asilimia 47.


> “Kiwango cha misaada ya elimu ya msingi kwa nchi za kipato cha chini kimeshuka kutoka asilimia 36 mwaka 2002 hadi asilimia 22 mwaka 2016”

Nchi za chini miongoni mwa zenye kipato cha kati pia zinakabiliwa na pengo la fedha. Mikopo ya mashirika kadhaa ya kimataifa kwa serikali moja kwa ajili ya maendeleo ya elimu katika nchi hizi pia inasalia kuwa chini. Kwa mfano, mgawo wastani kwa ajili ya elimu kati ya 2002 na 2017 ilikuwa ya asilimia 10.5 kwa mikopo yenye masharti nafuu kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (IDA) huku ikiwa asilimia 6.4 tu ya mikopo isiyo ya masharti nafuu kutoka Benki ya Kimataifa ya Ujenzi na Maendeleo (IBRD). Aidha, mgawo wa elimu katika mikopo ya IBRD umeshuka kutoka asilimia 8.2 mwaka 2012 hadi asilimia 4.7 mwaka 2017, au robo ya mgawo wa sekta ya nishati na uchimbaji wa mali asili (Mchoro wa 19). Mazungumzo yanaendelea kuhusu pendekezo la Tume ya Kimataifa ya Kufadhili Fursa za Elimu Duniani ili kuanzisha Mfuko wa Kimataifa wa Elimu ili kuongeza mikopo ya benki kwa ajili ya maendeleo kwa elimu katika nchi za chini miongoni mwa zilizo na kipato cha kati.

**MCHORO WA 19:**

**Kiwango kidogo na kinachoendelea kupungua cha mikopo ya Benki ya Dunia isiyo ya masharti huenda kwa elimu**

*Mgawo wa jumla wa mikopo ya IDA na IBRD, kulinganisha elimu na sekta ya nishati na uchimbaji, 2002–2017*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig19_9
*Chanzo:* Uchambuzi wa timu ya Ripoti ya GEM kulingana na ripoti mahususi za kila mwaka ya Benki ya Dunia.

## KUTUMIA MISAADA KAMA CHOMBO CHA KUPUNGUZA UHAMIAJI

Wazo kwamba msaada wa nje unaweza kupunguza uhamiaji umepokea uungwaji mkono miongoni mwa watunga sera. Kuongeza mapato ya kutosha katika nchi za asili kunaweza kupunguza kichocheo kikuu cha uhamiaji. Ajenda ya Ulaya kuhusu Uhamiaji na sera za misaada kwa baadhi ya nchi zinaunga mkono wazo hilo.

Utafiti kuhusu mielekeo ya uhamiaji kutoka nchi 210 za asili kwenda nchi 22 za wafadhili (hatima) unaonyesha kwamba nchi zinazopeleka idadi kubwa ya wahamiaji zilipata kiasi kikubwa cha misaada ya kigeni. Hata hivyo,kinachoathiriwa na uhusiano huo ni vigumu kutambua. Misaada ikifikia familia masikini, inaweza kuwasaidia kupata fedha za uhamaji. Misaada pia inaweza kuongeza habari kuhusu nchi za wafadhili na kupunguza gharama za wahamiaji na hivyo kuhamasisha uhamiaji. Kwa hivyo, watunga sera wanafaa kudhibiti matarajio kuhusu uwezo wa misaada kusaidia katika kudhibiti uhamiaji.

> “Si rahisi kutambua kinachoathiriwa na uhusiano kati ya misaada ya kimataifa na wahamiaji wanaofika”

Athari ya misaada ya elimu, hasa kwa uhamiaji, ni vigumu sana kubainisha kutokana udogo wake. Hata kama msaada wa elimu huchangia kupunguza uhamiaji, hauwezi kufanya hivyo haraka. Hata hivyo, elimu inaweza kuwa na jukumu muhimu la kupatanisha katika uhamiaji kwa nchi za asili na zinazopokea watu. Uchunguzi wa mwelekeo wa uhamiaji kutoka nchi za Kaskazini mwa Afrika kuelekea OECD uliashiria kuwa ukuaji wa mapato kutokana na misaada katika nchi za asili ulikuwa msukumo kwa wahamiaji wenye elimu ya chini. Lakini kuridhika na huduma za umma za nchini, ikiwa ni pamoja na shule, zinaweza kuzuia uhamiaji. Kwa ujumla, sifa za watu katika nchi inayopokea wahamiaji – wanakoelekea wahamiaji, ukuaji wa idadi ya watu mijini, uwiano wa umri na utegemezi – na manufaa ya elimu katika nchi zinazopokea watu zilikuwa vishawishi vikuu katika viwango vya uhamiaji kuliko viwango vya misaada.

## KUBORESHA UFANISI WA MISAADA YA KIBINADAMU KATIKA ELIMU

Misaada ya kibinadamu iliongezeka mwaka 2017 kwa mwaka wa nne mfululizo, huku ufadhili wa kimataifa wa kibinadamu kwa elimu ukifikia dola milioni 450 za Marekani. Hata hivyo, mgawo wa elimu katika jumla ya misaada

ya kibinadamu ilikuwa asilimia 2.1 ambao uko chini sana ya lengo la angalau asilimia 4. Kwa muda sasa, elimu imekuwa mojawapo ya sekta zinazopokea ufadhili mdogo wa kifedha, ikilinganishwa na sekta nyinginezo. Hata hivyo, Mkutano wa Ulimwengu wa Misaada ya Kibinadamu wa 2016 ulijumuisha ahadi mpya kwa elimu katika dharura kwa kuanzishwa kwa mfuko wa kimataifa wa Elimu Haiwezi Kusubiri (ECW).

Mifumo kadhaa ya ushirikishaji, ya wima (kimataifa hadi vijijini) na uelekeo sawa (kati ya sekta na watendaji), hufanya usanifu wa misaada ya kibinadamu na uchangiaji wake kuwa mgumu katika kuongeza sehemu ya elimu kwenye uitikiaji wa dharura. Usaidizi wa Umoja wa Mataifa huandaliwa kwa njia mbili. Mipango ya misaada ya kibinadamu (HRP) hutumia mkakati ya nchi, kwa kawaida kwa zaidi ya mwaka mmoja. Maombi ya msaada wa haraka hutaka uitikiaji kwa dharura ili kushughulikia mahitaji ya papo hapo zaidi ya miezi mitatu hadi sita. HRP zina maudhui machache yanayohusiana na elimu, isitoshe aghalabu elimu haijazingatiwa sana katika maombi ya msaada.

Hakuna mfumo wa kuripoti wa lazima kuhusu matumizi ya misaada ya kibinadamu kimataifa, hivyo ni vigumu kufuatilia matumizi katika elimu. Hifadhidata ya Mfumo wa Kamati ya Msaada wa Maendeleo ya Wakala wa OECD haina uchanganuzi wa data kuhusu misaada ya kibinadamu kulingana na sekta, ingawa inadokeza kuwa karibu dola milioni 400 za Marekani za msaada wa maendeleo zilitumiwa kugharamia elimu ya wakimbizi katika mwaka wa 2016. Ofisi ya kujitolea ya Umoja wa Mataifa ya Uratibu wa Ufuatiliaji wa Fedha za Mipango ya Misaada ya Kibinadamu hufuatilia elimu, lakini asilimia 42 ya fedha mwaka 2017 iliendea sekta mseto, ikagawanywa miongoni mwa sekta au au haikubainishwa. Hivyo kusababisha makadirio ya matumizi ya elimu yasiyo sahihi.

Ufadhili usiotosha elimu unatokana na uhaba katika maeneo kadhaa yakiwemo, nia ya kisiasa, ushirikishaji wa mwelekeo wima na usawa, uwezo wa wahusika wa misaada ya kibinadamu na maelezo au taratibu za uwajibikaji.

Utafiti wa gharama uliofanywa mwaka wa 2015 ulipata pengo la ufadhili wa dola bilioni 8.5 za Marekani, ambalo linafaa kuzibwa na jumuiya ya kimataifa. Hii ni sawa na dola 113 za Marekani kwa kila mtoto, hili ni ongezeko la mara kumi katika matumizi ya kila mwanafunzi. ECW inalenga kuongeza dola bilioni 1.5 za Marekani kwa mwaka na kuongeza mgawo kwa elimu katika misaada ya kibinadamu kwa asilimia 1.2 kufikia 2021. Washirika wake watahitaji kushiriki juhudi za kukusanya fedha, ama kuwezesha malengo ya kibinadamu katika misaada ya maendeleo au kuongeza kipaumbele cha elimu ndani ya misaada ya kibinadamu.

Mipango haipaswi kutegemea shughuli ambazo mashirika yamezoea kutekeleza; badala yake, kuna haja ya kuwa na vitendo ambavyo vinaleta elimu jumuishi yenye usawa wa ubora mzuri. Kundi la Elimu Ulimwenguni limeanzisha mwongozo wa kutathmini mahitaji. Kama mdau mkuu mpya, ECW inaweza kutekeleza miongozo hii kwa kuwataka washirika kuitumia katika usanifu wa mipango na kuendeleza uwezo wao.

Misaada ya kibinadamu imekuwa na changamoto ya kuiratibu ndani na nje ya watendaji wakuu. Elimu inapaswa

Ili kukidhi hata mahitaji ya msingi zaidi ya elimu ya watoto walio katika migogoro kutahitaji mgawo wa sekta elimu katika misaada ya kibinadamu kuongezeka...



kuwa kiungo muhimu katika mipango ya misaada ya kibinadamu inayohusu sekta mbalimbali. Katika mgogoro wa Rohingya nchini Bangladesh, elimu ilijumuishwa kutoka hatua ya kwanza ya utoaji wa misaada, utoaji wa huduma za elimu ulianza haraka sana. Hata hivyo, mara nyingi ukosefu wa uratibu ulisababisha baadhi ya vituo vya kujifunza kuwa bila wahudumiwa, kwani huduma zisizo za elimu zilichukua muda wa watoto.

Mipango ya pamoja inahitajika kati ya watendaji wa misaada ya kibinadamu na wa maendeleo. Ingawa mipango inayojumuisha sekta nyingi ilisaidia kujumuisha elimu katika misaada ya kibinadamu katika hali ya Rohingya, haijafanikisha kujumuishwa katika mfumo wa elimu wa Bangladesh. Maombi ya misaada katika migogoro ya muda mrefu imekuwa ikipata ufadhili mdogo, huku mipango ya kitaifa ya elimu ikiwa haijasisitiza kuhusu ustahimilivu au kushughulikia mgogoro. Mipango ya misaada ya kibinadamu kwa elimu kwa muda mfupi inafaa kujumuishwa na masilahi mengine kwa namna iliyopangika, kwa mfano nchini Uganda, ambapo Mpango wa serikali kwa Elimu ya Wakimbizi na Jamii Wenyeji uliotangaza mwezi Mei 2018, umetenga dola milioni 395 za Marekani ili kutumiwa ndani ya miaka mitatu kufikia wakimbizi na wenyeji wapatao 675,000 kwa mwaka.

Mataifa fadhili kama vile Australia, Kanada, Norway na Uingereza yanahamia katika mifumo ya kufadhili miradi ya miaka mingi ili kuhakikisha kwamba washirika wa misaada ya kibinadamu wanauhakika wa ufadhili, ECW ina 'chombo cha ustahimilivu wa miaka mingi,' ambacho pia kinalenga kupunguza pengo lililopo kati ya maendeleo na misaada ya kibinadamu. Uwajibikaji katika misaada ya kibinadamu unahitaji kuimarishwa. ECW imesisitiza uwazi na matokeo kwa kuweka viwango vya juu katika mfumo wake wa matokeo ya kimkakati inayoshughulikia sio tu matokeo ya mwisho bali pia, kwa njia muhimu, jinsi inavyofanya kazi na ufanisi wake wa uendeshaji.


# Matumizi ya kaya

Ukosefu wa data kuhusu michango ya kaya kwa muda mrefu umetatiza uchanganuzi wa jumla ya matumizi yanayoenda kwenye elimu. Kwa mara ya kwanza, UIS ilitoa data ya kaya mwaka 2017, lakini hata hivyo ufikiaji wa kaya ungali mdogo. Idadi ya kaya zilizo katika uchanganuzi wa matumizi katika elimu inaweza kuwa ya juu sana katika baadhi ya nchi za kipato cha chini na za kati, kwa mfano El Salvador (asilimia 50) na Indonesia (asilimia 49) **(Mchoro wa 20)**.

**MCHORO WA 20:**

**Kiasi cha matumizi ya kaya kwa ajili ya elimu ni kikubwa katika baadhi ya nchi za kipato cha chini na za kati**

*Asilimia ya Pato la Taifa linalotumika kwa ajili ya elimu kutegemea chanzo cha fedha na kundi la mapato ya nchi, nchi zilizochaguliwa, 2013–2017*




*GEM StatLink:* http://bit.ly/fig19_13
*Chanzo:* hifadhidata ya UIS.

Kwa ujumla, takwimu za matumizi ya kaya hazionekani kubadilika pakubwa sana mwaka baada ya mwaka, ingawa kuna matukio yaliyo tofauti. Nchini Chile, maandamano makubwa ya wanafunzi kuhusu upungufu wa ufadhili wa serikali katika sekta ya elimu ya serikali umesababisha mabadiliko katika sera ya umma. Kwa sababu hiyo, mgao wa matumizi ya kaya kwa elimu imepungua kati ya 2005 na 2015 kutoka karibu asilimia 50 hadi chini ya asilimia 20.

# Mapendekezo

Ripoti hii inaziomba serikali kushughulikia mahitaji ya elimu ya wahamiaji na watu waliofurushwa makwao, pamoja na mahitaji ya watoto wa watu hawa, kwa umakini sawa na wanaowapa wenyeji.

## KULINDA HAKI YA ELIMU KWA WAHAMIAJI NA WALIOFURUSHWA MAKWAO

Kanuni ya kutobaguliwa katika elimu inatambuliwa katika mikataba ya kimataifa. Vikwazo vya ubaguzi, kama vile mahitaji ya cheti cha kuzaliwa, lazima ikataliwe kabisa katika sheria ya kitaifa. Kanuni zilizopo hazipaswi kuwa na mianya au maeneo yasiyo na maelezo ya kutosha yanayoweza kufasiriwa kwa vyovyote na watu binafsi au maofisa wa shule. Serikali ni sharti zilinde haki ya wahamiaji na wakimbizi kupata elimu bila kujali hati zao za utambulisho au hali ya makazi na zinafaa kutumia sheria bila ubaguzi.

Kuheshimu haki ya elimu ni sharti kuwe zaidi ya sheria na michakato ya utawala. Mamlaka za kitaifa zinafaa kuanza kampeni za kuhamasisha jamii za wahamiaji na wakimbizi kuhusu haki zao na taratibu za kujisajili shuleni. Mamlaka inayofanya mipangilio inatakiwa kuhakikisha kuwa kuna shule za umma zinazoweza kufikiwa kutoka makazi yasiyo rasmi na makazi duni na kwamba hazipuuzwi katika mipango ya kuboresha mijini.

## JUMUISHA WAHAMIAJI NA WALIOFURUSHWA MAKWAO KATIKA MFUMO WA TAIFA WA ELIMU

Baadhi ya mifumo ya elimu huwachukulia wahamiaji na wakimbizi kama watu wa muda mfupi au wanaopita, tofauti na wenyeji. Kufanya hivyo si vizuri; kunazuia maendeleo ya jamii hizo kielimu, kijamii na fursa za baadaye, pia kunadhoofisha juhudi za kuwa na jamii mseto zenye mshikamano. Sera ya umma lazima iwajumuishe katika ngazi zote za elimu ya kitaifa.

Kuwajumuisha wahamiaji kunaweza kufanyika kwa njia kadhaa. Ingawa kujipata katika lugha mpya ya mafundisho kunahitaji masomo ya maandalizi, wanafunzi hawapaswi kutenganishwa na wenyeji wao kadiri iwezekanavyo. Mifumo ya elimu haifai kuwapeleka wanafunzi walio na ufanisi wa chini, miongoni mwao wahamiaji, katika madarasa tofauti. Kutokana na mkusanyiko wa kijiografia wa wanafunzi wahamiaji ilivyo katika nchi nyingi, wanaofanya mipango ya elimu wanapaswa kutumia mbinu kama vile ruzuku za usafiri na kuwatengea wanafunzi shule ili kuhakikisha mipaka inayotokana na makazi haisababishi ubaguzi katika elimu.

Serikali zinatakiwa kuhakikisha kwamba elimu kwa wakimbizi haisumbuliwi kadri iwezekanavyo. Ingawa matukio ya kipekee – wakimbizi kuwekwa katika makazi yao kando au vikwazo vya kutokuwa na uwezo kwa wenyeji – yanaweza kuzuia ujumuishaji kamili, serikali zinatakiwa kupunguza muda unaotumiwa katika shule zisizofuata mtalaa wa kitaifa au hazielekei katika kupata vyeti tambuliwa, kwa sababu kufanya hivyo huleta matokeo hasi katika elimu.

## KUELEWA NA KUPANGA KWA AJILI YA MAHITAJI YA ELIMU YA WAHAMIAJI NAWALIOFURUSHWA

Nchi zilizo na idadi kubwa ya wahamiaji na wakimbizi zinahitajika kuchukua data kuhusu watu hao katika mifumo ya usimamizi wa taarifa ili kupanga na kuweka bajeti ipasavyo. Kutenga nafasi katika shule au nafasi za ajira kwa wahamiaji na wakimbizi ni hatua ya kwanza ya ujumuishaji.

Mazingira ya shule yanafaa kubadilishwa na kuboreshwa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi. Wanaoingia katika mifumo iliyo na lugha mpya ya mafundisho wanahitaji elimu saidizi kutoka kwa walimu waliohitimu. Wale ambao elimu yao ilikatizwa watafaidika ikiwa kuna mipango ya elimu ya kasi ili kuwawezesha kurejelea na kuingia tena shuleni katika kiwango kinachofaa. Kujumuishwa kwa wakimbizi katika elimu kuna uwezekano mkubwa wa kufanikiwa ikiwa kutajumuisha huduma za ustawi wa jamii kwa wakimbizi, kwa mfano, kupata ruzuku ya kifedha yenye masharti ili kugharimia ada zisizo za moja kwa moja za shule. Ikiwa ni wahamaji wa ndani, hususan watoto wa jamii za kuhamahama au wafanyakazi wa msimu, ni bora kwa serikali kuzingatia kalenda za shule zinazofaa, mifumo ya kufuatilia elimu na mitalaa inayohusiana na maisha ya wahusika.

Watu wazima wanahitaji usaidizi ili kuendeleza ujuzi wao kwa njia ya elimu na mafunzo ya kiufundi na ili kujikwamua vikwazo, kama vile kazi za ujuzi wa chini au gharama za juu za mafunzo, ambazo huwazuia kuwekeza katika ujuzi. Wanahitaji mipango ya elimu ya kifedha ili waweze kusimamia hali zao za kiuchumi, kutuma fedha zaidi nyumbani na kuepuka kudanganywa au unyonyaji wa kifedha. Mipangoya elimuya nje ya darasa, inayoweza kutolewa katika ngazi ya serikali za mitaa, inaweza kuongeza juhudi za kuimarisha ujumuishaji wa kijamii.

## WAKILISHA HISTORIA YA UHAMIAJI NA KUFURUSHWA KATIKA ELIMU KWA USAHIHI ILI KUKABILIANA NA UBAGUZI

Kujenga jamii jumuishi na kuwasaidia watu kuishi pamoja kunahitaji zaidi ya uvumilivu. Serikali zinapaswa kurekebisha maudhui ya elimu na ufundishaji, kurekebisha mitalaa na kufanya vitabu vya kiada upya ili kuakisi historia na uanuwai uliopo. Maudhui ya elimu yanafaa kuangazia mchango wa wahamiaji katika utajiri na ustawi. Pia inafaa kutambua sababu za mvutano na migogoro, pamoja na historiaya masuala yaliyosababisha watu kuhamishwa au kubaguliwa. Mbinu za ufundishaji zinafaa kukubali mitazamo mingi, kukuza maadili ya kuishi pamoja na kufahamu faida za kuwa na watu wa jamii anuai katika jamii. Zinafaa kupinga kasumba na kuendeleza ujuzi muhimu wa kufikiri ili wanafunzi waweze kuondoa shaka ya kutagusana na tamaduni nyingine na kupuuza picha hasi inayoonyeshwa na vyombo vya habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi. Serikali zinafaa kukopa na kuzingatia destruri nzuri za elimu inayoendeleza mtagusano wa tamaduni.

## KUANDAA WALIMU WA WAHAMIAJI NA WAKIMBIZI KUSHUGHULIKIA TOFAUTI NA CHANGAMOTO

Walimu wanahitaji msaada wa kuwa wachocheaji wa mabadiliko katika mazingira ya shule yanayozidi kuathiriwa na uhamiaji na ufurushwaji.

Mipango ya elimu ya sasa ya walimu inayohusu uhamiaji unaonekana kuwa ya sadfa na isiyo sehemu ya mtalaa mkuu. Serikali zinafaa kuwekeza katika elimu ya awali na inayoendelea ya mwalimu ili kujenga ujuzi wa msingi na uwezo wa kusimamia mazingira mbalimbali, lugha mbalimbali na miktadha ya tamaduni mseto, ambayo pia huathiri wanafunzi wenyeji. Kuongeza uelewa wa walimu wote kuhusu uhamiaji na ufurushwaji, si tu kwa wanaofundisha madarasa yenye wanafunzi wa asili mbalimbali. Walimu watarajiwa na walimu wanaofanya kazi na viongozi wa shule wanapaswa kupewa zana za kukabiliana na mitazamo hasi, chuki na ubaguzi katika darasa, shule na jamii, na kuimarisha kujiamini na kuhisi ukaribisho miongoni mwa wanafunzi wakimbizi.

Walimu walio katika mazingira ya wahamiaji pia wanahitaji kufahamu matatizo fulani ya wanafunzi na wazazi waliofurushwa makwao na watagusane na jamii hizo. Wakati walimu si washauri, wanaweza kufundishwa kutambua msongo wa mawazo na dhiki na kuwaelekeza wanaohitaji usaidizi wa wataalamu. Ikiwa hakuna wataalamu, walimu wanapaswa kuwa tayari kutoa huduma hizo kwa familia. Walimu wa wakimbizi na walimu waliokimbia makazi yao hupata msongo wa mawazo wao wenyewe. Sera za usimamizi zinahitaji kutambua na kupunguza matatizo magumu ambayo baadhi ya walimu hufanyia kazi; kusimamia na kuhakikisha usawa kati ya aina za wataalamu wa kufundisha ili kudumisha motisha; na kuwekeza katika maendeleo ya kitaaluma.

## KUTUMIA UWEZO WA WAHAMIAJI NA WATU WALIOFURUSHWA MAKWAO

Wahamiaji na wakimbizi wana ujuzi ambao unaweza kusaidia kubadilisha maisha yao wenyewe na familia zao, lakini pia uchumi na jamii za kwao au za wenyeji, iwe wanarudi au wasaidie kutoka mbali. Kutumia uwezo huu kunahitaji mifumo rahisi, nafuu na ya wazi zaidi ya kutambua sifa na ujuzi wa kitaalamu (ikiwa ni pamoja na ule wa walimu) na kutoa maelezo kuhusu mafunzo ya awali ambayo hayakuthibitishwa au kupatiwa cheti.

Nchi zinafaa kuzingatia ahadi za Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji Salama, wenye Utaratibu na wa Mara kwa Mara katika kutambua kufuzu na kuhitimisha mazungumzo chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Kutambuliwa kwa Elimu ya Juu ili iweze kuidhinishwa mwaka 2019. Mashirika ya kutathmini, ya kutoa leseni na taasisi za kitaaluma zinapaswa kusawazisha mahitaji na taratibu katika viwango baina ya mataifa, kikanda na kimataifa, kufanya kazi na serikali na mashirika ya kikanda na ya kimataifa. Viwango sawa vya shahada, utaratibu wa kuhakikisha ubora na mipango ya uhamiaji kwa ajili ya masomo inaweza kusaidia kutambua sifa.

## JUMUISHA MAHITAJI YA ELIMU YA WAHAMIAJI NA WALIOFURUSHWA MAKWAO KATIKA MISAADA YA KIBINADAMU NA YA MAENDELEO

Ingawa theluthi mbili ya wahamiaji wa kimataifa wanaelekea nchi za kipato cha juu, wakimbizi 9 kati ya 10 huenda katika nchi za kipato cha chini na cha kati, ambazo zinahitaji usaidizi kutoka kwa washirika wa kimataifa. Kutimiza mahitaji kunahitaji kuongezeka mara kumi kwa sehemu ya misaada ya kibinadamu iliyotengewa elimu. Suluhisho endelevu zaidi ni kwa jumuiya ya kimataifa kutimiza ahadi za Mkataba wa Kimataifa juu ya Wakimbizi na Mwongozo wa Kina wa Kukabiliana na Suala la Wakimbizi za kuelekeza misaada ya kibinadamu na maendeleo kutoka hatua za mwanzo za mgogoro, kusaidia utoaji wa elimu jumuishi kwa wenyeji na wakimbizi. Elimu inapaswa kujumuishwa katika kubuni mikakati ya kukabiliana na masuala haya, hasa elimu ya chekechea na utunzaji wa watoto wachanga. Pia inapaswa kuwa sehemu ya kifurushi cha jumla cha masuluhisho yanayohusisha sekta nyingine, kwa mfano malazi, lishe, maji, usafi wa mazingira na ulinzi wa kijamii. Wafadhili wanahitaji kujumuisha marekebisho haya katika msaada wanaotoa wa kibinadamu. Kwa kutumia kasi ya mfuko wa Elimu Haiwezi Kusubiri, wanahitaji kubuni uwezo wa kutathmini mahitaji na waunganishe juhudi za kupanga ili wazibe mwanya uliopo katika maendeleo ya kibinadamu na wachochee kupatika kwa fedha zinazogharamia miaka mingi na ambazo kupatikana kwake kunaweza kutabirika.

# Uhamiaji, ufurushwaji na elimu:

## KUUNGANISHA JAMII BADALA YA KUIGAWANYA

Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu ya mwaka wa 2019 inachunguza athari za uhamiaji na ufurushwaji katika elimu katika aina zote za kuhama: ndani na nje ya nchi, kwa hiari na kwa kulazimika, ili kutafuta ajira na elimu. Pia inakagua maendeleo katika elimu katika Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu.

Kutokana na kuongezeka kwa uanuwai, ripoti hii inachunguza jinsi elimu inaweza kujenga jamii zenye umoja na kusaidia watu wasiwe tu wanastahimiliana bali wajifunze kuishi pamoja. Elimu imeyotolewa kwa usawa huleta watu pamoja; kutokuwa na usawa huendeleza utengano kati ya wahamiaji na wakimbizi na wenyeji.

Mikataba miwili mpya ya kimataifa juu ya wahamiaji na wakimbizi inatambua jukumu la elimu na kuweka malengo yanayoambatana na ahadi ya kimataifa ya kujumuisha wote. Ripoti hii ni chombo kwa mikataba hii. Inajadili masuala ya sera ambayo yanagusia wahamiaji wa msimu, uunganishaji wa shule za vijijini, mitalaa inayohimiza mtagusano wa tamaduni, kujumuisha wakimbizi katika mifumo ya kitaifa ya elimu na kupambana na ubaguzi, kutambua viwango vya kuhitimu, kugawia shule fedha kwa umakini, matumizi bora ya msaada unaotengewa elimu na walimu kuwa tayari kufundisha madarasa yenye uanuwai.

Ripoti hii inaomba nchi kuona elimu kama chombo cha kukabiliana na uhamiaji na ufurushwaji na nafasi kwa wale wanaohitaji elimu.

*Elimu ni haki ya kila binadamu na inachangia pakubwa katika kumaliza umaskini, kuleta maendeleo endelevu na amani. Watu wanaohama, iwe kwa sababu za kikazi au elimu, iwe wamejiamulia au wamelazimika, pia wana haki ya kupata elimu. Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu, 2019 inatilia mkazo uwezo mkubwa na nafasi nyingi zinazotokana na kuhakikisha wahamiaji na waliofurushwa makwao wamepata elimu bora.*

**António Guterres, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa**

*Ripoti hii inakusanya ushahidi uliopo juu ya uhamiaji na elimu ili kuchora taswira inayoonyesha fursa ya ajabu, pamoja na kuonyesha mahali na sababu zinazoweza kunyima fursa ya kupata elimu. Inafanya hivi wakati ambapo jumuiya ya kimataifa inajitahidi kufikia malengo ya SDG na kuongeza faida nyingi za uhamaji duniani kote..*

**William Lacy Swing, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (Oktoba 1, 2008 hadi Septemba 30, 2018)**

*Ripoti hii inatoa mtazamo thabiti wa kutilia mkazo elimu katika Mkataba wa Kimataifa juu ya Wakimbizi na umuhimu wa kujumuisha wakimbizi katika mifumo ya kitaifa ya elimu na Mipango ya Sekta ya Elimu.*

**Filippo Grandi, Kamishna Mkuu wa Wakimbizi katika Umoja wa Mataifa**

Global Education Monitoring Report

United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization

Sustainable Development Goals

Sustainable Development Goals

www.unesco.org/publishing • www.unesco.org/gemreport